# Nipashe

Jumatano Machi 11, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580176

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Mfugaji atozwa faini mil. 60/- kwa madai kukiuka sheria mipango miji

UKURASA 4



Siku ya wanawake inapotumiwa kuainisha ajenda za uchaguzi

Ukurasa 14

Wasomi duniani, Mangula walivyomuibua upya Nyerere

Ukurasa 15

siasa

JUMATANO MACHI 11, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Wanajeshi Marekani waanza kuondoka nchini Afghanistan

Ukurasa 17

KATIBA MPYA...

Kuitwa kiporo kilichochacha, kwa nini kuruhusu kichache?

Na Mwandishi Wetu

MCHAKATO wa kuandika katiba mpya ulianza baada ya Rais Jakaya Kikwete, kuteua wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, ambao jukumu lao lilikuwa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu muundo wa katiba wanayoitaka.

Hata hivyo, mchakato huo haukuhitimishwa kwa kuipatia nchi katiba iliyopendekezwa na sauti za umma zinasikika kuuliza lini andiko hilo litapatikana?

Wakati hayo yakizungumzwa, ni wazi kuwa mabilioni ya shilingi yalitumiwa na wajumbe wa tume, bunge la katiba na shughuli nyingine za kufanikisha suala hilo, lakini halikufanikiwa.

Hivi karibuni Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Dk. Bashiru Ally, analipigilia msumari suala hilo, akieleza kuwa katiba mpya ni kiporo kilichochacha na hakifai kupasha moto kwa namna yoyote.

Mtendaji Mkuu wa CCM ana-

INAENDELEA UK.16

Katibu Mkuu wa CCM, Bashiru Ally. PICHA: MTANDAO

Pérez de Cuéllar Katibu Mkuu aliyeacha alama zisizofutika UN

Ukurasa 19

William Ruto anapokandamizwa na utata wa kifo cha mlinzi wake Ukurasa 20

UKURASA 13

# HUKUMU

**MBOWE**, vigogo Chadema kulipa mil. 350/- au jela miezi 5, washindwa kulipa faini, waenda jela...*Endelea ukurasa wa 2*



Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, akijadiliana jambo na Mshauri Mkuu wa chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, katika chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya yeye na wenzake kusomewa hukumu ya kesi ya uchochezi, iliyokuwa ikiwakabili. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## PM AKANA KUFUKUZWA MENEJA WA TANROADS

UKURASA 4

## Membe ahoji mchakato kufukuzwa kwake CCM

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO **SIMBA, SINGIDA MECHI YA REKODI** UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6




Askari Polisi wakiwafukuza waandishi wa habari katika eneo la Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutolewa kwa hukumu ya kesi ya uchochezi iliyokuwa ikiwakabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na wenzake. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Hukumu kina Mbowe jela miezi 5 au faini mil.350/-

**Na Hellen Mwango**

VIGOGO wanane wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti, Freeman Mbowe na aliyekuwa Katibu Mkuu, Dk.Vincent Mashinji (sasa mwana CCM), wamehukumiwa kulipa faini ya jumla Sh. milioni 350 au kwenda jela miezi 5 kila mmoja, baada ya kukutwa na hatia katika makosa 12 ya uchochezi.

Mahakama imewafutia kosa la kula njama na kuwatia hatiani katika makosa 12 ya uchochezi, huku Mbowe peke yake akihukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 70 na Dk. Mashinji Sh. milioni 30.

Hukumu hiyo ilisomwa jana kwa saa tatu na dakika 45 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Hakimu alisema baada ya kupitia ushahidi wa jumla ya mashahidi 13 wa pande zote mbili, mahakama yake imewaona washtakiwa wote wana hatia.

"Dk. Mashinji umeonekana kwenye maandamano, kwa hiyo mahakama hii imekuona wewe pamoja na wenzako mna hatia," alisema.

Hakimu Simba alisema mahakama yake imezingatia kwamba wapo washtakiwa waliofutiwa dhamana na kukaa mahabusu na washtakiwa ambao ni wakosaji wa mara ya kwanza.

"Mahakama hii inawahukumu washtakiwa wote kwa kosa la pili kulipa faini ya Sh. milioni 10 kila mmoja na wakishindwa watakwenda jela kutumikia kifungo cha miezi mitano," alisema.

Katika kosa la tatu na la nne, Hakimu huyo alisema linawakabili washtakiwa wote, hivyo watalipa faini ya Sh. milioni 10 kila mmoja na wakishindwa, watakwenda jela miezi mitano.

"Mbowe utalipa faini ya Sh. milioni 10 kwa kosa la sita, Sh. milioni 10 nyingine ya kosa la nane, Sh. milioni tano kwa kila kosa kwa kosa la 10 na 11 na Sh. milioni 10 kwa kosa la tisa," alisema Hakimu Simba wakati akiendelea kuichambua hukumu hiyo.

Alisema maneno yaliyotamkwa na washtakiwa kwenye kampeni na yalikuwa yameshazuiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iliyokuwa imekataza kauli zisizofaa kwa jamii.

Alisema washtakiwa ni viongozi na walistahili kuwa mfano wa kufuata sheria kwa sababu wao wanashiriki moja kwa moja kuzitunga.

"Mahakama hii inatoa adhabu kali ili iwe fundisho kwa viongozi kama ninyi mnaposimama kwa wananchi," alisema.

Washtakiwa hao walishindwa kulipa faini hiyo, hivyo wote kupelekwa gerezani.

Viongozi mbalimbali wa vyama vingine vya upinzani, walihudhuria mahakamani hapo akiwamo Mshauri Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad na Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia.

Mbali na Mbowe na Dk. Mashinji, washtakiwa wengine ni Katibu Mkuu John Mnyika, Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Zanzibar, Salum Mwalimu na wabunge Mchungaji Peter Msigwa, Halima Mdee, Esther Matiko, John Heche na Esther Bulaya.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya hukumu hiyo, Mbatia alisema mahakama imewatoza faini kubwa, lakini akasisitiza kuwa hana uzoefu na masuala ya sheria. "Wanasheria watatuelekeza nini kifanyike baada ya hukumu, sisi wengine hatuelewi sheria, faini ni kubwa labda wakikata rufani, italeta nafuu kwa washtakiwa," alisema.

Wakili wa utetezi, Peter Kibatala, alisema hawajaridhika na hukumu hiyo kwa sasa wanashughulikia kulipa faini, lakini wana nia ya kukata rufani.

**KESI YENYEWE**

Katika kesi ha msingi, Mbowe na viongozi wenzake walishtakiwa kwa mashtaka 12 ya uchochezi na moja la kula njama.

Mashtaka 12 yaliyokuwa yakiwakabili katika shtaka la kula njama, wanadaiwa kati ya Februari Mosi na 16, 2018, wakiwa Kinondoni Dar es Salaam, kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani kwa kutenda kosa la jinai na kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Bulaya alikuwa anakabiliwa na shtaka la kushawishi kutenda kosa la jinai, ikidaiwa kuwa Februari 16, mwaka huo, katika viwanja vya Buibui, Kinondoni jijini Dar es Salaam, alishawishi wakazi wa Kinondoni kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu.

Katika shtaka ambalo lilikuwa linamkabili Heche peke yake, ilidaiwa kuwa Februari 16 mwaka huo, katika Viwanja vya Buibui, Kinondoni, katika mkutano wa hadhara, Mbunge huyo wa Tarime Vijijini alitoa maneno ya chuki dhidi ya serikali.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi na ulifunga ushahidi ukiwa na mashahidi wanane.

Upande wa Utetezi uliongozwa na Wakili Peter Kibatala na uliita mashahidi watano.

Hati ya mashtaka ya awali ilikuwa na mashtaka 12 yakiwamo ya kufanya mkusanyiko usio halali, lakini hati mpya iliyokuwa kortini, ina mashtaka 13 likiwamo shtaka la kufanya maandamano yasiyo halali wakiwa na lengo la kuvamia Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni.

Nchimbi alidai shtaka la kwanza mpaka la nne linawakabili washtakiwa wote, kwa madai kuwa walikula njama ya kutenda kosa kufanya mkusanyiko usio halali na wenye ghasia.

Nchini alidai shtaka la tano, sita, tisa, 10 na 11 yanamkabili Mbowe, akidaiwa kuhamasisha hisia za chuki, ushawishi wa hali ya kutoridhika na uchochezi.

Mbowe alinukuliwa katika mkutano huo wa Kinondoni akidaiwa kusema: "Tumejipa kibali cha kutangulia mbele ya haki... haiwezekani wanaume wazima na akili zetu na wake zetu na watoto wetu tufanywe ndondocha.

"Hii ni nchi ya ajabu. Mimi leo nipo hapa kuliandaa taifa... Kule Afrika Kusini juzi, jana aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Jacob Zuma amelazimishwa kujiuzulu... Robert Mugabe wa Zimbabwe kang'olewa, Waziri Mkuu Ethiopia juzi ameondolewa kwa people's power, Magufuli ni mwepesi kama karatasi'.

Nchimbi alidai shtaka la nane linamkabili Heche, aliyedaiwa kutoa maneno ya kuonyesha kutokuridhishwa, alipotamka kuwa "kesho patachimbika, upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii, wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano... watu wanapotea.. watu wanauawa, wanaokotwa kwenye mitaro, lazima ukome".

Mshtakiwa Msigwa anashtakiwa katika shtaka la 12, akidaiwa katika tarehe hiyo alishawishi wananchi wa Kinondoni kutembea na silaha mbele ya umma.

Shtaka la 13 linamkabili Bulaya ambaye anadaiwa aliwashawishi wakazi wa Kinondoni kukaidi amri iliyowataka kutawanyika.

**POLISI VS CHADEMA**

Kabla ya hukumu hiyo, jana mchana, Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, alionekana akiongea na polisi kuomba kwenda kuzungumza na wafuasi wa Chadema ambao walipomwona, walishangilia kisha akaanza kuongea nao.

Lema alisema yeye siyo muoga na kwamba mtu hawezi kuwa jasiri bila nidhamu.

"Hapa ni mahakamani, kesi inaendelea sauti yenu inakuja sana, lakini hapa ni barabarani 'attention' (utayari) walioyonayo polisi juu ya kelele na leo ni siku ya hukumu inayomhusisha Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, siyo wasiwasi mdogo ni wa msingi," alisema.

"Hili jambo (hukumu) litokee litakavyotokea hampaswi kuwa na hofu, safari ya ukombozi ina matatizo na majaribu mengi," Lema alisema kisha akakatisha na kiongozi wa polisi aliyemwondoa kwa madai anahutubia.

Lema alitii amri ya kiongozi huyo kwa kuondoka eneo hilo huku akiwasisitiza wafuasi hao wa Chadema kuondoka maana "watatumia".

Muda mfupi baadaye, askari polisi walianza kuwatawanya na kukamata watu kadhaa na kuwapandisha kwenye magari ya polisi, huku wakitangaza hali ya hatari eneo hilo.==

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Hellen Kijo-Bisimba (kushoto), akichangia mada kwenye uzinduzi wa Mtandao wa Watetezi wa Wanawake na Haki za Binadamu Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mkurugenzi wa Mfuko wa Wanawake Tanzania, Mary Rusimbi na Mkurugenzi Mtendaji wa KIWOHEDE, Justa Mwaituka. Habari Uk. 24. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Membe akosoa mchakato wa kufukuzwa CCM

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, amehoji mchakato wa kumvua uanachama uliofanywa na Kamati Kuu (CC), badala ya Halmashauri Kuu (Nec) ya chama hicho.

Pia ameshangazwa na kauli ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally ya kutamani aombe radhi kama wengine huku akihoji afanye hivyo kwa kosa lipi.

Akizungumza na Nipashe, siku chache baada ya kurejea nchini akitokea Afrika Kusini alikokuwa anamuuguza mwanawe tangu uamuzi ulipotolewa dhidi yake wa kumfuta uanachama, alisema anashangazwa uamuzi huo kufanywa na Kamati Kuu badala ya Halmashauri Kuu pamoja na wito wa kuomba msamaha.

"Halmashauri Kuu yaani Nec ndiyo pekee itakayopokea, kujadili na kuamua kama tuna makosa au la. Kamati Kuu haina mamlaka hayo. Kamati Kuu inaweza tu kuweka mapendekezo yake, lakini siyo kutoa uamuzi, uamuzi ni wa Nec."

"Kamati Kuu haikupaswa hata kutangaza mapendekezo yake yaliyowasilishwa kama maamuzi. Walipaswa kukaa kimya mpaka Nec ikutane. Haijakutana bado, lini itakaa, hatujui."

"Kwa hiyo mtu kuniambia niombe radhi wakati najua mchakato haujakamilika watu wataniellewaje?" Alihoji.

Alipoulizwa kama ana mpango wa kukata rufani kuhusu uamuzi huo, alisema: "Sijafanya kosa lolote la kustahili adhabu hiyo."

Wakati akiongea na Nipashe juzi kuhusu wito wa Bashiru wa kuwa milango iko wazi kwa watu wanaotaka kuomba radhi na kama ameshafanya au anakusudia kufanya hivyo alisema;

"Mlitakiwa kumuuliza Bashiru niombe radhi kwa kosa lipi? Au kwa kuwa nimefukuzwa basi nisijali sababu za kufukuzwa. Mimi niombe tu radhi ya nini?"

Februari 28, mwaka huu, Kamati Kuu ya CCM ilitangaza kumfukuza Membe ambaye amewahi kuwa waziri katika serikali ya awamu ya nne na Mbunge wa Mtama, kwa kile kilichoelezwa kwenda kinyume na maadili ya chama hicho.

Wakati Membe akivuliwa uanachama, Katibu Mkuu wa zamani wa chama hicho, Abdulrahman Kinana, alipewa karipio na kutakiwa kutogombea nafasi yoyote ndani ya chama hicho kwa miezi 18, huku aliyekuwa Katibu Mkuu mwingine wa chama hicho, Yusuph Makamba, akiomba msamaha.

Machi 3, mwaka huu, akihojiwa na chombo kimoja cha habari nchini, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alisema anasubiri kusaini barua ya kuomba radhi kutoka kwa Membe.

Alifafanua kuwa tangu awe Katibu Mkuu wa chama hicho ameshasaini barua 14 za wanachama waliofukuzwa na kuomba radhi, hivyo anasubiri ya 15 kutoka kwa Membe kama akitaka.

"Namtakia maisha marefu matarajio yangu atarudi CCM, nikiwa hai ama nimekufa kwa sababu milango ya kuwapokea wanachama wapya ipo wazi na milango ya wanachama kuondoka kwa hiari iko wazi, milango wanachama waliofukuzwa na kuomba radhi ipo wazi.

"Nimeshasaini barua za wanachama waliofukuzwa na kuomba radhi 14 ninasubiri ya 15 ya Membe kama akitaka. Nitaisaini tu."

"Nimempokea Lowassa (Waziri Mkuu mstaafu Edward Lowassa), Sumaye (Waziri Mkuu mstaafu Frederick Sumaye), siku moja ninaweza kuja kumpokea hata Membe, nikianza kubwabwaja hapa ni kama sina picha pana.

# Ajenda saba za SADC kujadiliwa kwa video

**Na Gwamaka Alipipi**

MAWAZIRI wa Fedha, Mipango, Mambo ya Nje, Viwanda na Biashara wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), wanatarajia kujadiliana ajenda muhimu saba kwa njia ya video.

Hatua hiyo imetokana na Afrika Kusini, ambayo ni mmoja wa mwanachama wa jumuiya hiyo, kuathirika na ugonjwa wa virusi vya Corona.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Kanali Wilbert Ibuge, alizitaja ajenda hizo kwa ni pamoja na ya utekelezaji wa kaulimbiu ya mwaka ya SADC isemayo 'mazingira wezeshi kwa ajili ya maendeleo endelevu na jumuishi ya viwanda, kukuza biashara na ajira ndani ya SADC'.

Nyingine ni masuala ya fedha na michango ya jumuiya, tathmini ya utangamano itakayowezesha nchi wanachama kujipima kuhusu utekelezaji wa malengo ya jumuiya hiyo baada ya mwaka 2020, dhima ya SADC hadi kufikia mwaka 2050 na mpango mkakati wa maendeleo wa SADC kwa mwaka 2020-2030.

"Ajenda nyingine ni maadhimisho ya miaka 40 ya SADC, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia ujumbe wa SADC wa waangalizi wa uchaguzi, hati za kusafiria za SADC na uanzishwaji wa shirika la utalii kwa nchi za kusini mwa Afrika," alisema.

Kanali Ibuge alisema kutokana na ushauri uliotolewa katika maazimio ya kikao cha Mawaziri wa Afya wa SADC juzi, kikao cha Baraza la Mawaziri wa jumuiya hiyo kilichopangwa kutanguliwa na kikao cha maofisa waandamizi kuanzia machi 12-14, kimefupishwa na kitafanyika kwa njia ya video kuanzia Machi 16-18.

Alisema utaratibu wa mkutano wa Baraza la Mawaziri unaotarajiwa kufanyika Tanzania kama mwenyekiti wa jumuiya hiyo, utabadilika na utafanyika kwa njia ya video na kwamba mawaziri watafanya mkutano wakiwa katika nchi zao.

"Utaratibu wa kuendesha mkutano kwa njia ya video umeridhiwa na Sekretarieti ya SADC pamoja na nchi mwenyekiti kwa kuwa unalenga kuondoa hatari ya kuenea kwa Corona endapo mmoja kati ya washiriki atakuwa amepata maambukizo," alisema.

Alisema kikao cha Baraza la Mawaziri Machi 18, kitafunguliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, na kitaongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi.

Kanali Ibuge alisema kukatishwa kwa mkutano huo nchini kutaleta athari kiuchumi kwa wafanyabiashara kutokana na wageni 250 waliotarajiwa kuingia nchini.

Naibu Katibu Mtendaji wa SADC anayeshughulikia utengamano, Dk. Thamba Mhlongo, alisema suala la hati za kusafiria za kidiplomasia kwa maofisa wa SADC litajadiliwa na Baraza la Mawaziri kwa kupitisha bajeti ya kuzitengeneza.

Alisema mchakato wa kuziandaa hati hizo umechukua muda wa miaka minne na sasa umeshakamilika, kilichobaki ni kupitishwa kwa bajeti.




# Waziri Mkuu: Sikumfukuza kazi Meneja Tanroads Morogoro

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema hajamfukuza kazi Mhandisi Godwin Andalwisye, anayekaimu nafasi ya Meneja wa Wakala wa Barabara (Tanroads) Mkoa wa Morogoro.

Kwa kuzingatia hilo, Majaliwa amemwagiza Mtendaji Mkuu wa Tanroads kuendelea kumtumia Andalwisye kama mtaalamu wa madaraja wakati wakiendelea na hatua za kumpata meneja wa mkoa.

Alisema hayo jana baada ya kutembelea eneo unapoendelea ujenzi wa Daraja la Mkange Kiegeya na kupokea taarifa za ujenzi kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Mhandisi Patrick Mfugale, kabla ya kutembelea makaburi ya Kolla, eneo ilipozikwa miili ya watu waliokufa kwa ajali ya moto wa lori la mafuta eneo la Msamvu.

"Sijasema mumfukuze ila nimesema nafasi ya umeneja haimfai, anafaa kuendelea kubaki kama mtaalamu wa madaraja, nilisikia bado yuko hapa nikajua ni mgomo baridi asiondoke, lakini nimeelewa ufafanuzi wako (Mhandisi Mfugale) kuwa ni mtaalamu wa madaraja na bado tunamhitaji kwa kazi hiyo," alisema.

Waziri Mkuu pia aliwaagiza mameneja wa mikoa wa Tanroads kukagua makalavati na madaraja yaliyo kwenye barabara kuu ili kuchukua hatua haraka za matengenezo na kuondoa athari kama ilivyojitokeza kwenye barabara kuu ya Morogoro-Dodoma.

Alisema ni vyema mameneja hao wakajenga tabia ya kuchunguza madaraja hadi ndani badala ya kuangalia juu juu ili kuepusha athari.

Pia, alisema serikali inafahamu uharibifu wa miundombinu unaoendelea katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na mvua na kuagiza ukarabati wa dharura ufanyike ili wananchi waendelee kupata huduma wakati matengenezo makubwa na ya kudumu yakisubiri kipindi cha kiangazi.


Mfugale alimwambia Waziri Mkuu kuwa ndani ya wiki mbili zijazo, wanatarajia kazi ya ujenzi wa daraja iwe imekamilika isipokuwa uwekaji wa lami, ili magari yapishane juu ya daraja kama ilivyokuwa awali.

"Tunachokiomba ni mvua tu zisinyeshe, ikinyesha kazi inakuwa ngumu, kinachoendelea sasa ni kujenga hizo zege pembeni ili tukazisimamishe pembeni mwa daraja," alisema. Aliahidi usiku wa kuamkia leo wanatarajia kuanza kumwaga zege upande wa pili wa barabara ya mchepuko ili kuwezesha magari yote kutumia njia hiyo wakati watakapofunga kwa muda kipande cha barabara hiyo kuu ya Morogoro-Dodoma ili kuwezesha ujenzi wa daraja kufanyika kwa ukamilifu.

Alisema kwa sasa msongamano wa magari umekwisha, na mawasiliano yamerudi kama kawaida.

Akiwa makaburi ya Kolla alipokutana na viongozi wa serikali ya mkoa, viongozi wa dini na wananchi, Waziri Mkuu aliuagiza uongozi wa mkoa na Manispaa ya Morogoro kuendelea kuboresha eneo lote la ardhi ya makaburi kwa kuweka uzio na utaratibu wa kuzika kwa kuzingatia maeneo ya Waislamu na Wakristu pamoja na kuweka ulinzi katika eneo hilo.

Awali, Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, alisema uongozi wa mkoa umeridhishwa na ujenzi huo na kwamba wataendelea kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa, michango ya fedha taslimu iliyochangwa hadi kufikia Februari 28, mwaka huu ilikuwa ni Sh. milioni 59.5, ambazo ziliwekwa benki kwenye akaunti maalumu na kiasi kilichotumika hadi sasa ni Sh. milioni 19.8 huku salio lililobaki likiwa ni Sh. milioni 39.6.



Mkurugenzi wa Huduma za Kidijitali wa Vodacom Tanzania, Nguvu Kamando, akizungumza na waandishi wa habari kwenye maadhimisho ya wiki ya ubunifu, jijini Dar es Salaam jana. Vodacom, imetoa fursa kwa wanavyuo waliomaliza masomo na wenye uwezo wa ubunifu ili kuwawezesha kufikia malengo yao ya ubunifu kwa kushirikiana na SmartLab. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Smartlab Tanzania, Edwin Bruno. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Elimu rushwa ngono sasa mtaa kwa mtaa

**Na Halfani Chusi**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Kitengo cha Kupambana na Rushwa ya Ngono, imesema imejipanga kuanza kutoa elimu mtaa kwa mtaa ili kuhakikisha inawafikia watu wa rika zote.

Mkurugenzi wa Idara hiyo, Janeth Mawinza, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipofungua kikao cha mgawanyo wa majukumu na wadau mbalimbali katika taasisi hiyo pindi watakapoanza kutoa elimu hiyo.

"Leo (jana) tumeitana hapa na ninyi wadau katika taasisi hii ya kupambana na rushwa ya ngono ili kupeana mikakati ya kuanza kutoa elimu hii mtaa kwa mtaa, tutaanzia Wilaya ya Ilala siku ya Ijumaa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema rushwa ya ngono ni hatari zaidi ya rushwa ya kawaida kwa kuwa madhara yake ni makubwa kwa mwili wa binadamu, ikiwa ni pamoja na kifo.

"Tumejitoa kukomboa hiki kizazi ambacho kinaonekana kuanza kupotea kwa sababu ya rushwa ya ngono, rushwa hii ni hatari na inaua, ukiachana na kuua, pia inamweka mtu katika hatari ya kupata magonjwa hatarishi kama kaswende, na gono sambamba na kumharibu mtendwa kisaikolojia.

"Kikubwa tunaomba ushirikiano wa kutosha pindi mtakapoona tunapita mtaani kutoa elimu, tuna mambo mengi ambayo tunatamani jamii ijue juu ya hii rushwa ya ngono hasa kwa hawa wanafunzi na watoto wa kike ambao ndiyo wahanga wenyewe," alisema.

Ofisa kutoka Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi Ilala, Christina Onyango, alisema wako bega kwa bega na taasisi hiyo kuzuia rushwa ya ngono.

# Mfugaji atozwa faini ya mil. 60/- kionevu

**Na Mwandishi Wetu, TABORA**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ametoa siku saba kwa uongozi wa Mkoa wa Tabora kufanya tathmini ya mpango wa uanzishwaji wa mamlaka za miji midogo na hatua zilizochukuliwa kwa mifugo iliyokamatwa ndani ya hifadhi za misitu na wanyama.

Amesema tathmini hiyo inapaswa kufanyika ili kuondoa malalamiko makubwa ya wafugaji katika mkoa huo yanayoendelea bila msaada wowote.

Moja ya malalamiko ya wafugaji katika mkoa huo ni kutozwa faini kinyume cha taratibu, wakimwambia waziri huyo kuhusu mfugaji mwenzao kutozwa faini ya Sh. milioni 60 kionevu na mamlaka za kiserikali.

Vilevile, waziri huyo amemwagiza Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Robert Makungu, kufuatilia na kuchukua hatua na kutoa taarifa katika maeneo yote ambayo sheria na taratibu zilikiukwa na baadhi ya watumishi wa serikali katika kutekeleza sheria kwa kutokujua au kwa makusudi na kuichafua serikali mbele ya wananchi.

Akizungumza kwenye mikutano ya hadhara katika Vijiji vya Nata wilayani Nzega, Kigwa wilayani Uyui, Ipole wilayani Sikonge na Mnada wa Ipuli Manispaa ya Tabora, Urambo na Kijiji cha Zugimlole Kaliua, Mpina alipokea malalamiko makubwa ya wafugaji dhidi ya mamlaka za serikali.

Wafugaji wa miji midogo ya Nzega, Igunga, Urambo na Manispaa ya Tabora, walidai mamlaka zimewakuta wakiwa na maeneo yao wanayoyamiliki kihalali na kufanya shughuli za mifugo na kilimo, lakini baada ya kuanzishwa mamlaka hizo, wanakamatwa na kuambiwa mifugo haitakiwi bila kuelezwa mahali pa kupeleka.

Walisema mifugo yao ikikutwa ikiwa inakwenda kwenye malisho, minadani, maeneo ya majosho na chanjo, hukamatwa na kushikiliwa kwa muda mrefu na kutozwa faini ya Sh. 50,000 hadi Sh. 100,000 kwa ng'ombe na Sh. 20,000 kwa mbuzi, jambo ambalo linawapa usumbufu na kuwatia umaskini.

Pia walilalamikia kukamatwa mifugo yao na kutozwa faini zisizo kwenye sheria pindi wanapokamatwa wakiingia kwenye hifadhi za misitu, wakimtolea mfano mfugaji mwenzao aliyetozwa faini ya Sh. milioni 60.

Kutokana na malalamiko hayo, Mpina alimwagiza Katibu Tawala Mkoa wa Tabora kupitia vielelezo vyote juu ya malalamiko hayo kwa kupata majina ya wafugaji waliotozwa faini hizo pamoja na kupata majina ya viongozi waliohusika kwenye vitendo vya rushwa na kuchukua hatua dhidi yao.

Pia aliagiza majosho yote 38 yasiyofanya kazi katika Mkoa wa Tabora, yakarabatiwe na kuanza kuogesha mifugo ifikapo Aprili na kwamba halmashauri itakayopuuza maagizo hayo ya serikali, majina ya viongozi hao yawasilishwe wizarani kwa hatua zaidi.

Waziri Mpina pia alizitaka mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini ya shughuli za kiuchumi katika maeneo yao ili kuzuia kamata kamata ya mifugo katika maeneo yao na kukinzana na sheria zingine.

Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Gift Msuya, alimhakikishia Waziri Mpina kuwa wafugaji wa Uyui kuanzia sasa, hawatatozwa faini kiholela na kwamba kama mfugaji atakamatwa asitozwe faini yoyote hadi kibali chake ili kuondoa rushwa kwa baadhi ya watendaji wa serikali wasiowaaminifu.

## HABARI KITAIFA

# Jafo awaweka mtegoni ma-RC mikopo ya makundi maalumu

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amewatahadharisha wakuu wa mikoa nchini ambao watawasilisha bajeti zao bila kutenga asilimia 10 ya vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, kwa mujibu wa sheria hazitapitishwa.

Jafo alitoa angalizo hilo jana mjini hapa alipokuwa katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Pwani ambacho kilijadili mpango wa bajeti ya mwaka 2020/2021 kwa mkoa huo.

"Mkoa wowote, mkuu wake wa mkoa akileta taarifa ya mapendekezo ya mpango wa bajeti haitajadiliwa katika kikao cha kamati ya bajeti endapo haitaonyesha asilimia 10 iliyotengwa kwa mujibu wa sheria," alisema.

Alisema kwenye taarifa ya bajeti kila Mkuu wa mkoa atatakiwa kuwa na jedwali linaloonyesha namna halmashauri zinavyotoa asilimia 10 kwa ajili ya mikopo ya makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Alisema, hatakubaliana na Mkuu wa Mkoa yeyote ambaye atakwamisha bajeti kwenye Wizara ya Tamisemi badala yake atapeleka majina kwa Rais kumweleza watu wanaokwamisha bajeti katika ofisi yake.

Aliwataka wakurugenzi kuzingatia sheria hiyo ili wasiwe chanzo cha kukwamisha bajeti ya mikoa yao.

Akizungumzia suala la ukusanyaji wa mapato, Jafo alisema Mkoa wa Pwani bado hali hairidhishi kutokana na halmashauri mbili pekee kati ya tisa ndizo zinazofanyika vizuri.

Kufuatia hali hiyo ametoa agizo kwa wakurugenzi kuhakikisha



wanasimamia fedha zinazokusanywa kuingizwa katika mfumo wa serikali.

Alisema, mashine nyingi za kukusanyia fedha bado zinachezewa na kusababisha makusanyo yanayopatikana kutoingizwa katika mfumo wa serikali.

Katika hatua nyingine Jafo alitoa maelekezo kwa wakuu wa wilaya zote nchini kuainisha maeneo ambayo yameathiriwa na mvua na kusababisha baadhi ya shule kufungwa.

Alisema, ni vyema maeneo hayo yakajulikana ili wanafunzi wanaosoma katika shule hizo watafutiwe mbadala waendelee na masomo hususani wale ambao wanamitihani ya kitaifa.

Akifungua kikao hicho Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, alisisitiza kila halmashauri kusimamia ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vya ndani.

Kikao hicho kilipitisha mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2020/2021, Sh. 251,575,515,125.

# Mkataba Unesco kuleta fursa nchini

**Na Romana Mallya**

TANZANIA inatarajia kuwasilisha kwa mara ya kwanza taarifa ya kitaifa ya utekelezaji mkataba wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco), inayohusu kulinda na kuendeleza uanuai wa kujieleza kiutamaduni.

Ripoti hiyo ambayo inatarajia kuwasilishwa Unesco wiki hii, ilikabidhiwa jana jijini Dar es Salaam kwa Waziri Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Dk. Mwakyembe alipongeza timu iliyohusika kuiandaa taarifa hiyo ya mkataba wa mwaka 2005.

Aliwaomba wadau wajiandae kupokea fursa mbalimbali za ndani na nje kupitia mkataba huo.

"Ninasema hivyo kwa sababu tuna tatizo kubwa Tanzania la kushindwa kuziwahi na kutumia fursa zinazojitokeza. Huo ni ugonjwa, tunajua kulalamika, lakini fursa zikijitokeza tunavuta sana miguu," alisema.

Dk. Mwakyembe alitolea mfano Kiswahili na kusema imekuwa ni lugha kubwa duniani na fursa zake zipo kila sehemu.

"Sasa hivi ukimshauri mtoto wako kusoma Public Relations au International Relations unamsumbua mtoto kupata ajira baadaye.

"Kama mtoto wako ana kipaji cha lugha, mwambie asome Kiswahili hatakosa ajira... hii ndiyo kazi iliyopo sasa hivi, kati ya lugha 6,000 kubwa duniani, Kiswahili ni lugha katika lugha 10 zinazoongewa na watu wengi duniani."

Alisema kila nchi kwa sasa ikianzisha televisheni au redio lazima iwe na Kiswahili ndani yake.

"Nikaamua na kusema hii ni fursa ya Watanzania waliosoma lugha waanze kuitumia, tukaanzisha utaratibu wa kuwasajili kwenye kanzi data, ambalo tunasambaza kwenye balozi zetu malipo ni Sh. 10,000," alieleza.

"Kwa muda mrefu sasa tuna majina siyo zaidi ya 1,500, lakini maombi ninayopata kutoka Kenya na Uganda waingizwe kwenye mfumo huo ni mengi kuliko ya Watanzania, ndiyo maana ninasema tunajua kulalamika."

Alisema aliita Baraza la Kiswahili Zanzibar (Bakiza) na Tanzania Bara (Bakita) na kuwaeleza badala ya kufanya ushindani kutafuta Kiswahili kilianzia wapi, washikamane kutafuta fursa.

Kuhusu taarifa hiyo ya utekelezaji mkataba wa Unesco, Dk. Mwakyembe alisema amepata maelezo ya kutosha kuhusu taarifa hiyo, na kwamba hana sababu ya kurudia.

"Nimeridhika kazi hii inalenga kuendeleza sekta ya sanaa, utamaduni na ubunifu Tanzania na nje ya mipaka. Ninajua mmeshiriki katika kujadili kuainisha fursa na changamoto na kutoa mapendekezo ya uboreshaji wa sera kwenye mkataba huu," alisema.

Ofisa Programu wa Unesco, Nancy Angulo, akizungumza kwa niaba ya Mwakilishi wa Unesco, alisema taarifa hiyo inatarajia kuwasilishwa kwenye shirika hilo mapema wiki hii.

Kaimu Mkurugenzi msaidizi wa urithi wa utamaduni na maadili ya taifa, Boniface Kadili, alisema mkataba huo unatoa fursa ya kuwa na uhuru wa kujielezea kisanaa, kiutamaduni, ubunifu, uandishi na filamu.

Alisema umeandaliwa kwa kukusanya taarifa mbalimbali za kisera na kimkataba zilizoridhiwa na nchi na kuziweka pamoja.

Mwenyekiti wa kamati ya utayarishaji wa ripoti hiyo, Robert Mwampembwa, alisema ripoti hiyo ni ya miaka minne na jana walimkabidhi Waziri Mwakyembe aipitie na akiiridhia itaingizwa kwenye mfumo wa kidigitali wa Unesco.


**The Guardian Limited**

## JOB VACANCY

**The Guardian Limited ,publisher of leading Tanzania newspapers, The Guardian and Nipashe, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

### CIRCULATION FIELD OFFICER - DAR ES SALAAM

**Job Purpose:**

To boost copy sales and develop relationships with agents and vendors in the sales channel in the assigned area to meet your set sales targets.

**Main Responsibilities:**

The successful candidates will be responsible for the following key results:

- Work with the agents and vendors in making sure that the business grows and The Guardian Limited publications are available and visible and sold at the set retail prices with optimal return levels.
- Develop and grow more channels of distribution.
- Monitor indicators relating to market arrivals, circulation sales and returns indicators and make appropriate reports to Circulation Supervisor.
- Identify and build rapport with existing and potential customers by communicating the benefits of Selling The Guardian and Nipashe.
- Monitor newspaper distribution and sale trends in particular areas, prepare weekly sales plans and update supervisor on a regular basis.
- Monitor daily performance of TGL brands in your particular areas of operation in comparison to our rival publications and make reports that guide growth strategies.
- Open up new markets in particular areas of operation that will in turn translate into higher sales.
- Attend customer complaints that in one's particular area of operation so as to maintain good customer relations and protect the company's interests.
- Liaise with supervisor in credit control and debt management within particular area of operation.
- Submit daily and weekly reports on progress on activities, including meeting set sales targets.
- Manage debt collection and credit control within one's respective area operation.
- Demonstrate ability to work under minimum supervision.

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 2 year's relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge, and familiarity with a wide range of newspapers brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via HRO email address: ;**vacancy@guardian.co.tz** by March 13, 2020

NB: Only shortlisted candidates will be contacted.

***The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

615654302

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanasiasa wavumiliane kudumisha demokrasia

KUVUMILIANA si suala linaloishia ndani ya familia kwani ni kitu kinachohitajika zaidi kwenye kila nyanja iwe siasa, imani na hata kwenye kuendesha miradi ya kiuchumi.

Uvumilivu ni muhimu iwe serikalini, ndani ya vyama vya siasa, asasi za kiraia na bungeni ili kuepusha mitafaruku na kuleta hofu kuwa pengine ukiwa kiongozi wa serikali, chama au taasisi hauko salama.

Ukosefu wa uvumilivu wa kisiasa unaweza kusababisha madhara kwa baadhi ya viongozi kwa mfano, kutishiana maisha na hata kusababisha kudhuriana.

Tunasema haya kwa sababu taifa linaelekea kwenye uchaguzi mkuu Oktoba mwaka huu, pengine baadhi ya viongozi wanaweza kutumia majukwaa ya kisiasa kuwa eneo la kujibizana, kusema siri za ndani za vyama walivyohama na kunyoosheana vidole.

Tunakumbusha kuwa huo si wakati wa kuonyeshana siasa za chuki hasa kwa mahasimu wa kisiasa ambao ni vyama vya upinzania na chama tawala.

Wakati kampeni za kisiasa zinatarajiwa kuanza ni vyema kusikiliza mawazo ya wadau wote. Wapinzani wasikilize CCM na chama tawala kiwasikilize wapinzani.

Tunaona kusikiliza hoja za watu wengi ni njia ya kupata maoni mengi na mbalimbali ambayo yanasaidia kuboresha mipango na mikakati ya maendeleo inayopangwa.

Kampeni na harakati za uchaguzi zinapoanza uvumilivu wa kisiasa unahitajika zaidi ili kila mmoja atoe mawazo yake kwa ajili ya kutimiza jukumu la kuisimamia, kuikosoa na kuishauri serikali.

Bungeni ni vizuri serikali kusikiliza upinzani, lakini upinzani kusikiliza hoja za serikali zinazoukosoa na kuushauri ili kupata mawazo mengi ambayo yanafanyiwa kazi kwa kuchambuliwa ili kusukuma maendeleo ya nchi.

Tunaona kuwa wakati huu wa kuelekea kwenye kampeni na uchaguzi mkuu, viongozi wafahamu kuwa jamii wanayoiongoza iko kwenye kiwango cha juu cha demokrasia na uhuru wa mawazo.

Ni uwanja unaoruhusu kupata maoni na fikra nyingi, michango ya mawazo ya kila aina na tofauti kutoka vyanzo mbalimbali.

Kwa hiyo, ni vyema serikali iyasikilize, kuyachambua na kuyachukua yale yanayofaa ili kupata mchele na pumba.

Wakati mwingine kupata mawazo ya wengi kunakuwa ni uwanja mpana wa kujua vitu vingi zaidi na namna ya kutekeleza majukumu muhimu ya maendeleo.

Pamoja na maoni ya wanasiasa ni vyema kusikia pia kutoka kwa wasomi kwani wao ndiyo kioo cha serikali cha kujitazamia, ili kila mmoja achangie namna ya kuendeleza viwanda, kuondoa umaskini na kuifanya Tanzania kuwa taifa la uchumi wa kati.

Hata hivyo tunawakumbusha wanasiasa kufanya mambo kwa misingi na taratibu za kisheria badala ya kukurupuka.

Pamoja na kwamba uchaguzi, kuchaguliwa na kuchagua ni haki ya kila mtu, wanasiasa wakumbuke kuwa demokrasia si kitu cha kufikiria ni mienendo bayana na mambo yanayoonekana yakihusisha watu, taasisi kama vyama vya siasa na wananchi.

Tunawakumbusha wanasiasa kuwa demokrasia zinazowapa nguvu za kujitutumua majimboni ni lazima izingatie, sheria, taratibu na miongozo ili kuwahakikishia uwepo wa nidhamu, amani na utulivu.

Wanasiasa, viongozi wa vyama na wabunge si wageni, kama wawakilishi wa wananchi wanazijua sheria na kanuni, hivyo wazisimamie ili kampeni na uchaguzi uwe wa tija na si kuvurugana.

Tunapokwenda kwenye kampeni tukubali kusikiliza sauti na matakwa ya wengi, wachache na makundi ya wanyonge kwa sababu kila upande una umuhimu wake kwenye kudumisha demokrasia na kuisimamia serikali ili taifa lifikie maendeleo ya kisiasa, uchumi, kijamii na mengine mengi tunayoyatamani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Huu unaweza kuwa ukomavu wa kisiasa

**KAMATI** Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imemfukuza uanachama kada wake aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi, Bernard Membe, kwa kukiuka maadili ya chama.

Mbali na kumfutia Membe uanachama, kamati hiyo pia ikatoa karipio kwa Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, Abdulrahman Kinana, kwa kukiuka maadili ya chama, lakini kumsamehe Yusuph Makamba kwa makosa kama hayo.

Wakati adhabu ya Membe ikiendelea, CCM inasema milango ya kuondoka kwa hiari yao, kuwapokea wanachama wapya na waliofukuzwa wakienda kuomba radhi, wote kwa pamoja iko wazi.

Kwa hatua hiyo, CCM inasema kuwa kada wake huyo aliyefutiwa uanachama wa chama hicho, anaweza kuomba radhi akarudishwa kundini kuungana na wanachama wenzake.

Hiyo ni kauli ya Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, kwamba chama kinasubiri kuona barua ya kuomba radhi kutoka kwa Membe, hivyo katibu huyo hawezi kuanza kubwabwaja kana kwamba hana picha pana.

Pengine kauli ya Dk. Bashiru inaonyesha kuwa anatambua kwamba kila binadamu ana upungufu yake na kila mtu ana maeneo, ambayo amebarikiwa kuwa na uwezo wa kuyaelewa na mengine hana.

Vilevile penye wengi ni lazima tofauti zitakuwapo tu ila jambo la msingi ni wahusika kusaidiana ili waendelee kuwa kitu kimoja, lakini suala la nidhamu ni muhimu zaidi ili kuwekana sawa.

Hali ikishafikia hapo kama hiyo ya kumfuta mtu uanachama, kama ana mapenzi na chama, kinachofuata ni kuomba radhi ili arudishwe kundini kama ambavyo katibu anasema.

Kwenye suala la kuomba radhi, wapo baadhi ya watu ambao wamejaliwa busara na hufikia kuomba hata kama hawajafanya kosa, lengo likiwa ni kuepusha malumbano yasiyo na msingi.

Hivyo ni nafasi ya kada huyo kutafakari kwa kina akitambua kuwa hata vikombe havina miguu, lakini siyo ajabu vikagongana kabatini, hivyo suala la kutofautiana lipo, lakini lisipewe nafasi ya kugawa wanachama.

Ikumbukwe kuwa wapo baadhi ya makada wa CCM ambao waliowahi kutimuliwa katika chama hicho, kisha wakaomba radhi na kurejeshwa kuendelea kukitumikia chama kama kawaida.

Kuomba radhi na kusamehewa ni jambo muhimu, kwa sababu hakuna binadamu aliyekamilika, na kwa kutambua hilo, ndiyo maana katibu huyo anasisitiza kuwa milango iko wazi kwa makundi hayo yote.

Chama ni wanachama na bila wanachama hakuna chama, hivyo akiondoka mwanachama mmoja au kufukuzwa, idadi ya wanachama inapungua, hivyo si jambo la kufurahia pale mwanachama anapoondoka au kufukuzwa.

Kutokana na ukweli huo, Dk. Bashiru anakemea wanachama kutosherehekea hatua zilizochukuliwa za kumfutia uanachama kada wao Membe kwa vile kumpoteza mwanachama ni msiba.

Inawezekana kinachosemwa na katibu huyo ni ukomavu wa kisiasa na hasa kwa kutambua kuwa siasa siyo uadui na pia kutofautiana kimtazamo, kimawazo ni jambo la kawaida.

Kwamba kada wao amekwenda kinyume na taratibu za chama na kufutiwa uanachama, lakini pia chama kimeweka milango wazi ili akitafakari kisha akarudi kuomba radhi, basi anapokelewa.

Hatua hiyo inaonyesha hakuna chuki yoyote, ila mara nyingi wapambe ndiyo huwa wanadaiwa kushabikia na kuongeza chokochoko pale tofauti kama hizo zinapojitokeza ndani ya chama.

Lakini inaonekana Dk. Bashiru amewashtukia, ndiyo maana anaweka wazi kwamba wanachama wasisherehekeee Membe kufutwa uanachama bali watambue kuwa kuondokewa na mwanachama ni msiba.

Matarajio yake ni kwamba ipo siku Membe atarudi CCM na kuungana na wanachama wenzake, kwa vile milango ya kuwapokea wanachama wapya, walioondoka kwa hiari na waliofukuzwa na kuomba radhi iko wazi.

Kauli ya katibu huyo inaonyesha kukomaa kisiasa juu ya uendeshaji wa chama, katika dhana na misingi ya demokrasia, uwazi kwenye ushiriki wa wanachama kukitumikia na kufanya maamuzi muhimu.

Utaratibu wa mwanachama kufutiwa uanachama, lakini bado akapewa nafasi nyingine ya kuomba radhi ili arejeshwe kundini kuendelea kuwatumikia wananchi ni wa mfano wa kuigwa.

Wapo baadhi ya makada wa CCM ambao waliowahi kutimuliwa katika chama hicho, kisha wakaomba radhi na kurejeshwa, utaratibu kama huu inaimarisha umoja ndani ya chama.

## BARUA / MJADALA

# Tutaacha lini kutumia vyombo vya plastiki?

*MHARIRI naomba nipongeze Nipashe kwa kazi kubwa ya kutuelimisha na kutusaidia wananchi ili tufahamu mambo yanayoendelea kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu.*

*Pamoja na pongezi zangu naomba kuuliza iwapo kuna jitihada za kuwaelimisha wananchi kuhusu matatizo ya kuendelea vyombo vya plastiki ambavyo tunaambiwa vina athari kiafya.*

*Binafsi natembelea shule za msingi na sekondari na kukuta wanafunzi wanalia vyakula kwenye vyombo vya plastiki kuanzia sahani hadi vikombe. Baadhi ya sahani zinaanza kuchubuka huku vikombe navyo vikiwa na hali kama hiyo.*

*Niishauri serikali itembelee shule na kushauri wamiliki na uongozi wa shule kubadilisha kutumia vyombo hivyo ambavyo huenda vikichubuka husababisha watoto kulishwa sumu za plastiki tena katika umri mdogo.*

*Wakati wa kampeni ya kuondoa mifuko duni ya plastiki baadhi ya wataalamu walitangaza kuwa vifaa na vyombo vya plastiki vina sumu kutokana na kemikali zinazotumiwa kuvitengeneza hivyo ni hatari kwa watu.*

*Tunaomba hata kama shule haziwezi kununua vyombo vya plastiki vitumike vya bati ambavyo havina athari kwa watoto wala mazingira yetu.*


*Lakini tunashauri kuwa pamoja na kuzuia kuvitumia kulia chakula vyombo hivyo visitumike kuwekea vyakula nikimaanisha mabeseni au ndoo ambazo huwekea vyakula na maji kwenye shule hizo.*

*Tunaiomba serikali kuweka kiwango cha vyombo vya aina hiyo ambavyo vinafaa kutumiwa na wanafunzi na hata jamii nyingine ili kulinda afya.*

**Daudi Ndano**
**DSM.**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Unyama huu wa sumu umeshitua watu wengi

**Na Mwandishi Wetu**

SUALA la watu kupewa sumu na kupoteza maisha ni jambo linalofahamika katika jamii lakini hili la Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Philipo Mangula, kulishwa sumu linaendelea kugonga vichwa vingi vya Watanzania.

Poleni familia pamoja na Mongula kwa ajali hiyo ambayo inawafanya watu kuzidi kushangaa kuwa usalama uko wapi , kwa kuwa viongozi wa ngazi za juu kama hao walikuwa wanadhaniwa kuwa wako salama zaidi , lakini ukweli ni kwamba hata wao maisha yao yanatishiwa pia na maadui.

Inawezekana kuwekewa simu kwenye glasi ya mvinyo, kwenye chakula na vinywaji vingine kwenye sehemu za burudani ambako wakati mwingine si rahisi kugundua.

Ni wazi kuwa sumu zinasababisha kifo pengine kutokana na kukausha maji mwilini, au kufanya damu kuganda na wakati mwingine kuumiza mishipa ya fahamu na ubongo.

Yote hayo ni mambo yanayoweza kusababishwa na sumu mwilini lakini zipo nyingine zinazoua taratibu ni wazi kuwa kiasi chochote cha sumu kikiingia mwilini kinaweza kuhatarisha maisha na afya ya aliyelishwa.

Pamoja na kwamba tatizo hilo la kulishwa sumu kiongozi huyo wa CCM limebainika, kuna haja ya viongozi wengine kuchukua tahadhari kwa kuwa waovu wapo na wanafanya bidii kuhujumu maisha ya watu.

Kwa kilichompata Mangula ni kwamba inaweza kuelezewa kuwa pengine sumu ni kitu kinachowazunguka watu wengi, lakini jambo la msingi ni watu, wasitumie sumu kutishia maisha ya wenzao.

Dunia imejaa sumu za aina mbalimbali mathalani, kuna nyoka wenye sumu kali, wapo samaki na viumbe wengine wa majini wenye sumu kali , si hivyo hata jamii za nge zinatajwa kuwa na sumu kali. Uyoga nao ni sumu, kama ambavyo hata ndege nao wanaelezwa kuwa wapo baadhi yao manyoya yenye sumu na ni hatari iwapo vumbi lake litamwingia mwanadamu.

Kama huo ndiyo ukweli kuwa maisha ya mwanadamu yamezungukwa na sumu mbalimbali, kwanini watu watumie sumu kuangamiza maisha ya wenzao? Ni ukweli kuwa kutumia sumu bila kujali ni ya aina gani kumdhuru Mangula ni jambo ambalo limeshangaza wengi.

Wakati Fulani Rais wa Marekani Donald Trump, alisema katika harakati za kazi zake kuna wakati alilazimika kula mikate (burger) kutoka kampuni ya Mac Donald , ili kujiepusha na uwezekano wa kulishwa sumu.

Kwa viongozi wakuu hatari za kushambuliwa na kuuawa kwa sumu zipo na kikubwa ni kuchukua tahadhari kwa kuwa maadui wako macho wakati wote na wanatumia mwanya kutimiza azma zao.

Kwa sababu polisi na wataalam wanaendelea na uchunguzi ni vigumu kuzungumzia kilichompata Mongula, lakini ukweli ni kwamba wengi wamepata kiwewe na taharuki na wangependa kufahamu kilichompata na wahusika wa mkasa huo.

Tatizo la viongozi kulishwa sumu lipo ndiyo maana hata Rais John Magufuli, wakati akiwa Waziri wa Ujenzi, anaeleza kuwa alilishwa sumu na wabaya wake, waliochukizwa na kazi alizokuwa anafanya na Rais wakati huo, Benjamin Mkapa, kumtaja kuwa mchapakazi bora na moja wa askari shujaa wa miavuli.

Kilichotokea kwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, kinaweza kutokea kwa yeyote kwa sababu wauaji mara zote wana sababu ya kufanya ukatili huo.

Cha msingi ni kuona umuhimu wa kuchukua tahadhari za hali ya juu ikiwamo pia kuwa makini na vyakula pia kushikana mikono na watu wengi. Ni vyema kunawa mara moja baada ya kushikana mikono ikibidi hata kutumia sabuni au dawa nyingine zenye nguvu na ukali zaidi.

Aidha, hata kupewa zawadi ni vyema pia kuwa makini ili kuepusha uwezekano wa kushika sumu hasa wakati huu wa uchaguzi au kwenye minyukano ya kisiasa.

Pamoja na kuchukua tahadhari za vyakula pengine hata kusalimiana kwa kukumbatiana nako kunaweza kukuachia sumu . Mbinu ya kutumia kadi au maua viongozi wakiwa hospitalini au wakiumwa inaweza pia kutumiwa kwa hiyo ni vyema kuchukua tahadhari kuepuka uwezekano wa kudhuriwa na watu wenye nia mbaya.

Pamoja na kujikinga, wataalamu wa sumu wanaeleza kuwa miili ya binadamu ina namna ya kujiepusha na sumu ili zisiingie mwilini na kuleta madhara moja kwa moja, kwa mfano ngozi inazuia mwili na sumu kwa kuizuia kupenya.

Wakati mwingine tumbo linakataa sumu kwa kufanikisha kuitoa kwa kuitapika au kuharisha. Aidha, nguvu ya hisia nayo inahusika kukataa sumu kuingia mwilini. Hata hivyo kikubwa ni kwa kila mmoja kuchukua tahadhari .

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Bil.10/- kunoa wataalamu wa kufundisha Kifaransa

Na Faustine Feliciane

UBALOZI wa Ufaransa nchini, umesema umetenga zaidi ya Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kufundisha walimu na maprofesa wa kitanzania lugha ya Kifaransa ili watumike kufundisha wanafunzi kuanzia ngazi ya shule za msingi mpaka vyuo vikuu.

Akizungumza kwenye mkutano wa pamoja wa mabolozi wa nchi zinazozungumza Kifaransa wanaowakilisha nchi zao Tanzania, Balozi wa Ufaransa, Frederic Clavier, alisema lengo la Ufaransa kutenga fedha ni sehemu ya mpango wa kuhakikisha lugha ya Kifaransa inazungumzwa na Watanzania wengi.

"Fedha hizi ni kwa ajili ya mkakati wa mwaka 2020/2021 na baada ya hapo zinaweza kuongezwa kulingana na mahitaji kwa kipindi hicho...tungependa kuona na Tanzania kama ilivyo kwa Morocco, DRC na Comoro nayo inaingia kwenye kundi la nchi zinazozungumza Kifaransa," alisema Balozi Clavier.

Aidha, alisema katika maadhimisho ya miaka 50 ya umoja wa nchi zinazozungumza Kifaransa, kutakuwa na matukio mbalimbali yatakayoadhimishwa kwa wiki moja kuanzia Machi 17 mpaka 28.

"Kama Ufaransa tungependa kuona Tanzania kama nchi inaingia kwenye kundi la nchi za Francphonie... hii ni sababu ya kutenga fedha kuendeleza Kifaransa Tanzania, tunaamini kuwapa elimu kundi la wasomi itasaidia kuwafundisha wengine," alisema na kuongeza:

"Lugha ya Kiswahili ni lugha kubwa kama kilivyo Kiingereza na Kifaransa, tunaamini kama Tanzania pia itakuwa na watu wengi wanaozungumza Kifaransa itafungua njia nyingi za fursa za kiuchumi."

Balozi wa Morocco nchini, ambaye ni Makamu wa Rais wa Francphonie, Abdelilah Benrayane, alisema maadhimisho hayo yataenda pamoja na matukio mbalimbali ikiwamo kuwainua wanawake katika maendeleo.



Wachuuzi wa maturubai wakiwa wameyapanga kwenye eneo ambalo barabara inaendelea kujengwa, Mwenge, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachoweza kuleta usumbufu kwa wajenzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# W'biashara waipa tano NEMC vita taka sumu

Na Mwandishi Wetu

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limepongezwa na wadau kwa kupambana na taka zenye sumu ili zisitapakae nchini.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wa wafanyabiashara ambao walijadili, pamoja na mambo mengine, mafanikio na matatizo ya utekelezaji wa marufuku ya mifuko ya plastiki. Marufuku hiyo ilianza Juni 1, mwaka jana.

Wajumbe walisema moja ya tatizo kubwa linaloikabili dunia ni namna ya kupambana na taka zenye sumu na taka za aina nyingine, ambazo huongezeka kwa wingi kila siku kwa sababu ya ongezeko la watu na shughuli zao.

Baada ya kuliona hilo, Baraza hilo lilisisitiza kwamba kila kiwanda nchini kiwe na cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira (TAM) na kufanya ukaguzi.

Mbali ya cheti hicho, NEMC inafanya ukaguzi wa viwanda na maeneo ya biashara na kutoa elimu kwa umma.

Mwishoni mwa wiki NEMC iliharamisha vifungashio vya tubing, ambavyo vinatumika kufungia karanga, barafu, korosho na ubuyu.

Juma Mohamed, ameishauri NEMC kuendelea na juhudi ya kupambana na mifuko ambayo hairuhusiwi nchini. "Wananchi wamesahau mifuko ya plastiki. NEMC wapambane na kasoro hizi: Mara watu wanaingiza nchini mifuko haramu tutawashtaki, wawakamate. Kadhalika wawasaidie kwa nguvu zote wajasiriamali wadogo ili mifuko izalishwe kwa wingi na bei ishuke," alisema na kuongeza:

"Kwa mfano, wenye maduka hawana karatasi au magazeti ya kufungia bidhaa za wateja wao."

Mohamed alisema kupiga marufuku tu hakutoshi, bali jitihada iwe ni kuweka kitu mbadala ili wananchi wadogo wasifadhaike.

Jonathan Nathanael, mwenye kiwanda cha kutengeneza chakula cha kuku jijini Dar es Salaam, aliisifu NEMC kwa kupunguza siku za kupata cheti cha TAM kutoka siku 140 mpaka siku 75, na kusema jambo hilo limewavutia wawekezaji wengi na ambao wanaunga mkono azma ya serikali ya ujenzi wa viwanda.

"Kwa sisi wawekezaji mambo yetu yamekuwa mazuri, huko nyuma tulilazimika kutumia siku zaidi ya 140 kupata cheti cha TAM, lakini siku hizi ni ndani ya siku 75 tu tunapata cheti hicho," alisema Nathanael.

Aliongeza kuwa kuwa NEMC imefanya kazi kubwa ya kuyafanya mazingira kuwa rafiki, na kuwa baraza limechukua hatua mbalimbali ikiwamo kuvifunga au kuvipiga faini viwanda ambavyo vimekiuka kanuni za kulinda mazingira.

Mussa Amrani, mjasiriamali wa Tegeta Nyuki, jijini Dar es Salaam, aliunga mkono hoja ya Mohamed kwamba ni kweli mifuko ya plastiki imepotea, lakini amelalamika kwamba wenye magenge na wenye maduka hawana karatasi za kufungia bidhaa. "Karatasi za kusitiri bidhaa ni suala la usafi pia. Tishu zipo, makasha yapo, lakini karatasi nyepesi za kusitiri bidhaa magengeni hakuna. Hii maana yake nini? alihoji.

Hivi karibuni NEMC ilitoa tathmini ya miezi 11 utekelezaji wa katazo la mifuko ya plastiki na Mkurugenzi Mkuu, Dk. Samuel Gwamaka, alieleza kuwa utekelezaji umekuwa wa mafanikio. Hata hivyo alionya kwamba vita dhidi ya mifuko hiyo haijakwisha.

# Vijana 200 EA kujadili amani

Na Mwandishi Wetu

VIJANA wa nchi za Afrika Mashariki wanatarajia kukutana jijini Arusha kujadili masuala ya amani na usalama, kama namna nzuri ya uwajibikaji kwa vijana.

Mratibu wa Mkutano huo chini ya Shirika lisilo la kiserikali la Power of Parent's Voice (PPVO), Sharon John, alisema lengo ni kuwaleta vijana pamoja kujadiliana na kushirikishana mambo mbalimbali ya nchi zao na kujifunza.

Alisema mkutano huo utafanyika mwishoni mwa Aprili, mwaka huu kwa siku tatu kukutanisha vijana zaidi ya vijana 200 kwa kujadili usalama kwa nchi na wajibu wa vijana katika migogoro na kuwa na amani endelvu, kwa maendeleo ya viwanda na jamii.

"Tumelenga Malengo ya Dunia ya mwaka 2063 ya Afrika tunayoihitaji na zaidi kipengele cha nne kinachozungumzia amani na usalama, kwanini tunahitaji amani na kwanini ni muhimu kwa maendeleo ya Afrika na dhumuni la kuwa na amani Tanzania," alisema.

"Tunataka kufungua mijadala kwa ngazi ya kimataifa kutoka kufanyika ngazi ya shuleni, na vijana kueleza changamoto wanazokumbana nazo vijana katika nyanja mbalimbali," alibainisha.

Alisema: "Kazi ya kijana katika kujenga amani ya Afrika na kwanini waingizwe kwenye kutengeneza amani, vijana ndiyo nguvu kazi ya taifa ila wanaachwa nyuma katika kujenga amani."

"Tumeona tuwafundishe kwanini tunasema tuwafundishe amani maana bila hilo maisha hayataenda kwa kuwa hakutakuwa na uchumi wala maendeleo," alisema.

Kwa mujibu wa John, lengo ni kuwaunganisha vijana zaidi ya 600 wenye fikra tofauti, kuwakuza katika elimu ili kupanua uelewa wao hivyo vijana wa hizo nchi wakikutana watajadiliana.

Alisema baada ya mkutano huo vijana hao watatembelea hifadhi za taifa na kuchangia kwenye uchumi wa nchi.

## HABARI KITAIFA

## Wanafunzi wataka elimu ya hedhi kwa walimu

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

WANAFUNZI wa kike katika Shule ya Sekondari Malagarasi Wilaya ya Kibondo, Mkoa wa Kigoma, wameomba elimu itolewe kwa walimu kuhusu hedhi ili kumwepusha mtoto wa kike na adhabu.

Ombi hilo limetolewa na wanafunzi wa kidato cha tano na sita katika shule hiyo wakati wa ugawaji wa taulo za kike zilizotolewa na Shirika lisilo la kiserikali la Oxfarm pamoja na Chama cha Wafanyakazi wa serikali na afya (TUGHE).

Noela Alexander, mwanafunzi wa shule hiyo alisema, walimu wanapaswa kutambua kuwa kuna baadhi ya wanafunzi wanapitia maumivu makali wanapokuwa katika mabadiliko hayo, hivyo utolewaji wa adhabu ni kama unyanyasaji dhidi yao.

"Ningeomba wawashauri walimu wawaeleze hili ni tatizo waelewe mabadiliko hayo hata kama wanasema si ugonjwa ni hali ya kawaida ya mwili, lakini ni tatizo kwa wengine na ikitokea mtu ana tatizo hilo atiliwe maanani kama ruhusa apewe au dawa," alisema.

Alisema baadhi yao wanapitia maumivu kipindi chote cha hedhi na kusababisha kukosa baadhi ya vipindi vya masomo licha ya wakati mwingine kulazimishwa kuhudhuria darasani.

Mwanafunzi Anita Paulo, alisema inapaswa kuwekwa mpango wa kusaidia wanafunzi wa kike wanaotoka katika familia duni kupata taulo za kike kwa kuwa baadhi ya wanafunzi walio shule za bweni wanashindwa kumudu gharama hizo kutokana na wazazi wao kushindwa kuwapa fedha.

Glory Elirehema alisema, wanaomba uboreshwaji wa huduma za maji katika shule hiyo kwa kuwa ni kikwazo kutokana na kuwapo kwa uhaba wa huduma hiyo.

Kilio Nyoroka, Mwakilishi kutoka Oxfarm alisema, wanatoa elimu ya hedhi salama pamoja na kuwagawia taulo za kike zinazodumu kwa muda wa mwaka mmoja.

Jumla ya taulo za kike 170 na vifaa vingine vinavyotumika katika hedhi vimetolewa ikiwamo chombo cha kufulia, sabuni, kanga na nguo za ndani vyenye thamani ya Sh. milioni tano.

# Mafuriko yakata daraja lingine Moro

**Na Christina Haule, MOROGORO**

MVUA zinazoendelea kunyesha mkoani Morogoro, zimeendelea kusababisha mafuriko katika maeneo mbalimbali na kuleta madhara kwa wananchi na kusababisha kukatika kwa daraja la Mto Vbandani lililopo mtaa wa Mgonanzelu kata ya Mbuyuni Manispaa ya Morogoro.

Mvua hiyo imesababisha maji na tope kujaa kwenye nyumba za watu, mali kuharibika na wengine wakihama makazi yao.

Akizungumza na Nipashe, Meneja Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) Manispaa ya Morogoro, Mnene James, alisema daraja hilo lilibomoka majira ya asubuhi baada ya mvua iliyoanza kunyesha Machi 9 hadi saa 5.

Alisema, mvua hizo zimeendelea kuharibu miundombinu hiyo, na kwamba ofisi ya mkoa inafanya tathmini ili kuona umuhimu wa kuweka daraja lingine ambalo litakamilika hivi karibuni na kurejesha mawasiliano vizuri kati ya wakazi wa maeneo ya Sabasaba na Boma.

James alisema chanzo cha maji na udongo kuingia kwenye nyumba za watu na kukatika kwa daraja ni mvua kubwa zinayonyesha na kusababisha maji kwenda yakiwa na magogo makubwa na takataka kutoka maeneo ya Milima Uluguru.

Alisema, wanaendelea na jitihada za kutoa magogo na udongo kwenye madaraja ili maji yapite bila kusababisha madhara.

Naye Diwani wa Mbuyuni, Samuel Msuya, alisema licha ya mvua hizo kutoleta maafa kwa binadamu, zimesababisha madhara kwa wakazi wa kata hizo, ikiwamo kuharibiwa mali zao, huku nyumba sita zikipata athari ikiwamo kubomoka na mali kuibwa.

Msuya alisema, kubomoka kwa daraja hilo kunaweza kukaleta madhara kwa jamii kufuatia huduma za kijamii zikiwamo zahanati na shule.

Aidha, alisema ameshaanza kuchukua hatua ikiwamo kupiga dawa za kuzuia magonjwa ya milipuko, huku mkurugenzi ameshaomba ifanywe tathmini kujua kaya ngapi zimeathirika huku wakiendelea na juhudi za kurejesha daraja.

Mvua kubwa zilizoanza kunyesha tangu Machi 6, mwaka huu, zimesababisha vifo vya watu watatu Manispaa ya Morogoro waliosombwa na maji na kuharibu miundombinu katika baadhi ya maeneo.

Mvua pia iliharibu daraja wilayani Gairo, na kuharibu daraja katika barabara kuu ya Morogoro-Dodoma.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya siku tano ya maadili kwa utumishi bora kwa watendaji wa wilaya hiyo, jijini Dar es Salaam juzi, yatakayotolewa na wakufunzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kigamboni. Kushoto ni Mkuu wa Chuo hicho. Prof. Shadrack Mwakalila. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# THRDC: Watetezi wanahofia usalama

**Na Beatrice Shayo**

MRATIBU wa Kituo cha Haki za Binadamu (THDRC), Onesmo Olengurumwa, amesema hali ya watetezi wanawake katika kizazi cha leo imegubikwa na changamoto nyingi ikiwamo kuhofia usalama wa maisha yao.

Alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo THDRC iliwaalika wanawake wakongwe na chipukizi katika utetezi wa haki za binadamu.

Alisema baadhi ya changamoto zinazodidimiza utetezi wa haki za binadamu kwa kundi hilo ni kutokuaminiana, kukosa umoja, mifumo kandamizi, uwoga kutokana na changamoto za kiusalama.

"Wengine kuingia katika nafasi walizonazo kama ajira pekee na kukosa ari na moyo wa utetezi," alisema Olengurumwa.

Aliongezea: "Tofauti kubwa kati ya utetezi wa kizazi cha kwanza na kizazi cha leo ni kuwa watetezi wanawake wa awamu ya kwanza waliingia katika utetezi kama harakati na wengi wa watetezi wa leo wameingia katika utetezi kama ajira."

Alisema kizazi cha leo wamejikita katika utetezi finyu wa makundi ya haki pekee na kuacha kuangalia haki za binadamu kwa ujumla kupitia makundi ya haki na pamoja kama ilivyokuwa kizazi cha kwanza.

"Kizazi cha leo kimeshindwa kuonyesha uhusiano kati ya haki wanazopigania mathalani haki za mtoto au wanawake na masuala ya utawala bora, utawala wa sheria na siasa safi," alisema.

Aidha, alisema kutokana na sababu alizozitaja hali ya utetezi wa haki za binadamu Tanzania umezidi kushuka ukizingatia wanawake ndio jeshi nzuri na kubwa la utetezi wa haki za binadamu nchini.

Olengurumwa alisema ili hali ya utetezi wa haki za binadamu irejee katika mstari wake ulionyooka hakuna budi kuhakikisha kundi la watetezi wanawake wanakumbushwa umuhimu wao katika sekta ya utetezi wa haki za binadamu nchini katika kutatua changamoto na kuboreshewa usalama wao wakati wa utetezi.

Alisema takwimu zinaonyesha mashirika mengi ya haki za binadamu kwa sasa yanaongozwa na wanawake, hivyo watumie fursa hiyo kama taifa kuamsha hari na moto wa utetezi wa haki za binadamu.

Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Hellen Kijo Bisimba, alisema wamefanya kampeni ya kubadilisha sheria kandamizi ingawa jambo hilo linaendelea mahakamani.

"Utakuta mtu anafuatilia kesi yake akikaribia kushinda anapigwa chini hilo ni changamoto hasa sheria za mirathi ni kaa la moto," alisema.

Alisema kwenye masuala ya ukatili wa kijinsia kila mmoja analipigia kelele, hivyo hilo ni jambo nzuri.

HABARI KITAIFA

## Sera ya ubunifu sasa yafanyiwa maboresho

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, amesema serikali inafanya maboresho ya sera ya ubunifu kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi kwa wadau wote wanaofanya shughuli hizo nchini.

Pia amewataka wabunifu kufanya kazi za kibunifu zinazoleta mapinduzi na zinazotatua kero mbalimbali nchini hususani vijijini.

Ole Nasha alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua Wiki ya Ubunifu ambayo inashirikisha wabunifu zaidi ya 6,000 kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Alisema pamoja na kuwapo kwa sera hiyo inayosimamia masuala ya ubunifu, lakini kuna haja ya kufanyiwa maboresho ili kuendana na wakati uliopo.

"Ninafahamu tayari ipo sera ya ubunifu ambayo inafanya kazi mpaka sasa, lakini kutokana na mabadiliko ya kila siku ya sayansi na teknolojia, kuna haja ya kufanyiwa tena maboresho ili iendane na wakati wa sasa, na lengo tunataka kuweka mazingira wezeshi kwa wabunifu kufanya kazi bora zaidi," alisema Ole Nasha.

Alisema pamoja na kuendelea kufanyika kwa kazi za kibunifu, kuna haja ya kuhakikisha kazi hizo zinaleta mapinduzi katika teknolojia kwa kuhakikisha zinafanya kazi ya kutatua matatizo yaliyopo kwenye jamii na katika kipindi hiki cha ujenzi wa Tanzania ya viwanda badala ya kubaki kuwa za maonyesho.

"Ninafahamu kwa sasa Tanzania tunaendelea kupiga hatua kubwa katika sekta ya ubunifu, kazi nyingi za kibunifu zinafanyika, lakini nyingi bado hazijaanza kufanya kazi, tunaomba zote zinazobuniwa ziwe ni zile zinazofanya kazi," alisema Ole Nasha na kuongeza:

"Tunataka ubunifu usaidie kutatua changamoto za maji kule vijijini, kuleta majibu ya changamoto za afya, umeme na nyinginezo."

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech), Dk. Amos Nungu, alisema kufikisha kazi za kibunifu kwenye jamii, ni kazi ya kila mtu isipokuwa na serikali kwa upande wake inapaswa kuweka mazingira wezeshi kufikia hatua hiyo kama ambavyo inafanya kwa sasa.

Mkurugenzi Mkazi wa Mfuko wa Ubunifu kwa Maendeleo ya Binadamu (HDIF), Joseph Manirakiza, alisema hakuna mafanikio mazuri ya kibunifu yatakayoleta manufaa kama kazi za kibunifu zitakazokuwa zinafanyika ni zile zile.

"Hatuwezi kufanya kitu kile kile halafu tukategemea kupata matokeo mazuri, Tanzania ina changamoto nyingi ambazo tunahitaji kuweka ubunifu kuzitatua," alisema Manirakiza.

Wiki hiyo ya ubunifu nchini imefanyika kwa miaka sita mfululizo na inaandaliwa na HDIF na Ukaid, kwa kushirikiana na Costech na kufadhiliwa na wadau wengine wa maendeleo wakiwamo, UNDP, Unicef, UN Women, UNCDF, na Vodacom Tanzania.

# Mkuchika ataka wanawake kujitokeza kuwania uongozi

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, amesema uwapo wa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, katika nafasi hiyo kumechangia kuleta hamasa kwa wanawake wengi kuingia katika nafasi za uongozi.

Pia alisema katika awamu hiyo, Tanzania imefanya mageuzi makubwa ya kuwapatia nafasi wanawake na kuwaomba kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi mkuu mwaka huu kuwania nafasi mbalimbali za kisiasa.

Mkuchika alitoa kauli hiyo katika hafla ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani iliyoandaliwa na Chama cha Wanawake wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

"Uwapo wa Makamu wa Rais wa Kwanza mwanamke Tanzania, umeleta hamasa kubwa kwa wanawake kuingia katika nafasi mbalimbali za uongozi, tumeshuhudia uwapo wa Naibu Spika wa Bunge ambaye naye pia ni mwanamke, mawaziri, majaji wa Mahakama Kuu, Mahakama ya Rufani na wakuu wa mikoa," alisema Mkuchika na Kuongeza:

"Wengine ni Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na watendaji wakuu wa mashirika na taasisi za umma ikiwamo katika nyanja za Wakurugenzi."

Mkuchika alisema kwa kutambua uwezo mkubwa walionao wanawake katika kuleta mabadiliko katika jamii, ipo haja ya kuendelea kuwathamini, kuwalinda na kuwaendeleza ili kuwa na uhakika wa ushiriki wao kikamilifu katika mchakato wa maendeleo ya taifa.

Alisema takwimu za ulinganifu katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita inaonyesha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika kutoa nafasi za uongozi kwa wanawake.

Mkuchika alisema mawaziri na manaibu waziri walikuwa asilimia 24.5, mwaka 2019 (18.5) na mwaka huu (24.5).

Kwa upande wa Makatibu Wakuu, alisema mwaka 2018 walikuwa asilimia 11, mwaka 2019 (17) na mwaka huu asilimia 17.

Mkuchika alisema Makatibu Tawala wa mikoa walikuwa asilimia 31 mwaka 2018, mwaka jana asilimia 31 na mwaka huu asimilia 27.

Makatibu Tawala Wasaidizi alisema mwaka 2018 walikuwa asilimia 19, mwaka jana asilimia 20 na mwaka huu asilimia 21.

Wakuu wa wilaya alisema mwaka 2018 walikuwa asilimia 29, mwaka jana asilimia 29 na mwaka huu asilimia 33.

Makatibu Tawala wa Wilaya mwaka 2018 alisema walikuwa asilimia 16, mwaka jana (16) na mwaka huu (33).

Alisema Wakurugenzi wa halmashauri za serikali za mitaa mwaka 2018 walikuwa asilimia 17, mwaka jana (17) na mwaka huu (19).

Majaji alisema mwaka 2018 walikuwa asilimia 37, mwaka jana (39) na mwaka huu (35), wakati mabalozi walikuwa (22) mwaka 2018, mwaka jana (22) na mwaka huu (25).

Mbali na nafasi hizo za juu, Mkuchika alisema pia serikali inazingatia kutoa kipaumbele cha ajira kwa waombaji wa kike ili kuhakikisha kunakuwapo na uwiano wa kijinsia katika ajira hizo serikalini.




Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha (kulia), akipata maelezo ya namna ya kutumia mkaa mbadala, baada ya kuzindua wiki ya ubunifu katika eneo la Kijiji cha Makumbusho, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Msimamizi wa Uzalishaji wa Dorcas Aid International Tanzania, Justin Bonto. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wafugaji waonywa uharibifu barabara

**Na Neema Hussein, KATAVI**

UPITISHWAJI wa mifugo katikati ya barabara za lami, umetajwa kuwa moja ya changamoto ya uharibifu wa barabara hizo katika Mkoa wa Katavi.

Changamoto ilitajwa juzi na Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) mkoani hapa, Mhandisi Martin Mwakabende katika kikao cha utekelezaji na ukarabati wa miundombinu ya barabara iliyoharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha.

Mwakabende alisema wamewajulisha wafugaji kuhusiana na suala hilo, lakini tatizo hilo linaendelea.

"Hii ni moja ya changamoto ambayo inachangia sana barabara zetu kuharibika ingawa kuna changamoto zingine ikiwamo mvua, ila niseme tu mfugaji atakayebainika kuchungia mifugo katikati ya barabara hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake," alionya Mwakabende.

Kwa upande wake Mhandisi Albert Kyando, Kaimu Mratibu wa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini ( Tarura), alisema vigezo vinavyozingatiwa katika mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara katika halmashauri ni wingi wa watu, wingi wa magari na sio wingi wa kilometa tu.

Aliyasema hayo kutokana na mjumbe wa kikao cha Bodi ya Mfuko wa Barabara kuuliza swali kuhusu ni vigezo vipi vinazingatiwa katika mgawanyo wa fedha za barabara, kutokana na Halmashauri ya Tanganyika kuonekana kuwa na kilometa nyingi za barabara na kiasi cha fedha ni kidogo.

Akijibu, Mhandisi Kyando alisema: Mbona Wilaya ya Tanganyika imetengewa fedha kidogo huku barabara yake ikiwa na kilometa nyingi tofauti na halmashauri zingine... vigezo sio kuangalia wingi wa kilometa tu bali kunakuangalia wingi wa watu na wingi wa magari pia."

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, aliitaka Tarura kuhakikisha barabara ya kutoka Ilembo kwenda Gpsa inakamilika ndani ya siku 30.



# Gambo ashtukia ubadhirifu utalii

**Na Cynthia Mwilolezi, NGORONGORO**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amesema kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma, zinazotokana na makusanyo ya ushuru wa watalii na magari yao, katika geti lililopo eneo la Engasero wilayani Ngorongoro.

Geti hilo moja linakusanya ushuru kwa wilaya tatu za Mkoa wa Arusha, ambazo ni Ngorongoro, Monduli na Longido.

Gambo alisema hayo baada ya kuwasili katika geti hilo, ikiwa ni siku ya kwanza ya ziara yake ya kikazi wilayani Ngorongoro.

"Kuna taarifa za uhakika za ubadhirifu wa fedha za mapato yanayotokana na ushuru wa watalii na magari yao, zinazokusanywa kwenye geti hili, kwa sababu hii iliyoundwa Kamati na Katibu Tawala Mkoa wa Arusha,

Richard Kwitega na wakurugenzi wa halmashauri hizi... sasa nawaagiza kaeni pamoja mje na njia sahihi ya kukusanya mapato haya kwenye geti hili," alisema na kuongeza:

"Haiwezekani Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ngorongoro, Raphael Siumbu, akae hapa siku tatu akusanye zaidi ya Sh. milioni nne, halafu ninyi mnakaa hapa kwa siku tatu halafu mnakusanya Sh. 800,000," alisema.

Kuhusu miundombinu ya barabara kuharibiwa na mvua katika eneo la

Oldonyolengai, Gambo alimtaka Mhandisi Ngeleja Joshua kumwagiza mkandarasi anayetengeneza barabara hiyo, kutengeza eneo hilo mara moja, kwa kuwa barabara inameguka na magari yatashindwa kupita.

Awali Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ngorongoro, Raphael Siumbu, alisema mtandao wa wizi wa fedha hizo za ushuru ni mkubwa, kwa kuwa unahusisha pia watumishi wa ofisi yake, na kwamba uchunguzi wa kina unaendelea na baada ya siku tatu utakuwa umekamilika.

"Kwa mwaka halmashauri inakusanya Sh. milioni 200 pekee, na hii inatokana na mtandao huu wa wizi, ambao mpaka ofisini kwangu upo na kwa sasa nimebadilisha utaratibu wa kutoa 'control' namba," alisema.

Wakizungumza na gazeti hili, baadhi ya watumishi wa halmashauri hiyo, ambao hawakutaka kutajwa majina yao, wanaokusanya ushuru katika geti hilo, walisema mashine zao hazifanyi kazi kikamilifu, kutokana na shida ya mtandao katika eneo hilo, na wanawatoza watalii fedha taslimu ambazo hazilipwi kwa 'control namba'.

# Zahanati yawaletea ukombozi wafugaji

**Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA**

JAMII ya wafugaji wa Kijiji cha Irkujit Kata ya Edonyongijape wilayani Simanjiro mkoani Manyara, inatarajia kuondokana na adha ya kutembelea umbali wa kilomita 12 kufuata huduma ya afya Mji Mdogo wa Orkesumet, baada ya zahanati yao kukamilika.

Zahanati hiyo inatarajiwa kukamilika hivi karibuni, baada ya Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, kuendesha harambee juzi ya kukamilisha ujenzi huo na kupata Sh. milioni 2.4, huku Mkurugenzi wa Halmashauri ya Simanjiro, Yefred Myenzi, kuahidi kutoa mabati 66 ya kuezekea zahanati hiyo iliyofikia hatua ya lenta.

Chaula akizungumza juzi katika Kijiji cha Irkujit wakati akiwapongeza wanawake ambao ni watumishi wa halmashauri hiyo, kwa kuanzisha wazo la umaliziaji zahanati hiyo, kwa kuchangia Sh. 200,000 za kununua mifuko ya saruji.

Alisema zahanati hiyo ikikamilika itakuwa msaada kwa jamii ya wafugaji, hasa wanawake na watoto waliokuwa wanafuata huduma ya afya Mji Mdogo wa Orkesumet.

"Binafsi nawachangia Sh. 250,000, na nimeendesha harambee ya papo kwa papo ya kula keki nimepata Sh. milioni 2.4 ambazo kati ya hizo ahadi ni Sh. milioni 1.5 na fedha taslimu Sh. 940,000... hii ni hatua kubwa nasema sasa zahanati yetu itakamilika hivi karibuni," alisema.

Myenzi alisema binafsi amechangia Sh. 200,000 na halmashauri itatoa mabati 66 ya kuezekea zahanati hiyo.

Myenzi alisema atahakikisha baada ya zahanati hiyo kukamilika watawaleta watumishi akiwamo mganga na wauguzi ili watu wakiugua wapatiwe matibabu katika zahanati hiyo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Asia Ngalison, aliwashukuru wanawake walioanzisha mchakato wa kuchangia zahanati hiyo kwani imeleta tija kwa jamii.

"Pia tunamshukuru mkuu wetu wa wilaya kwa kutuendeshea harambee ambayo imekuja na manufaa makubwa kwani zahanati hiyo itakamilika hivi karibuni," alisema.

Mkazi wa Kijiji cha Irkujit, Joyce Michael, alisema ni muda mrefu wanapata adha ya kutembea umbali wa kilomita 12 kwenda na 12 kurudi kufuata huduma ya afya Orkesumet.

Alisema kukamilika kwa zahanati hiyo ni ukombozi kwao hasa wanawake na watoto, ambao ndiyo walikuwa waathirika wakubwa wa changamoto ya ukosefu wa zahanati.

Sera ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaelekeza kila wilaya iwe na hospitali, kila kata iwe na kituo cha afya na kila kijiji kiwe na zahanati.



Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo (kulia mwenye miwani), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 80 kwa Mtendaji wa Jinsia kutoka Shirika la World Education Inc (WEI) Bantwana, Grace Muro, kwa niaba ya vikundi vya wanawake, ili isaidie wanawake katika vikundi vyao vya uzalishaji, zilizotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu juzi, katika sherehe za kilele cha Siku ya Wanawake iliyofanyika katika viwanja vya Mazingira Bora. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# DC ataja mwarobaini ubakaji watoto

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, amewaomba wanawake kutowaamini watoto wa kiume wa ndugu zao na kuwaachia watoto wao kulea, ili kupunguza idadi ya matukio ya ubakaji na ulawiti vinavyoshamiri wilayani humo.

Ombi hilo alilitoa jijini Arusha, wakati akizungumza na kinamama kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo kitaifa yalifanyika Jumapili, lakini Halmashauri ya Jiji la Arusha waliadhimisha Jumatatu.

Alisema familia nyingi zinakumbwa na matukio hayo kutokana na kuwaamini kupita kiasi watoto wa mjomba, dada na ndugu wengine, jambo ambalo kwa sasa kila mmoja anapaswa kuacha na kuchukua tahadhari.

"Mimi nawaomba kinamama acheni kabisa kuamini watoto wa ndugu, kwani matukio mengi ya ubakaji na ulawiti yanafanywa na watoto wa ndugu, ambao wa damu, tena ikiwezekana chukueni tahadhari hata kwa baba wa watoto wenu, maana wengine baadhi wanabaka na kulawiti watoto wao wa kuwazaa, msiamini mtu kupita kiasi," alisema.

Aidha, aliwasihi wanawake kusaidiana kurudisha jamii kwenye maadili, kwani yameporomoka kupita kiasi.

"Nawaomba tusaidiane kuwarudisha watoto wetu kwenye kuwajenga kiroho kwa kuwahimiza kwenda nyumba za ibada kanisani au msikitini kutegemea na imani ya kila familia... kwa kufanya hivi itatusaidia sana kujenga taifa lenye hofu ya Mungu na kuwa na maadili mema katika jamii," alisema.

Pia alikemea jamii za wafugaji pembezoni mwa Jiji hilo kuacha kubagua watoto kwa kusomesha watoto wa kiume pekee na kudharau wa kike. Daqarro alisema ni vema kila mtu akafahamu mtoto wa kike akisoma jamii nzima imeelimika, na asilimia kubwa ndio viongozi wazuri wa baadaye na waangalizi wa familia, tofauti na watoto wa kiume.

Alisisitiza lazima kila familia ikazingatia usawa wa kijinsia na kukemea na desturi zilizopitwa na wakati.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Arusha, Jasmine Bachu, aliwaomba wanawake kupendana na kuacha chuki miongoni mwao, ili wasaidiane kushika nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu.





# Ajira zanukia kiwanda cha ngozi

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

MKUU wa Gereza la Karanga lililopo Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, Rajab Igongi, ameweka wazi kuwa ajira za kiwanda cha bidhaa za ngozi kinachojengwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), kwa ubia na jeshi hilo zitahusisha wataalamu mbalimbali ambao si askari.

Igongi aliyasema hayo juzi, wakati Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira na kamati yake ya ulinzi na usalama walipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa kiwanda hicho kipya cha kwanza nchini.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa (Mghwira), wananchi wa Kilimanjaro ndio watakaonufaika kwa kupata ajira kwa sababu kiwanda hiki kitaajiri wataalamu mbalimbali ambao si askari kuja kufanya kazi hapa," alisema.

Ujenzi wa kiwanda hicho utagharimu, zaidi ya Sh. bilioni 75.3 na unatarajia kukamilika mwezi Februari mwaka huu na ujio wake utafungua fursa za ajira kwa watu zaidi ya 4,000.

Akiwa katika eneo la ujenzi wa mradi huo, Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Mghwira alipata fursa ya kuzungumza na uongozi wa Gereza la Karanga pamoja na kutembelea majengo mbalimbali yanayojengwa katika eneo hilo la mradi.

Igongi alisisitiza kuwa kiwanda hicho kitakapoanza kazi kitachangia mapato kwa kuwa mamlaka mbalimbali za kukusanya mapato zitakusanya kodi kutokana na uzalishaji wa kiwanda hicho.

Mradi huo ulianza mwezi Oktoba, mwaka jana na ulitarajiwa kukamilika Machi, mwaka huu.

Kulingana na takwimu za Wizara ya Mifugo, ngozi ghafi inayotokana na mazao ya mifugo, zaidi ya vipande milioni nane huwa vinapotea, kati ya vipande milioni 10 vinavyozalishwa nchini.

**"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa (Mghwira), wananchi wa Kilimanjaro ndio watakaonufaika kwa kupata ajira kwa sababu kiwanda hiki kitaajiri wataalamu mbalimbali ambao si askari kuja kufanya kazi hapa," alisema.**

# Wanafunzi wanusurika kifo wakisali wilayani Hai

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

WANAFUNZI 36 wa Seminari ya Kiislamu ya Mudio iliyopo Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, wamenusurika kifo, baada ya bweni lao kuteketea kwa moto wakiwa wanasali sala ya magharibi.

Mkuu wa sekondari hiyo, Said Zuberi, alithibitisha jana kuwa bweni hilo liliwaka moto na kuteketea Machi 9, mwaka huu, majira ya saa 12:30 jioni na kusababisha baadhi ya wanafunzi wanaolala katika bweni hilo kupoteza vifaa mbalimbali.

"Ni kweli bweni hilo liliungua wakati wanafunzi wakiwa wamekwenda kusali swala ya Magharibi. Moto ulianza kwa kuteketeza chumba kimoja cha bweni hilo lililokuwa na wanafunzi 36, lakini hakuna mwanafunzi aliyejeruhiwa," alisema.

Nipashe ilipomtafuta jana Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Salum Hamduni, kuzungumzia ajali hiyo ya moto, alijibu kwa kifupi kwamba hana taarifa kamili kuhusu tukio hilo, ingawa anajua kuna moto ulitokea.

"Kuna vitu vingi vimetokea hapa katikati, sasa ukinishtua kwa kutaka taarifa kwamba ni nini kinaendelea nitakuwa nakundanganya, lazima tuwe na uhakika na kinachosemwa tutawajulisha," alisema Kamanda Hamduni.

Kwa mujibu wa Mkuu wa sekondari hiyo, chanzo cha moto huo bado hakijajulikana na kwamba kuna wanafunzi wanne wa kidato cha tatu wamehojiwa na polisi kuhusu tukio hilo.

Alisema baada ya kutokea ajali hiyo, wanafunzi, walimu pamoja na wananchi waliojitokeza katika hatua za awali na pia askari wa Kikosi cha Jeshi la Zimamoto na Ukoaji kiliwahi kufika kwenye eneo hilo na kukuta moto umezimwa na wananchi.



Ofisa mwezeshaji, Eliwilimina Buberwa kutoka Taasisi ya Maendeleo Uru ya Moshi, akitoa elimu ya namna ya kutengeneza taulo za kike kwa njia rahisi, kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Mangi Sabasi na Mawela Sekondari, mjini Moshi mkoani Kilimanjaro, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wanafunzi familia duni wakosa vipindi 36

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

BAADHI ya kaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro ambazo zinatishiwa na kipato duni, watoto wa kike wanaotoka kwenye familia hizo wanadaiwa kukosa vipindi 36 kila mwezi shuleni, kutokana na kushindwa kumudu gharama za kununua taulo za kike.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mtendaji wa Taasisi ya Maendeleo ya Uru (UDF), Wakili Wilhard Kitali, utafiti unaonyesha kuwa wanafunzi wa shule za sekondari na msingi hasa eneo la Moshi Vijijini, wanakosa vipindi si chini ya siku tisa kwa siku.

Wakili Kitali alitoa mrejesho huo jana mbele ya mahakimu wakazi, mawakili, wataalamu wa maendeleo ya jamii na wadau mbalimbali katika Sekondari ya Mangi Sabasi, iliyopo Kata ya Uru Kusini, wakati wa uzinduzi wa programu ya 'Binti Baki Darasani.'

"Suala la hedhi salama tumeliona pia ni tatizo kubwa ambalo linawakumba wanafunzi wengi. Baada ya kufanya utafiti, tumegundua kwamba wako wanafunzi ambao wanakosa vipindi si chini ya siku tisa, kwa maana kwa siku wanafundishwa vipindi tisa na wanafunzi wa kike wanapokuwa kwenye hedhi, wako baadhi yao wanakosa masomo kwa siku nne na wengine wanakosa hadi siku saba. Ukifanya hesabu ya nne mara tisa, unapata 36."

"Kwa mwezi, kuna mtu anapoteza vipindi 36 kwa sababu tu amekosa Sh. 2,000 ya kununua taulo za kike. Sasa Uru Development Foundation tukaguswa na tukaona tuje na kampeni hii ambayo inaitwa 'Binti Baki Darasani', ambayo lengo kubwa ni kuwasaidia wale wasiokuwa na uwezo kugawiwa taulo za kike bure ili waweze kubaki darasani, wapate elimu vizuri na wasome vizuri na siku moja wawe mahakimu, mawakili, walimu, madaktari na wakumbuke kurejesha fadhila kwa wenzao wasiokuwa na uwezo wa kununua vitu hivi."

Akizungumza na wanafunzi wa shule za sekondari za Mangi Sabasi na Mawela, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Moshi, Julieth Mawole, alisema baadhi ya mila na tamaduni, suala la hedhi linapewa tafsiri potofu na hivyo kuongeza changamoto kwa watoto wa kike.

"Naamini mpango huu wa UDF, utawasaidia sana watoto wa kike wasome wakitambua kuwa zipo taasisi na Watanzania wanaowajali na kutambua changamoto za kijinsia wanazopitia," alisema Hakimu Mawole.

Meneja wa Chama wa Ushirika cha Akiba cha Kuweka na Kukopa Moshi Vijijini (M.R.T Saccos), ambaye ni Mkurugenzi wa Hugos Garden, Bosco Simba, alishauri taasisi hiyo kuhakikisha taulo za kike inazotoa zinamaliza au kupunguza kabisa tatizo hilo Moshi Vijijini.

"Mmetueleza hapa kwamba shughuli zenu mmejikita zaidi kusaidia utoaji elimu, tunataka kuona ufaulu unaongezeka, tunataka kuona hawa wanafunzi wanafika mbali katika elimu.

"Kwa hiyo pamoja na mambo mengine mnayoyafanya kwa kushirikiana na jamii inayowazunguka, hamasisheni wadau mbalimbali kuchangia kwenye elimu ikiwamo chakula shuleni, ujenzi wa vyoo bora, madarasa lakini kwa wale wanafunzi ambao hawana uwezo kabisa, taasisi yenu ifanye utaratibu wa kuwasaidia japo kuwachangia kidogo katika masuala mbalimbali shuleni."



Ukurasa 15

## Wasomi duniani, Mangula walivyomuibua upya Nyerere

## Siku ya wanawake inapotumiwa kuainisha ajenda za uchaguzi




Ukurasa 14



Ukurasa 17

## Wanajeshi Marekani waanza kuondoka nchini Afghanistan


# siasa

JUMATANO MACHI 11, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 19

## Pérez de Cuéllar Katibu Mkuu aliyeacha alama zisizofutika UN

KATIBA MPYA...

# Kuitwa kiporo kilichochacha, kwa nini kuruhusu kichache?

**Na Mwandishi Wetu**

MCHAKATO wa kuandika katiba mpya ulianza baada ya Rais Jakaya Kikwete, kuteua wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, ambao jukumu lao lilikuwa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu muundo wa katiba wanayoitaka.

Hata hivyo, mchakato huo haukuhitimishwa kwa kuipatia nchi katiba iliyopendekezwa na sauti za umma zinasikika kuuliza lini andiko hilo litapatikana?

Wakati hayo yakizungumzwa, ni wazi kuwa mabilioni ya shilingi yalitumiwa na wajumbe wa tume, bunge la katiba na shughuli nyingine za kufanikisha suala hilo, lakini halikufanikiwa.

Hivi karibuni Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Dk. Bashiru Ally, analipigilia msumari suala hilo, akieleza kuwa katiba mpya ni kiporo kilichochacha na hakifai kupasha moto kwa namna yoyote.

Mtendaji Mkuu wa CCM ana-

**INAENDELEA UK.16**



Katibu Mkuu wa CCM, Bashiru Ally. **PICHA: MTANDAO**

## William Ruto anapokandamizwa na utata wa kifo cha mlinzi wake

Ukurasa 20

# Siku ya wanawake inapotumiwa kuainisha ajenda za uchaguzi




Mwenyekiti Mbowe akiwa na wanachama wa Bawacha kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Jumapili Machi 8, 2020. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

JITIHADA ya kupata nafasi ya kuweka msingi wa ajenda za kutumia katika uchaguzi mkuu baadaye mwaka huu, ambao serikali imejitahidi kuyakinisha kuwa utakuwa huru na wa haki, zinaendelea kwa upande wa Chadema, ukiangalia wapi pa kuzipenyezea.

Hali hiyo inatokana na mazingira ya kutokuwapo mandhari ya kuanza shughuli halisi za kisiasa kitaifa nje ya maeneo ya uwakilishi yaani ndani ya majimbo ya uchaguzi waliko wapiga kura wa mbunge husika.

Kwa njia hiyo, uwepo wa shughuli ya kitaifa iliyoruhusiwa kwa mfano wakati wa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani, Jumapili Machi 8 kulitoa nafasi ya kuziainisha sera za uchaguzi za vyama vya siasa.

Mwenyekiti wa chama hicho kitaifa, Freeman Mbowe, anatumia nafasi aliyopewa kama mgeni rasmi wa adhimisho la Baraza la Wanawake la Chadema (Bawacha) kutoa salamu kadhaa zenye lengo la kutoa mwelekeo wa jumla na hata majukumu ya makundi tofauti ya jamii kuelekea uchaguzi mkuu.

Kwa kutumia jukwaa hilo, Mbowe anaainisha umuhimu wa wanawake nchini 'kuacha kulalamika na kuamka, kubadili mawazo na kupigania nafasi zilizoko kwa maendeleo yao.'

Wakati kimsingi hitaji hilo ni la maendeleo ya wanawake kiuchumi na kijamii kwa jumla, kuna mambo ya kuelekea uchaguzi mkuu yanayohitaji kuiainisha kwa undani zaidi.

> Hawakufika tu kama watazamaji bali wakiingia pembeni ya mkutano na hatua kwa hatua wakajiunga katika mkusanyiko wenyewe wakiwa bado kundi kubwa, wakiimba na kucheza.

Haikuwa ni mara ya kwanza kumsikia mwenyekiti huyo akieleza matumaini yake kuwa katika uchaguzi mkuu ujao chama hicho kinaweka mkazo sana kwa kundi hilo la wanawake.

Zipo sababu kadhaa za kufanya hivyo ambazo baadhi zilianza kuonekana mapema kabla hata mwaka haujaanza, yaani katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Mei Mosi, mwaka jana, katika mikusanyiko tofauti.

Ilikuwa kielelezo au kioo cha jamii, ni kundi gani katika jamii linaweza kukusanyika na kujenga uelekeo wa hoja, au ushiriki kisiasa wenye mwelekeo wa upinzani usiokuwa na mashaka mashaka, na ikaonekana kuwa labda kundi la wanawake lina uwezo huo.

Siku ya Wafanyakazi mwaka uliopita kulikuwa na maandamano tofauti kote nchini kwa ajili ya maadhimisho hayo, ila ingawa kimsingi ni sikukuu ya kitaifa, hivyo inahitaji kuadhimishwa kiserikali, kwa jumla mwelekeo ulikuwa ni kuiadhimisha kichama.

Hata katika mkusanyiko ambao ni kama ulikuwa wa kitaifa mkoani Geita, wilayani Chato, mkutano mkubwa uliopangwa kiserikali ulikuwa na wajumbe wengi waliokaa jukwaani wakivalia magwanda ya chama tawala.

Hivyo ilikuwa wazi kuwa maadhimisho yalikuwa yanafanyika kichama na siyo kiserikali, licha ya kuwa ndiyo mkutano pekee uliopewa kibali na polisi.

Kilichotokea ni kuwa kundi kubwa hasa la wanawake wanaounga mkono upinzani ambao waliruhusiwa safari hii kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake kivyao walikusanyika eneo fulani halafu badala ya kufanya mkutano huo (ambao ungetawanywa kwani haukuwa na kubali) wakaenda kwenye mkutano mkubwa.

Hawakufika tu kama watazamaji bali wakiingia pembeni ya mkutano na hatua kwa hatua wakajiunga katika mkusanyiko wenyewe wakiwa bado kundi kubwa, wakiimba na kucheza.

Ilikuwa ni burudani ya muda mfupi na huyo aliyeweka mkanda huo kwenye mtandao wa You tube hakuweka kipande kinachoonyesha kilichofuata kilikuwa nini.

Ndiyo mandhari inayoeleza kuwa Chadema ina tumaini ambalo halijifichi kuwa ni katika kundi la wanawake kijamii na pia katika chama chenyewe kuwa labda huko wanaweza kupata msukumo unaohitajika kupeleka ajenda hii au ile wakati wa uchaguzi mkuu.

Suala la msingi la kuweka tegemeo kwa kundi la kinamama ni la kijamii na kisaikolojia, licha ya kuwa mijadala inawezekana kama mwelekeo huo ni sahihi au la.

Ni jambo linalohitaji kutatuliwa na kujua kama katika mazingira ya kisiasa yaliyopo nchini, ni kundi gani linaloweza kutumainiwa kuwa ngome ya siasa za upinzani, kama ni vijana, watu wa kawaida (wanaume watu wazima) au ni wanawake.

Kujibu swahi hilo katika mandhari mapana ya siasa nchini pia inawezesha kujibu hoja ya kuweka mikakati ya kundi gani linaweza kukisaidia chama, kama jumuia ya chama, katika uchaguzi mkuu.

Ziko tofauti za kijamii na pia katika chama kati ya makundi hayo matatu na lipi linaweza kutumainiwa kuwezesha chama kufikia malengo, ambako maandamano ya Mei Mosi au ni mwaka uliotangulia?) yaliweka bayana ni kundi lipi ambalo lina uwezo wa kudiriki kusimama kidete kutetea agenda za upinzani kwa jumla na Chadema yenyewe.

Hilo ni tukio ambalo lilionyesha uthubutu na kudiriki kuwa katika mazingira ya sasa, inawezekana ni wanawake ndiyo wanaoweza kusimama kidete zaidi endapo kuna jumuiko limepangwa, au linahitaji kuendeshwa au kuelekezwa katika mpangilio fulani. Si rahisi kusema ni kwa njia gani jumuiya ya wanawake ndiyo ikawa na uwezo wa kujikusanya na kuingilia mkutano wa hadhara wa CCM uiokuwa na nembo ya mkutano wa kitaifa wa sikukuu ya wafanyakazi.

Wala siyo rahisi kueleza kama viongozi wa Chadema walipanga tukio hilo au ni viongozi wa jumuia hiyo wilayani Chato waliojituma, wakadiriki na kuwezesha uongozi kitaifa ugundue hilo.

Ukiangalia chama hicho katika miaka kadhaa iliyopita, unapata picha kuwa kimepoteza makada wengi zaidi kutoka kwa kundi la waliojiunga katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu uliopita pamoja na kundi la vijana.

Chadema haijapoteza viongozi kutoka Bavicha hivyo ni wazi kuwa ni kundi lenye umoja zaidi katika chama ukilinganisha na mengine. Kwa njia hiyo,

Mwenyekiti Mbowe anakuwa 'nyumbani'zaidi akijenga hoja kwao kuliko ambavyo angejisikia akitaka kufanya hivyo kwa makundi yanayoyumba na kuangalia mambo mengine ya nje.

# Wasomi duniani, Mangula walivyomuibua upya Nyerere

## • Wanazuoni Italia wataja alivyosimamia utu, haki, maendeleo kwa Tanzania na Afrika



Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Philipo Mangula, alipotembelea shamba na kukagua kilimo cha korosho kwenye mradi mkubwa wa shamba la pamoja lenye zaidi ya ekari 12,000 eneo la Masagati wilayani Manyoni . **PICHA: JOHN MAPEPELE.**

**Na John Mapepele,** SINGIDA

NOVEMBA 2019, Chuo Kikuu cha Urbaniana, kilichoko mjini Roma Italia kilimtafakari Baba wa Taifa Julius Nyerere, ambaye ni Mwanamajumui wa Afrika (Pan Africanist) kuhusu fikra na mchango wake kwa maendeleo endelevu Tanzania, Afrika na duniani.

Shabaha yake ni kuchangia kumtambulisha kiongozi huyu aliyejibidiisha kusarifu kwamba siasa ni tunu faradhi ya upendo kwa sababu lengo lake ni kukuza faida na maendeleo ya wote.

Ukumbi mkubwa wa Papa Mstaafu Benedikto wa XVI ulifurika wahadhiri, wageni na wanafunzi kutoka ndani na nje ya chuo hicho kufuatilia kwa makini mada na majadiliano kuhusu mchango wa Mwalimu Nyerere katika kusimamia utu, heshima, haki, ustawi na maendeleo ya Watanzania na Afrika.

Katika hotuba yake, Balozi wa Tanzania nchini Italia, George Kahema, alibainisha kwamba maisha, fikra na mawazo ya Nyerere yamefumbatwa na uadilifu, bidii, usawa, mshikamano na uvumilivu usio na kipimo.

Kama mtumishi wa serikali, utendaji kazi wa Nyerere ulisadifu kwa dhati fadhila na tunu msingi za maisha ya imani, matumaini na mapendo kwa Mungu na unyenyekevu uliotukuka kwa watu aliowatumikia.

Balozi Kahema anasema Nyerere alikuwa nguzo ya msingi ya kuwaunganisha Watanzania katika hekima, umoja na amani, tunu zilizowalea wote katika lugha moja ya Kiswahili na kuwawezesha kutambuana na kuishi kama ndugu licha ya wingi wa makabila yanayopatikana nchini.

> “Nyerere alisisitiza kwamba watu wasiokubaliana na kutoelewana wanapaswa kujifunza kukubali na kuwa tayari kuishi pamoja, licha ya tofauti zao.

Bidii yake ya kuwatumikia Watanzania kwa weledi na uadilifu mkubwa, itaendelea kumfanya Nyerere kuwa mwalimu maridhawa wa imani na siasa safi kwa vizazi vingo vya Tanzania na duniani kote.

### KIU YA UKOMBOZI

Kahema anasema Mwalimu aliamini kuwa amani, maendeleo na salama ya Tanzania inahusisha kwa karibu mataifa mengine, hivyo Nyerere alikuwa daima tayari kusaidia mataifa mengine ya Afrika kujikwamua katika madhila ya ukandamizaji na harakati ukombozi, umaskini, misukosuko na hali mbovu za kisiasa.

### KUMUENZI MWALIMU

Msimamo wa Mwalimu na makubwa aliyoifanyia Tanzania na Afrika umekuwa utangulizi wa kuakisi ziara ya hivi karibuni aliyoifanya Makamu wa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (Bara), Philipo Mangula kwa siku saba mkoani Singida na kutumia muda mwingi kusisitiza amani, upendo na mshikamano Nyerere aliwaachia Watanzania Baba wa Taifa.

Anadokeza kuwa maendeleo makubwa yaliyopatikana katika kipindi hicho ambacho aliitoa Tanzania chini na kuipandisha juu, akiiacha ikiwa na vyuo vikuu, shule za sekondari karibu kila mkoa na wilaya, hospitali za rufani, barabara na mashirika mengi ya umma pamoja na viwanda vya kila aina si kazi ndogo.

Makamu Mwenyekiti anasisitiza kuyatafakari kwa kina ili kulinda na kudumisha kazi ya Mwalimu katika kipindi hiki ambacho Tanzania inawindwa na maadui wa kutoka ndani na nje ya nchi kwa kujifunika mwavuli wa ukuzaji wa demokrasia.

Ziara ya Makamu Mwenyekiti, inaakisi maono ya Mwalimu Nyerere huku katika majumuisho ya ziara yake aliyoyafanya wilayani Manyoni anasisitiza kwamba Nyerere ni mtu, kiongozi, nguzo na Mtanzania muhimu aliyetoa mchango wake mkubwa katika harakati za kuwaelimisha Watanzania na Afrika kwa ujumla kutumia akili zao wenyewe kubuni mifumo ya kujitegemeza na kujikwamua katika wimbi la umaskini, ujinga na maradhi; maadui wakubwa wanaoendelea kuliumiza taifa na bara hili hata sasa.

Anasema Mwalimu Nyerere alijaa busara na kujiepusha na hila za mataifa ya kigeni mintarafu amani, umoja na maendeleo fungamani ya Tanzania na Afrika katika ujumla wake.

Kama kiongozi makini Nyerere alisimama kidete kuunda umoja miongoni mwa Waafrika. Azma na bidii ya Baba wa Taifa na viongozi wenzake wengine pia ilikuwa ni kuiunganisha Afrika nzima kuwa moja kwa kuunda Umoja wa Afrika ambao hata sasa licha ya kwamba haujatimiza malengo ya mtangamano ulianzishwa na Nyerere na Kwame Nkurumah wa Ghana.

Anakumbusha kuwa hili lilikuwa jambo muhimu lakini lenye changamoto kubwa na tete sana kwa sababu ya utofauti mkubwa wa lugha, tamaduni, dini, makabila na hata ukomavu wa kifikra.

Mwalimu alikazia kuungana hatua kwa hatua, lakini kwanza kuungana kikanda ili polepole nchi majirani zijilee na kuzoea kuungana kabla Afrika yote kiujumla haijaungana.

Ni katika muktadha huu, Mwalimu Nyerere na viongozi wengine walifanya makubaliano na kujituma kuunda jumuiya mbalimbali za kikanda Barani Afrika, kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS).

Mangula katika hotuba yake kwenye kila wilaya aliyopita hakuacha kusema kwamba Nyerere alikuwa nguzo muhimu katika juhudi za usuluhishi katika migogoro mbalimbali barani Afrika.

Umahiri wake kama mwalimu, uling'aa katika mioyo na macho ya wengi. Aliwakutanisha waliotofautiana na kutumia muda kuwaelekeza na kuzungumza nao kwa busara, upole na utulivu wa hali ya juu.

Anaongeza kuwa Nyerere alisisitiza kwamba watu wasiokubaliana na kutoelewana wanapaswa kujifunza kukubali na kuwa tayari kuishi pamoja, licha ya tofauti zao.

Kabla ya kupendekeza suluhisho Nyerere alizoea daima kuanza kwanza kubainisha kanuni msingi za maisha ya mwanadamu, kufafanua miongozo na taratibu na mwishoni aliweka mapendekezo suluhishi aliyoona yangefaa kuondoa migogoro.

INAENDELEA UK.18

KATIBA MPYA...

# Kuitwa kiporo kilichochacha, kwa nini kuruhusu kichache?



Katibu Mkuu wa CCM, Bashiru Ally, akifanya mahojiano katika studio ya East Africa Radio, alipofanya ziara katika vyombo vya habari vya IPP. **PICHA: JOHN BADI**

**INATOKA UK.13**

potembelea vyombo vya habari vya IPP na kukukutana na wanahabari, anaulizwa anamaanisha nini anaposema katiba mpya ni kiporo kilichochacha na hakifai kupasha moto kwa kuwa kikiliwa watu wataumwa tumbo?

Anasisitiza kuwa: "Hili jambo tuendelee kulijadili, tusifunge milango ya mjadala kwasababu ya uzito wa mjadala wenyewe, katiba ni chombo kizito na kujenga utamaduni wa kuheshimu katiba ni moja ya wosia wa Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere. Mwalimu hakuwa na tatizo na katiba iliyopo shida yake kubwa ilikuwa ni kutotekeleza katiba iliyopo," anasema Dk. Bashiru.

"Hatukufika mwisho, na ni jambo la bahati mbaya na hasara si ya fedha tu bali tuligawanyika zaidi kuliko wakati wowote, mjadala ilipoteza mwelekeo kutoka kwenye kujenga muafaka wa kitaifa na kwenda kwenye masuala yanayomomonyoa misingi ya utaifa. Kulikuwa na tishio la uimara wa Muungano mpaka watu wengine wakasusa, kundi moja likatoka na wengine wakabaki,"anasema Katibu Mkuu wa CCM.

Kwa mujibu wa katibu huyo, kususiana kuhusu jambo la maana kama hilo siyo hasara ya fedha peke yake, ni hasara pia ya kisiasa, kitaifa na muda uliotumiwa.

> Endapo kungekuwa na mazingira yoyote yale ya kuwa na mgombea wa pamoja, Membe angeweza kuwa chaguo rahisi kufikia ila hilo haliwezekani kwa sasa.



Mwenyekiti wa Tume, Jaji Warioba (kulia) na Makamu wake Jaji Ramadhani, katika moja ya mikutano ya kufanikisha mchakato wa katiba mpya. **PICHA: MTANDAO.**

### UKAWA IKO WAPI?

Katibu Mkuu wa CCM anasema kuwa mchakato wa katiba uliopelekea kuundwa kwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), uliokuwa tishio kwa CCM kwa kuwa kwa mara ya kwanza mgombea wake alishinda kwa kura chache kuwahi kupata wagombea wengine.

Adha, kwa bendera ya Ukawa CCM ilipoteza majimbo mengi zaidi tangu kuwepo kwa vyama vya upinzani nchini, anasema.

"Rais John Magufuli, alipata kura ambazo mgombea wa CCM hajawahi kuzipata katika mfumo wa vyama vingi asilimia 58 na mgombea wetu hakuwahi kuwa chini ya asilimia 60, Rais Mstaafu Jakaya Kikwete wakati anaingia alifikia asilimia 80,"anakumbusha.

"Kususiana kwa jambo kama hili si hasara ya fedha pekee bali ya kisiasa na waliotoka wakatoka wakidhani wanaweza kuendeleza mapambano kupitia uchaguzi wa mwaka 2015 na kuanzisha Ukawa na wananchi waliwaamini kuwa watakuwa ni mwarobaini wa mambo yanayoendelea,"anaongeza Kiongozi huyo wa CCM.

### KWA NINI NI KIPORO?

Dokta Bashiru anasema kinachomsikitisha ni kuwa chombo kilichoaminiwa na wananchi ili kujenga muafaka kwa jina la Ukawa, alitamani kukiona kikiendeleza mapambano na kusukuma ajenda.

"Ndiyo maana nakiita kiporo kilichochacha, Ukawa iko wapi? Wanaweza kuingia na agenda hiyo mwaka huu? Wanaweza kuaminika mwaka huu? Walikuwa wanatafuta katiba mpya kweli? Haijapatikana wamesambaratika...kumbe ilikuwa ni geresha ilikuwa ni kuteka mchakato wa katiba mpya kutafuta Ikulu, Ikulu haikupatikana Ukawa imeshasambaratika,"anasema.

Anaongeza: "Kuwa na wanasiasa wa namna hiyo wa kuwavuta wananchi kutafuta jambo jema na kuwaacha solemba nacho ni kiporo kilichochacha. Sasa unataka kuumwa matumbo kwa kula kiporo cha namna hiyo hatujamaliza matatizo ya Corona, tuingie kwenye kuumwa matumbo. Rais Magufuli anasema hatuwezi kuwa na siasa za kinafiki watu wanatafuta Ikulu kwa kisingizio cha katiba mpya."

Anabainisha kuwa kwa sasa unapikwa mlo usiochacha kwa kuanzia chini na kwamba meza haijakosa chakula kwa kuwa katiba za nchi zipo na kwamba mjadala uwe katika kutafuta katiba bora na mpya pamoja na kuheshimu zilizopo.

"Tatizo tulilonalo si kwamba iliyopo haifai ila ilivyopatikana haikuwa na ushirikishaji wa kuzingatia mawazo ya watu ...," anafafanua.

"Ni hatari kula kiporo kilichochacha na kazi yangu kama kiongozi ni kutahadharisha, lakini bado tunaheshimu mawazo ya wananchi, mjadala tuendelee nao lakini tulinde dhamana na katiba yetu,"anaongeza Dk. Bashiru.

Anasema kwa sasa kinachotakiwa ni kuanza kupika chakula ambacho hakijachacha huku akitolea mfano wa kuanza kukata vitunguu, karoti na kuanza kulima ambavyo havijalimwa.

"Meza hazijakosa chakula, tunazo katiba za nchi mjadala uwe katika kutafuta mpya, lakini pia tuheshimu zilizopo na tatizo tulilonalo siyo kwamba haifai bali ilivyopatikana haikuwa na ushirikishwaji wa kuzingatia mawazo ya watu mbalimbali katika muktadha mpya," anasema na kuongeza;

"Yawezekana hata tukipata nyingine mpya inaweza isiwe mpya kwa maudhui, tunaweza kukuta asilimia 80 ya vifungu ni vile vile, lakini angalau tubadilishe mchakato na usiwe wa wanasiasa pakee yao na sauti zionekane zinasikika na siyo zinasemewa na wanasiasa...ni hatari kula kiporo hiki, tukiaza kuathirika na kiporo dhamana atabeba mwenye dhamana na tunaheshimu maoni ya wananchi," anasema.

### MCHAKATO KATIBA MPYA

Itakumbukwa kuwa uteuzi wa wajumbe ulifanya kwa kutumia Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 ya mwaka 2012.

Jaji Joseph Warioba akiwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti Jaji Augustino Ramadhani, waliiongoza tume iliyokabidhi rasimu ya pili ya katiba kwa Rais Kikwete Disemba mwaka 20013, kwa ajili ya kwenda kwenye hatua ya Bunge Maalum la Katiba.

Kazi kuu za tume hiyo ilihusisha mikutano ya kukusanya maoni, kuyaratibu na kuchambua maoni ya wananchi kuhusu mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuandaa ripoti inayojumuisha rasimu hiyo.

Tume hiyo ilianza kazi rasmi Mei mosi, 2012 na kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, ilitakiwa kukabidhi kazi kipindi kisichozidi miezi 20.

Wajumbe walikusanya maoni ya wananchi kutoka pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano kupitia mikutano ya hadhara na faragha kuanzia Julai 2, 2012 hadi Disemba 19 , mwaka 2012.

Taarifa ya tume hiyo kwa wakati huo ilieleza kuwa jumla ya mikutano 1,763 iliandaliwa na kufanyika katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano na wananchi 1,365,337 (wanawake 531,480 na wanaume 833,857) walihudhuria.

"Kati ya waliohudhuria, wananchi 323,001 walitoa maoni kwa maandishi na kuongea katika mikutano hiyo. Baada ya mikutano hii, tume ilipanga na kufanya mikutano na viongozi wa kitaifa waliopo madarakani na wastaafu pamoja na makundi mbalimbali ya kijamii ili kupokea maoni yao kuhusu katiba mpya,"ilisema taarifa hiyo.

Mwenyekiti wa Tume wakati huo alieleza kuwa tume pia ilipokea maoni kwa njia ya barua pepe na ujumbe mfupi wa simu za mkononi, tovuti na mitandao ya kijamii, ikiwa ni pamoja na maoni yaliyotolewa na wananchi kupitia vyombo vya habari kama vile magazeti, redio na runinga.

Tume hiyo ilikuja na rasimu ya kwanza ambayo ilikabidhiwa Juni 3 mwaka 2013 kwa aliyekuwa Makamu wa Rais Dk. Mohammed Gharib Bilal, ambayo ilipelekwa kwa wananchi wakatoa maoni kupitia mabaraza ya katiba katika mamlaka za serikali za mitaa, pamoja na asasi, taasisi na makundi ya watu wenye malengo yanayofanana.

Baada ya kukabidhiwa kwa rasimu ya katiba, sheria ilitaja aina tatu za wajumbe wa Bunge la Katiba kuwa ni wabunge wote , wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na wajumbe 201 wa kuteuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Wengine ni makundi 10 zikiwamo taasisi zisizokuwa za kiserikali 20, za kidini 20, vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu 42, taasisi za elimu 20, watu wenye ulemavu 20, vyama vya wafanyakazi 19.

Vyama vinavyowakilisha wafugaji 10, wavuvi 10, wakulima 20 na vikundi vya watu wenye malengo yanayofanana 20.

Baada ya machakato wote rasimu iliwasilishwa kwenye Bunge la Katiba, na mjadala ulianza na ilikuwa ni ichapisho, vijembe, maneno ya kuudhi ya mtaani kuliko kutengeneza katiba yenyewe, kiasi cha kugawanyika na kuunda kwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa).

> Ila kila chama kinawakilishwa na watu kadhaa wenye ushawishi katika vyama hivyo.

Oktoba mwaka 2014, katiba inayopendekezwa ilikabidhiwa kwa serikali kwa ajili ya kwenda kwenye hatua ya kuipigia kura (kura ya maoni) kwa kuwa na timu mbili za wanaounga mkono na wanaoipinga lakini yote hayakufanikiwa kwa kuwa kulikuwa na mkwamo, kwa kile kilichoelezwa kuwa katiba inayopendekezwa ilikuwa ni sawa na kuweka viraka kwenye katiba ya sasa.

## Wanajeshi Marekani waanza kuondoka nchini Afghanistan



Baadhi ya askari wa Marekani wakiwa kazini nchini Afghanistan. **PICHA: MTANDAO**

MAOFISA wa Marekani wamesema baadhi ya wanajeshi wake wameanza kuondoka nchini Afghanistan, kama ilivyokubaliwa kwenye mazungumzo ya amani na kundi la Taliban.

Hatua hiyo inafikiwa katikati ya mvutano wa kisiasa mjini Kabul.

Mamia ya wanajeshi wa Marekani wameanza kuondoka nchini Afghanistan kama ilivyokuwa imepangwa awali, lakini hawatobadilishwa kutokana na kwamba Marekani inataka kusonga mbele na mipango yake ya kupunguza idadi ya askari wake kutoka 13,000 hadi 8,600.

Kazi ya kuwaondoa askari wa Marekani inakuja wakati ambapo viongozi hasimu wa Afghanistan wote waliapishwa kuongoza nchi Jumatatu katika hafla mbili tofauti kama marais wa nchi.

Hatua hiyo imeibua wasiwasi kwa Marekani wa jinsi ya kuendelea na utekelezaji wa makubaliano ya kukomesha vita ya miaka 18.

Mvutano baina ya Rais Ashraf Ghani ambaye alitangazwa kuwa mshindi wa uchaguzi wa mwezi Septemba mwaka jana na hasimu wake Abdullah Abdullah ambaye alielezea udanganyifu katika uchaguzi, unaongeza mashaka kwa hatua muhimu inayofuata na hata kuhatarisha kutumbukia tena katika machafuko.

Mvutano huo wa kisiasa umeyatia wasiwasi mazungumzo ya ndani na kundi la Taliban ingawa Rais Ghani, ameanza kuunda timu ya majadiliano.

"Jukumu letu ni kuhakikisha amani na kumaliza miaka 40 ya vita. Nitahakikisha amani inarejea na ujasiri wa watu na mfumo wa Jamhuri," alisema Ghani wakati akiapishwa Jumatatu iliyopita.

Msemaji wa Jeshi la Marekani nchini Afghanistan Sonny Legget, anasema kwenye taarifa yake kwamba jeshi limeanza "kutimiza sharti la kupunguza wanajeshi hadi 8,600 ndani ya siku 135".

Kati ya wanajeshi 13,000 wa Marekani walioko Afghanistan, 8,000 wanajihusisha na mafunzo na kuvishauri vikosi vya Afghanistan, wakati wengine 5,000 wakishiriki kwenye operesheni ya kupambana na ugaidi sambamba kulisaidia jeshi la nchi hiyo wanapohitajika.

Ghani amekuwa akijivuta kuwaachia wafungwa karibu 5,000 wa Taliban, kitu kilichokubaliwa kwenye mkataba wa amani wa Taliban na Washington.

Lakini hivi karibuni Ghani aliahidi kwamba atatangaza amri ya kuachiliwa wafungwa, baada ya Marekani na maofisa kadhaa wa kigeni kuunga mkono juhudi hizo."

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Mike Pompeo, anapongeza hatua hiyo ya Ghani ingawa "alipinga vikali" kuanzishwa kwa serikali mbili mjini Kabul.

Pompeo anaonya juu ya "matumizi yoyote ya nguvu kusuluhisha tofauti za kisiasa". Viongozi wote hususan Abdullah wanaungwa mkono na wababe wa kivita na wanamgambo waliojihami kwa silaha na hivyo kuibua wasiwasi kwamba huenda watatumia nguvu kumlinda mgombea wao.

Kundi la Taliban tayari limeyatuma magari yatakayowabeba wafungwa wanaotarajiwa kuachiwa, na pia wako tayari kuheshimu makubaliano kwa kuwaachia maofisa karibu 1, 000 wa serikali waliyokuwa wanawashikilia.

Ofisa mwandamizi wa Taliban mjini Doha mji mkuu wa Qatar ambako majadiliano baina ya wanamgambo na maofisa wa Marekani yalifanyika, anayesema magari hayo yameelekea karibu na gereza la Bagram ili kuwabeba wafungwa watakaochiwa.

**DW**

# Wasomi duniani, Mangula walivyomuibua upya Nyerere



Wana CCM waliokusanyika katika mkutano wa Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Bara, Philipo Mangula (hayuko pichani), ili kusikiliza majumuisho ya ziara yake mkoani Singida hivi karibuni. **PICHA: JOHN MAPEPELE**

**INATOKA UK.15**

**KUTUNZA AMANI**

Mchango wa Mwalimu Nyerere katika kusuluhisha migogoro utabaki kuwa shule ya tosha ya demokrasia kwa dunia mzima, ambapo aliwataka Wanasingida kuishi kwa kuelewana na kudumisha amani aliyoijenga Mwalimu Nyerere.

Mangula anasema Watanzania wanapaswa kuelewa kwamba amani ikitoweka hata kile kidogo ambacho kila mmoja amekihangaikia na kukitolea jasho, kitatoweka kama "ndoto ya mchana".

"Haya ndiyo yanayojitokeza sehemu mbali mbali za dunia. Katika kipindi hiki tete, Watanzania wawe makini zaidi, kwa kujikita katika umoja na mshikamano wa kitaifa, uzalendo, nidhamu pamoja na kutetea haki za binadamu ili kujenga jamii inayoheshimu utu wa binadamu, heshima, haki msingi, amani na maridhiano.

**AREJEA ZBAR**

Akitolea mfano wa machafuko ya amani na kisiasa wakati wa uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000, kipindi cha mstaafu Benjamin Mkapa visiwani Zanzibar, Mangula anasema kazi ya maridhiano ilichukua zaidi ya miezi 10 ili kumaliza tofauti.

Ananukuu ripoti ya Global Peace Index (GPI) inayotolewa na taasisi ya uchumi na amani (IEP) yenye makao yake makuu mjini Sydney nchini Australia, ya mwaka 2019, ikionyesha kuwa Tanzania imeongoza Afrika Mashariki kwa kuwa nchi yenye amani Zaidi.

Anasema imeshika nafasi ya 54 kati ya nchi 163, zilizoorodheshwa kuwa na amani zaidi duniani.

> Watanzania wanapaswa kuelewa kwamba amani ikitoweka hata kile kidogo ambacho kila mmoja amekihangaikia na kukitolea jasho, kitatoweka kama "ndoto ya mchana."

Anawataka wananchi kutochezea amani na kuyumbishwa na wanasiasia badala yake waione amani walio nayo kama mtaji mkubwa wa kuwaletea maendeleo ya kweli kwa kizazi cha sasa na baadaye ambapo alisema kuwa watu wengi hawapendi kuona Tanzania ina amani na kupiga maendeleo ya haraka kama inavyofanya sasa.

"Ndugu zangu hata tukichukulia mfano mdogo tu, katika kipindi cha miaka 75 ambayo tulitawaliwa na Wajerumani na Waingereza kwenye wilaya yote ya Manyoni hatukuwa hata na shule mmoja ya iwe sekondari au msingi, lakini leo tuna zaidi ya shule 30 katika kipindi kifupi, je hayo siyo maendeleo makubwa ?" anahoji Mangula

Anasisitiza kuwa mapinduzi makubwa ya kiuchumi yanayofanywa na serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli, yanatokana na msingi imara uliojengwa ambao ni amani na kwamba wachafuzi wa kubwa wa amani dunani kote ni wanasiasa ambao wamekuwa wakisukumwa na tamaa ya madaraka. Hata hivyo, wanaoumia ni watoto, wazee na kina mama.

Vilevile akitolea mfano wa machafuko ya kisiasa ya Rwanda ya mwaka 1994 anasema akiwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera wakati huo, alishuhudia wimbi kubwa la watoto na kinamama wakiteseka na kufa njiani wakati wakijaribu kukimbia nchi yao kunusuru maisha yao.

"Nilishuhudia wanawake na watoto wamejitanda kanga na kumsaidia mama mwenzao kujifungua mtoto pembeni mwa barabara na baada ya kujifungua tu wakaendelea na safari, kwa kweli huwa sipendi kukumbuka hali ile maana ni hatari na uchungu usioelezeka" anaongeza Mangula.

**UADILIFU UCHAGUZI**

Akiwa katika mikutano anasisitiza suala la uadilifu na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za CCM na serikali zinazohusu masuala ya uongozi.

Anabainisha kuwa vitendo vyoyote vya rushwa na wagombea kuanza kujipitisha kabla ya kipindi rasmi cha kuchukua fomu za kugombea na kuanza mchakato wa uchaguzi wa mwaka huu hakikubaliki na kusisitiza kuwa chama kitachukua hatua kwa wote watakaobainika kufanya hivyo na kwamba chama kipo makini hakitamwonea aibu wala kumbeba mwanachama yoyote.

Aidha, anazitaka Kamati za Siasa kwenye maeneo husika zitakazoshindwa kuwachukulia hatua wanachama watakaofanya makosa kuadhibiwa.

Mzee Mangula anatamatisha ziara yake kwa kutembelea mradi wa shamba la pamoja la korosho lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 12,000 eneo la Masagati lililoko wilayani Manyoni na kusifu juhudi zinazofanywa na serikali katika kuleta mapinduzi makubwa ya kilimo kwa wananchi bila kujali itikadi ya vyama vyao.

Anasema alama ya Chama Cha Mapinduzi ni jembe na nyundo inayosimamia wakulima na nyundo kwa wafanyakazi hivyo CCM inaamini kuwa wakulima na wafanyakazi wanamchango mkubwa kkwenye uchumi wa nchi yao.

**MAELEZO YA RC**

Anapomkaribisha Mangula mkoani Singida, Mkuu wa Mkoa, Dk. Rehema Nchimbi anamwelezea kuwa shamba hilo lilianzishwa kwa kushirikisha wananchi wote bila kuzingatia itikadi za vyama vyao lengo likiwa ni kuwabadili mawazo na mtazamo na kutafuta maendeleo ya kweli kwa wananchi wote

"Kutokana na utafiti uliofanyika mwaka 2002, na Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Kilimo Naliendele na matokeo yanaonyesha kuwa hali ya hewa na udongo vinafaa kwa kilimo cha korosho hivyo tulianza kuwahamasisha wananchi kulima zao hilo" anaongeza Dk. Nchimbi

Katibu Tawala Mkoa wa Singida Dkt. Angelina Lutambi, anataja baadhi ya manufaa ya mradi huo kuwa ni pamoja na udhibiti wa visumbufu kama magonjwa na wadudu, utunzaji ubora wa korosho kutokana na usimamizi wa karibu, upatikanaji wa uhakika wa soko katika eneo la mradi, kuwapatia wakulima pembejeo na huduma za ugani kwa wakati.

Lengo la shamba hilo kuhudumia eneo kubwa la kilimo kwa wakati mmoja na kwamba linatarajiwa kuwa chanzo kikuu cha malighafi za viwanda vya kusindika korosho.

Lutambi anaeleza baadhi ya manufaa mengine ya mradi huo kuwa ni kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri ya Manyoni kupitia ushuru na kodi za biashara mbalimbali zitokanazo na ongezeko la uchumi katika sekta mtambuka zinazoendana na zao hilo.

Nyingine anasema ni hali ya maisha ya wananchi kuboreka ikiwa ni pamoja na ujenzi wa makazi bora, kuwapa watoto na wategemezi elimu na kuongeza uhakika wa chakula katika kaya bila kusahau huduma za afya.

# Pérez de Cuéllar Katibu Mkuu aliyeacha alama zisizofutika UN

**Na Mwandishi Wetu**

KIFO cha Katibu Mkuu wa Tano wa Umoja wa Mataifa, Javier Pérez de Cuéllar, kimetangazwa wiki iliyopita, dunia ikiarifiwa kuwa amefariki akiwa na umri wa miaka 100.

De Cuéllar raia wa Peru ambaye aliaga dunia Jumatano ya Machi 04, alikuwa kiongozi wa UN kwa miaka 10 au mihula miwili.

Kiongozi huyo alianza kuutumikia Umoja wa Mataifa kuanzia 1 Januari mwaka 1982 hadi 31 Desemba mwaka 1991.

Kufuatia taarifa za kifo chake, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, anatoa salamu za rambirambi, akieleza masikitiko yake makubwa kufuatia kifo cha de Cuéllar.

"Alikuwa mwanasiasa mzoefu, mwenye stadi na mwanadiplomasia aliyejizatiti na mtu ambaye aliacha alama kubwa kwenye Umoja wa Mataifa na duniani kote," anasema Guterres kwenye taarifa yake hiyo.

Anaendelea kusema kuwa maisha ya Pérez de Cuéllar, yamekuwa ya siyo tu karne moja bali pia historia nzima ya Umoja wa Mataifa kuanzia ushiriki wake katika mkutano wa kwanza wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1946.



Katibu Mkuu Javier Perez de Cuella, akiwa nchini Namibia kulitembelea kundi la mpito la msaada wa jeshi la kulinda amani (UNTAG) lililofanyakazi Namibia na Angola. De Cuella alikuwa kwenye makao makuu ya jeshi hilo nchini Namibia mwaka 1989. **PICHA: MTANDAO UN**

**VITA BARIDI**

Akimuelezea Guterres anasema kipindi chake cha uongozi akiwa Katibu Mkuu kiliendana na zama mbili muhimu ambazo ni baadhi ya miaka migumu ya vita baridi na hatimaye mzozano wa kiitikadi , kipindi ambacho Umoja wa Mataifa ulianza kutekeleza kwa dhati dhima iliyobuniwa na waasisi wa chombo hicho."

**MIZOZO ALIYOKABILI**

Pérez de Cuéllar alikuwa na dhima maalumu katika maeneo muhimu yaliyokuwa ni mafanikio kidiplomasia ikiwemo uhuru wa Namibia, kumalizika kwa vita kati ya Iraq na Iran, kuachiliwa huru kwa mateka wa Kimarekani waliokuwa wakishikiliwa nchini Lebanon, mkataba wa amani nchini Cambodia na katika siku zake za mwisho kabisa ofisini mkataba wa amani wa kihistoria nchini El Salvador.

Katibu Mkuu, licha ya kutuma salamu zake za rambirambi kwa familia ya Pérez de Cuéllar, aliwafariji pia wananchi wa Peru na watu wengine wengi duniani kote ambao maisha yao yaliguswa na kiongozi huyo wa kimataifa ambaye ameaga dunia na kuiacha pahala bora zaidi.


**KUONGOZA UN**

Safari hadi kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, De Cuéllar ambaye kitaaluma alikuwa mwanasheria, tangu mwaka 1940 katika maisha yake alishika nyadhifa mbalimbali za kidiplomasia kuanzia kwenye Wizara ya Mambo ya Nje na kwenye Umoja wa Mataifa.

De Cuéllar aliwahi kuwa Balozi wa Peru nchini Uswisi, kwenye Muungano wa Kisovieti, Poland na Venezuela.

Kama miongoni mwa wajumbe wa Peru alishiriki kikao cha kwanza cha Baraza Kuu mwaka 1946. Na akawa Mwakilishi wa Kudumu wa Peru kwenye Umoja wa Mataifa mwaka 1971 na kuanzia hapo hakuondoka kwenye Umoja wa Mataifa.

> Umoja wa Mataifa ulikuwa ukienda sanjari na mabadiliko ya haraka ya kihistoria katika miaka ya karibuni na ulipata mafanikio makubwa katika ulinzi wa amani.



Mwaka 1975 De Cuéllar aliteuliwa kuwa Mwakilishi wa Katibu Mkuu nchini Cyprus na kushika nyadhifa nyingine mbalimbali mpaka Desemba 1977 na miaka miwili baadaye alichukua wadhifa wa msaidizi maalum wa Katibu Mkuu kwenye masuala ya kisiasa.

Na kuanzia Aprili mwaka 1981 alihudumu kama mwakilishi wa Katibu Mkuu katika kutatua mgogoro wa Afghanistan na hata aliporejea kufanyakazi kwenye Wizara ya Mambo ya Nje ya Peru, Pérez de Cuéllar aliendelea kumwakilisha Katibu Mkuu katika masuala ya Afghanistan.

Baada ya kuchukua madaraka rasmi kama Katibu Mkuu wa tano wa Umoja wa Mataifa, Januari 1, 1982, miezi michache baadaye katika ripoti yake ya kwanza kuhusu kazi za shirika hilo, kiongozi huyo alitoa tathimini iliyokosoa vikali , kwa mujibu wake wakati huo Baraza la Usalama.

Alisema:"Haliwezi kuchukua maamuzi ya hatua za lazima kutatua migogoro ya kimataifa. Na hata maamuzi hayo yanapofanyika matarajio ya utekelezaji wake katika mazingira ya mgawanyiko kwenye jumuiya ya kimataifa ni sifuri."

Kipaumbele chake kilikuwa kuubadilisha Umoja wa Mataifa kuwa shirika linaloweza kutimiza majukumu yake ya kuhakikisha amani na usalama.

Alisema "endapo hili halitofanyika jumuiya ya kimataifa itakuwa kazi bure katika masuala ya migogoro ya kijeshi ambayo inatishia msingi wa amani ya kimataifa."

Akiondoka madarakani mwaka 1991 de Cuéllar alitoa ripoti yake ya mwisho ambayo ilikuwa tofauti na ya kwanza safari hii aliandika kuhusu kufufua Umoja wa Mataifa, kumaliza mkwamo wa muda mrefu.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu ... "Umoja wa Mataifa ulikuwa ukienda sanjari na mabadiliko ya haraka ya kihistoria katika miaka ya karibuni na ulipata mafanikio makubwa katika ulinzi wa mani."

Licha ya kukosolewa hapa na pale mkuu huyo wa Umoja wa Mataifa alisema "hakuna mtu anayeweza kuongeza mara mbili utendaji wa Umoja wa Mataifa.

Alisema Umoja wa Mataifa unaingia katika zama mpya na unachukua majukumu ambayo hayakuwepo kwenye mipango ya awali ya kuanzishwa kwa umoja huu."

**HABARI ZA UN**

# William Ruto anapokandamizwa na utata wa kifo cha mlinzi wake



Mkuu wa Mashtaka nchini Kenya, George Kinoti. **PICHA: BB**

**Na Mwandishi Wetu**

UTATA umeibuka kuhusu mazingira ya kifo cha mlinzi wa Makamu wa Rais wa Kenya, Dk. William, Ruto, ambaye alikutwa ameuawa nyumbani kwake, mwezi uliopita.

Mlinzi huyo Sajenti Kipyegon Kenei, ambaye alikuwa mkuu wa usalama katika ofisi ya Ruto, kabla ya kufikwa na umauti, alitangazwa kuwa ametoweka kwa siku kadhaa katika mazingira ya kutatanisha.

Sajenti Kenei, anatajwa kuwa alikuwa shahidi muhimu katika kesi ya utapeli ya dola milioni 395 ambayo unamuhusisha rafiki wa karibu wa Makamu wa Rais Rasheed Echesa.

Aidha, ofisi ya Ruto inatuhumiwa ndiko kulifanyika kwa kikao cha kusuka mpango huo ambao ni wa manunuzi ya silaha kutoka kwa wafanyabiashara wa Poland.

Katika kauli ya hivi karibuni ya Mkuu wa Mashtaka nchini Kenya, George Kinoti, amedai kuawa kwa Kenei, kunahusiana na matukio katika ofisi ya kiongozi huyo.

Anasema Sajenti Kenei aliuawa kikatili, kinyume na taarifa za awali kwamba alijiua mwenyewe.

Wakati wa mazishi ya polisi huyo, Makamu wa Rais Ruto, alijaribu kupinga dhana kwamba aliuawa kutokana na kufuta ushahidi wa ofisi yake kuhusika na kashfa hiyo, badala yake alilaumu idara hiyo kwamba inatumika kisiasa.

Anasema anaamini kuwa kifo hicho kitatumika kumkandamiza na kumuondoa katika kinyang'anyiro cha urais wa mwaka 2022.

> Ofisi yangu haina uhusiano na Idara ya ulinzi DOD, hatununui bunduki katika ofisi yangu, hii ni njama ya kunikandamiza, hakuna anayewalenga wahusika kila kitu kidole kimeelekezwa katika ofisi yangu.

Anawataka watu kuacha kutoa dhana mbaya dhidi yake, kwani sura ya marehemu Sajenti Kenei, inajua wabaya wake, na kama angekuwa hai angesema ukweli.

**KIFO CHA I KINEI**

Mwili wa Sajenti Kenei ulipatikana nyumbani kwake ukiwa na majeraha ya risasi na haikufahamika ulifikaje hapo ikiwa siku kadhaa alitoweka.

Awali polisi ilitangaza kwamba kachjero huyo alijiua mwenyewe, jambo ambalo liliibua mjadala mkali katika mitandao ya kijamii.

Kifo cha askari huyo kilitokea wakati ambapo alitakiwa polisi kuandika maelezo yake kuhusu sakata ya zabuni hewa ya ununuzi wa silaha za mamilioni ya pesa walipotembelea ofisi ya Ruto mjini Nairobi.

Baadhi ya watu wanasema huenda mlinzi huyo aliuawa sehemu tofauti na nyumbani kwake, na baada ya mauaji hayo mwili wake ulipelekwa nyumbani kwake kwa lengo la kuficha ukweli na kupoteza ushahidi.

Kabla ya tangazo la kifo chake, ofisi ya Ruto ilitoa taarifa ikisema kwamba mlinzi huyo alitoweka.

Mkurugrnzi wa Mashtaka Kinoti anasema Sajenti Kenei , alitakiwa kuandikisha taarifa polisi kueleza jinsi aliyekuwa Waziri wa Michezo, Rashid Echesa na washukiwa wengine wanne walivyopanga zabuni ya kitapeli katika ofisi ya Ruto.

Wakiwa ofisini hapo walitiliana saini kandarasi feki ya kuuzia Wizara ya Ulinzi silaha, ambazo zingenunuliwa.

Kinoti alionyesha wanahabari picha zilizochukuliwa na camera za siri za CCTV, akionekana Sajenti Kenei akiwafungulia mlango na kuwaelekeza Echesa na ujumbe wake katika ofisi ya Ruto.

Echesa, rafiki wa karibu wa mwandani wa karibu wa Dk. Ruto, ameshtakiwa kwa kujaribu kujipatia dola za Marekani 395, 442,000 kutoka kwa wafanyabiashara wa Poland kwa kuwaahidi zabuni ya kuiuzia Idara ya Ulinzi ya Kenya vifaa vya kijeshi.

Baada ya kuibuka sakata hilo, makamu huyo wa rais aliwashutumu wabaya wake wa kisiasa kwa kumuingiza katika kasha huku akikiri kuwapokea wageni hao.

Anasema ripoti hizo ni kama porojo zenye hila na kwamba haziwezi kumuondoa katika mbio zake za kuelekea Ikulu.

Alipinga kukutana na waziri huyo wa zamani wa michezo pamoja na wafanyabiashara wake waliotembelea ofisi yake na kwamba hakuhusika katika mkataba huo bandia.

Ingawa inaonekana kifo cha aliyekuwa mkuu wa usalama katika ofisi ya Naibu Rais wa Kenya kinachukuwa mkondo wa kisiasa, wengi wanafuatilia sakata hilo wapo makini kujua ukweli ni nani yupo nyuma ya mauaji hayo.

**RUTO AJITETEA**

Dk. Ruto ameshutumiwa sana kufuatia kesi hiyo, huku viongozi wengine wakihoji vipi ulaghai wa hali ya juu unaweza kufanyika katika Ofisi yake bila yeye kujua.

Kwa upande mwingine, Naibu huyo wa Rais Ruto ameishutumu ripoti hizo kama porojo zenye hila.

Ruto amejitetea vikali kwamba hakukutana na waziri huyo wa zamani wa michezo pamoja na wafanyabiashara wake waliotembelea ofisi yake na hakuhusika katika mkataba huo bandia uliodaiwa kugharimu dola milioni 397.

Ingawa inaonekana kifo cha aliyekuwa mkuu wa usalama katika ofisi ya Naibu Rais wa Kenya kinachukuwa mkondo wa kisiasa, wengi wanafuatilia sakata hiyo kwa umakini mkubwa wakitarajia kwamba ukweli utapatikana.

Watu wengi wanafuatilia mwenendo mzima wa mauaji hayo kwa sababu alitakiwa kuandika taarifa ya maelezo kwa polisi kuhusu washukiwa wa sakata ya zabuni hewa ya ununuzi wa silaha za mamilioni ya pesa walipotembelea ofisi ya Ruto mjini Nairobi.

Aidha, kuonekana kwake kwenye kamera xa CCTV akifungua mlango nako kunaongeza hofu kuwa huenda aliuawa ili kuficha siri hiyo.

**RUTO AWAKA**

Ruto amelalamikia Idara ya Jinai kuwa inatumika kukabiliana naye kisiasa.

Akizungumza wakati wa ibada ya mazishi ya marehemu Kenei, Ruto alimtaka Mkurugenzi Kinei, kuacha kuingilia mambo ya kisiasa na badala yake abaki kufanya kazi ya polisi.

"Nataka kumwambia Mkurugenzi wa Idara ya Jinai DCI aachane na siasa, aangazie kazi ya polisi na kupata chanzo cha nani aliyemuua Kenei", anasema.

Anasema binafsi yuko tayari kukabiliana na wale wanaopanga njama ya kumuangusha kisiasa.

Akikwepa kuzungumzia kashfa hiyo ya mabilioni alielekeza lawama ofisi ya DCI.

"Ofisi yangu haina uhusiano na Idara ya ulinzi DOD, hatununui bunduki katika ofisi yangu, hii ni njama ya kunikandamiza , hakuna anayewalenga wahusika kila kitu kidole kimeelekezwa katika ofisi yangu," anaongeza.

Anaahidi hatopumzika hadi wauawaji wa Kenei watakapokamatwa na kufunguliwa mashtaka.

''Wale waliomuua Kenei hawatakuwa na amani , tutawasaka na wale walio na njama dhidi yangu, pengine mniue lakini sitatishika", anasisitiza.

Siku tatu kabla ya Kenei kuawa ofisa huyo , aliwaita walinzi wote kutaka ufafanuzi kuhusu wageni waliofika katika ofisi yake na kisha kupanga mpango huo.

"Jumatatu hiyo wakati nilipofika ofisini, nikamuita anayesimamia ulinzi katika ofisi ya majengo ya Naibu Rais, Joseph Rop, ambaye ni Kamishna wa Police, anayesimamia msafara, William Yampoi, wote wawili walikuja nikawauliza ni jambo gani lilitendeka Alhamisi iliyopita?," anasema.

"Hawa wawili wakaniambia ilitokea hivi, mpaka wakaniletea CCTV. Mimi nikamuita Kenei na wenzake wawili ambaye wanafanya kazi pamoja. Wakasimama mbele yangu na kuniambia ukweli wao," Ruto anaongeza. **BBC**



## Wazazi watupiwa lawama kikwazo elimu mtoto wa kike

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAZAZI na walezi wamenyooshewa kidole kukwamisha jitihada za mabinti katika kutimiza ndoto zao kwa kutowapatia elimu ya mahusiano.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi wa Shirika la Youth Education Through Sports Tanzania (YES -TZ), Keneth Simbaya, wakati wa sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambapo shirika hilo liliwakutanisha wanafunzi wa shule za sekondari, mabinti waliokabiliana na vikwazo mbalimbali na walimu kwa lengo la kutafakari siku hiyo muhimu.

Simbaya alisema elimu ya mahusiano kwa watoto wa kike haijawafikia mabinti wengi, ndio maana walio wengi wanakubali kurubuniwa na wanaume na kukatisha ndoto zao.

Alisema miongoni mwa masuala ambayo yanapaswa kutiliwa mkazo kwa sasa ni kutoa elimu ya mahusiano kwa mabinti kuanzia nyumbani hadi shuleni ili kuepukana na vishawishi.

"Elimu ya mahusiano inamjenga mtoto wa kike kukabiliana na vishawishi vyovyote kutoka kwa mwanaume pindi anapokuwa kwenye masomo au kwenye shughuli nyingine, tunapotafakari sikukuu ya mwanamke tubebe ajenga ya kuwafunda mabinti zetu," alisema Simbaya.

Aidha, Simbaya alisema moja ya mikakati ya Shirika la (YES TZ) ni kuhakikisha watoto hususani mabinti wanatimiza ndoto zao kwa kuhakikisha wanakuwa na afya njema, wanapata elimu ya demokrasia na utawala bora sambamba na kujifunza ujasiriamali.

Mmoja wa walimu walioshiriki kilele cha sikukuu hiyo, Silos Mwaswale kutoka Shule ya Sekondari Ilomba, aliwashauri wazazi kutowapendelea watoto wa kiume katika mahitaji badala yake waweke usawa.

Alisema baadhi ya wazazi wamekuwa na utamaduni wa kuwasikiliza zaidi wavulana kwenye masuala mbalimbali kuliko binti, ambaye kimsingi ana uhitaji mkubwa.

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Ilomba, Christina Greyson, alisema miongoni mwa vikwazo wanavyokabiliana navyo wazazi kutopawatia mahitaji muhimu ikiwamo nguo za ndani.

# Mila potofu, ushirikina chanzo ukatili Kyela

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

MILA potofu na imani za kishirikiana wilayani Kyela, vimetajwa kuwa chanzo cha matukio mengi ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wenye umri wa chini ya miaka 14 ambayo yanaathiri maendeleo ya makundi hayo.

Akizungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo yamefanyika kiwilaya katika Kata ya Nkuyu wilayani hapa, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Cloudia Kitta, alisema takwimu alizonazo kuhusu matukio ya ukatili wa kijinsia unaosababishwa na imani za kishirikina wilayani humo zinatisha.

Ingawa hakutaja kiwango cha takwimu hizo, lakini alisema taarifa anazozipata kutoka Jeshi la Polisi na Idara ya Maendeleo ya Jamii wilayani Kyela kuhusu matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto zinaonyesha vitendo hivyo vimekithiri, na kwamba hali hayo haiwezi kuvumiliwa na serikali.

"Ninazo takwimu ofisini kwangu ambazo zinatokana na taarifa ninazopewa na Polisi na Idara ya Maendeleo ya Jamii, zinaonyesha kuwa ukatili wa kijinsia unaosababishwa na imani za kishirikina na mila potofu uko juu sana, sasa serikali tumeamua kuchukua hatua kali kudhibiti hali hiyo," alisema Kitta.

Alisema ukatili huo umezidi katika matukio ya ubakaji wa watoto wenye umri mdogo, wanawake kunyimwa haki ya kumiliki mali ikiwamo ardhi pamoja na vipigo kwa wanawake kutoka kwa waume zao.

Kitta alisema kuwa matukio kama ya ubakaji wa watoto wadogo yanatokana na imani za kishirikina ambapo baadhi ya watu wanadhani kwa kufanya kitendo hicho wanaweza kupata utajiri au kuondoa mikosi.

"Haiwezekani mtu mzima aamue kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka saba... kwa vyovyote hapo kuna imani za kishirikina, na ndio sababu tumeamua sisi kama serikali kupambana na hizo imani pamoja na mila potofu kwa nguvu zetu zote," alisema Kitta.

Katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia wilayani Kyela, Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAid) limeamua kufadhili mradi ujulikanao kama Feed the Future, advancing Youth Tanzania wenye lengo la kuwafanya vijana hasa wa kike wajitambue na kuepuka ukatili wa aina hiyo.

Mkufunzi wa Mradi huo Feed the Future, Masha Sanga, alisema kuwa lengo ni kuwezesha vijana kupata maarifa katika uongozi, ujasiriamali na namna ya kutunza afya ili waweze kujitegemea na kushiriki katika vyombo vya kutoa maamuzi kwenye jamii.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imesema nayo imeamua kuingilia kati kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia hususan rushwa ya ngono ambayo nayo inadaiwa kuanza kushika kasi wilayani Kyela.

Ofisa wa Takukuru Wilaya ya Kyela, Baraka Mungure, alisema wameamua kuanza kutoa elimu kwa wanafunzi ili wazijue haki zao pamoja na kutambua wapi watoe taarifa wanapofanyiwa ukatili wa kijinsia.



Ofisa Msimamizi wa Kodi Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Julius Mjenga, akitoa elimu kwa wafanyabiashara wa mji wa Tunduma mkoani Songwe jana, kuhusu madhara ya kufanya biashara za magendo mipakani wakati wa kampeni ya elimu ya mkoa kwa mkoa inayoendelea katika mikoa ya Songwe na Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake waonywa mikopo watu binafsi

**Na Nebart Msokwa, MBARALI**

MKUU wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, amewataka wanawake kuacha kuchukua mikopo kwa watu binafsi, wanaowatoza riba kubwa kwa maelezo kuwa vitendo hivyo ni aina mpya ya ukatili wa kiuchumi.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo kiwilaya yalifanyika katika Kata ya Igurusi, na kusema mikopo hiyo inawasababishia mateso makubwa wanawake wakati wa kulipa.

Alisema wanatumia nguvu nyingi wakati wa uzalishaji, lakini wakati wa mavuno pesa zote zinaelekezwa kwenye kulipa madeni kwa watu ambao wanawakopesha kwa riba kubwa, hivyo wanajikuta hawaendelei kiuchumi.

Mfune aliwashauri wananchi wote wanaohitaji kukopa fedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao za kiuchumi ikiwamo kilimo kwenda kwenye taasisi za fedha ambazo ni rasmi kwa kazi hiyo na zinatoa mikopo kwa riba nafuu.

"Mnazalisha sana, lakini mikopo mnayochukuwa kwa watu binafsi inawafilisi unajikuta wakopeshaji wananeemeka, lakini nyie mnaendelea kuwa maskini, sasa nawashauri muache tabia hiyo badala yake chukueni mikopo kwenye benki," alisema Mfune.

Alisema serikali itaendelea kukabiliana na wahuni hao ambao wanatajirika kupitia migongo ya watu kwa maelezo kuwa biashara wanayofanya ni haramu na haistahili kuendelea kufanyika.

Aidha, aliwatahadharisha wanaume ambao wanaendeleza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Akisoma risara ya wanawake wa Wilaya ya Mbarali, Stella Admin, alisema ili wanawake wajikwamuwe kiuchumi, wanatakiwa kupigania haki ya usawa kati yao na wanaume kwenye shughuli mbalimbali kuanzia ngazi ya kaya mpaka Taifa.

Alisema moja ya haki ambayo wanawake wanatakiwa kuipigania ni kushiriki kwenye vikao vya maamuzi kuanzia ngazi ya vijiji hadi taifa ili mawazo yao yatambuliwe hasa kwenye shughuli za maendeleo.

Vilevile aliomba serikali kuweka msisitizo wa usawa kwenye sekta ya elimu, ajira na shughuli za kiuchumi kwa maelezo kuwa kuna baadhi ya tamaduni zinawabagua wanawake kwenye maeneo hayo.

"Tunapaswa kushirikishwa kwenye mipango ya maendeleo ili na sisi tutoe mawazo yetu ambayo yatasaidia kwenye shughuli hizo... sasa ni wajibu wetu wanawake kuungana kupigania haki hii badala ya kulalamika," alisema Stella.

Aliwataka mabinti wadogo kufanya kazi kwa kujiamini kwa maelezo kuwa kwa sasa kuna wanawake wanaofanya kazi serikalini, ambao ndio dira yao akiwamo Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan.

Diwani wa Igurusi, Hawa Kiwele, alisema moja ya matatizo yanayowakabili wanawake wa kata yake ni ukosefu wa huduma za afya karibu na makazi yao hali inayowalazimu kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta huduma hiyo.

Aliiomba serikali iwaboreshee Kituo cha Afya kilichopo kwenye kata hiyo ili waondokane na tatizo hilo, ambalo alisema wakati mwingine limekuwa likighirimu maisha ya kinamama na watoto.





## Ruwasa kufanya utafiti kwa h'shauri zinazofanya vibaya

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa), imejipanga kufanya utafiti ili kubaini sababu za baadhi ya halmashauri kufanya vibaya kwenye miradi ya maji.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Ruwasa, Mhandisi Clement Kivegalo, katika mkutano wa mrejesho wa uhakiki na tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Malipo kwa Matokeo (PBR) awamu ya nne, uliofanyika jijini hapa.

Aliagiza wakala huo kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID) kufanya utafiti huo na kuchukua hatua stahiki.

Alisema katika kigezo cha vituo vya kuchotea maji vinavyofanya kazi Halmashauri ya Tandahimba DC, Chunya DC, Newala DC na Kondoa DC zimefanya vibaya kwa awamu ya tatu na nne.

"Zilizofanya vizuri ni Halmashauri ya Bariadi, Bumbuli na Mlele," alisema.

Aidha, alisema kwa kigezo cha usahihi wa takwimu zilizowasilishwa Halmashauri zilizofanya vibaya ni pamoja na Kondoa TC, Songwe DC, Newala TC, Uvinza DC na Ubungo MC huku zilizofanya vizuri ni pamoja na Halmashauri ya Rorya, Buchosa na Sengerema.

Kuhusu kigezo cha kiutendaji, alisema Halmashauri zilizofanya vibaya ni Chunya DC, Ubungo MC na Momba DC.

Kwa upande wa mikoa, alisema Mkoa wa Mtwara, Dar es Salaam na Songwe umefanya vibaya kwenye utendaji huku mikoa ya Njombe, Simiyu na Kilimanjaro iking'aa kwenye utendaji.

Awali, alifafanua kuwa utekelezaji wa mpango unakwenda kwa mtindo wa motisha ambapo halmashauri inayofanya vizuri kwa maana ya kukidhi vigezo vilivyowekwa ndiyo inayopata fedha nyingi zaidi ikilinganishwa na halmashauri isiyofanya vizuri kwa vigezo hivyo hivyo.

"Kiwango cha malipo ya motisha au bonasi kinategemeana na jinsi halmashauri inavyokidhi hivyo vigezo baada ya uhakiki na tathmini inayofanywa na timu ya wataalamu wa kujitegemea," alisema.

Alitaja vigezo vikuu vinne vinavyozingatiwa katika kupata bonasi au motisha ni uwepo wa vituo vinavyofanya kazi na kutoa huduma ya maji safi na salama.

"Uwasilishaji wa takwimu na taarifa za huduma ya maji kila mwezi, usahihi wa takwimu na taarifa za huduma ya maji kila mwezi, usahihi wa takwimu na taarifa zilizowasilishwa na uthibitisho wa uwepo wa mpango wa kuboresha huduma za maji," alisema.

Alibainisha kuwa mpango huo umetengewa Sh. bilioni 194.5 na matumizi yake yatafikia ukomo ifikapo Machi 2022 na hadi sasa Sh. bilioni 107.3 zimetumika kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 2016 hadi Juni 2019.

"Zingine zitatumika mwaka 2020 sawa na asilimia 55 ya fedha zote za mpango huu na zimekuwa zikitolewa kwa kila awamu," alisema.

Alieleza kuwa awamu ya kwanza halmashauri 57 zilikidhi vigezo na kupata Sh. bilioni 2.53, awamu ya pili ilikuwa mwaka 2017/18, ambapo halmashauri 72 zilifuzu na kupata Sh. bilioni 11.23.

# Wamiliki wa 'Day Care' waonywa

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

KAMISHNA Msaidizi wa Ustawi wa Jamii wa Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaisha Moyo, amewaonya wamiliki wa vituo vya kulelea watoto mchana nchini (Day Care), wanaoendesha shughuli zao bila kujisajili kisheria.

Moyo aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifunga mafunzo ya wiki mbili kwa walimu walezi wa watoto katika shule pamoja na vituo hivyo mkoani Dodoma yaliyoandaliwa na Chuo cha Utaratibu Vocation Training College.

Alisema kumekuwapo na tabia ya baadhi ya watu kuanzisha vituo hivyo kiholela na kutozingatia sheria na taratibu zilizowekwa na wizara hiyo.

"Sheria yetu inamtaka kila mtu kuendesha hivi vituo akiwa tayari amesajiliwa na kupatiwa cheti ambacho kitamtambulisha siyo kuanzisha vituo kiholela bila kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria," alisema Moyo.

Alisema uwepo wa vituo hivyo ambavyo havijasalijiwa wala kufuata taratibu kutasababisha watoto kutolelewa kwenye malezi stahiki.

Alisema ni lazima kila kituo kinachoanzishwa kukaguliwa kwanza kabla hakijaanza kutoa huduma ili wataalamu wajiridhishe kama kina uwezo wa kutoa malezi ambayo yatawajenga watoto katika misingi bora.

"Kama leo hii tukaachia watu wakaanzisha vituo hivi vya watoto kiholela na wakawajenga katika misingi isiyo bora tunaweza kuwa na taifa ambalo ni hatari," alisema.

Hata hivyo, alisema kutosajiliwa na kutambuliwa na serikali kutasababisha vituo kuwa chanzo kikubwa cha ukatili kwa watoto.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu wa mafunzo hayo, Richard Simba, alisema kuwa wanakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo waajiri wengi kutofuata kanuni na miongozo ya wizara husika katika utendaji wa kazi za kila siku.

"Tatizo jingine ni waajiri kutotupatia mikataba ya ajira kwa mujibu wa sheria, kutokuwa na vituo vya mfano vya Day Care vya serikali, kutokuwa na kituo cha mafunzo kazini kwa walezi wa watoto wadogo mchana," alisema.

Naye Mratibu wa mafunzo hayo, Elias Ntilambigwa, alisema jumla ya walimu walezi wa watoto 101, wamepatiwa mafunzo ya namna ya kuendesha vituo hivyo na uwezo wa kutengeneza zana za kujifunzia na kufundishia.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la kusaidia watu wa makundi maalum la GFF, Aisha Msantu (mwenye miwani) na Mwenyekiti wa Bodi wa shirika hilo, Rehema Hamisi (kulia), wakikabidhi sehemu ya msaada wa vitu mbalimbali kwa watoto wa kituo cha kulelea watoto yatima na wale wa mazingira magumu cha nyumba ya matumaini Miyuji, jijini Dodoma jana. Wa pili kulia, ni mlezi wa kituo hicho, Sista Adelida Venanci. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Watakiwa kuacha kuwatenga wenye mahitaji maalum

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

JAMII imetakiwa kuacha tabia ya kuwatenga watu wenye mahitaji maalum ili wafikie malengo yao ya kielimu na kiuchumi.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali la GFF, Aisha Msantu, linalojihusisha na kusaidia watu wenye mahitaji maalum katika sekta ya afya, elimu, mazingira, ujasiriamali pamoja na kiuchumi alipokuwa akitoa msaada kwa watoto yatima wa nyumba ya matumaini Miyuji, jijini hapa.

Alisema jamii inapaswa kuacha vitendo vya kuwatenga watu wenye mahitaji maalum bali wawasaidie ili kufikia ndoto zao.

"Jamii haipaswi kuwakwepa watu wa mahitaji maalum bali wawasaidie na kuwapa msaada wa kufikia mafanikio yao na siyo kuwa tenga na kuwanyanyapaa," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya GFF, Rehema Hamisi, aliwataka watoto hao kusoma kwa bidii kwa kuwa elimu ndiyo urithi pekee utakaowasaidia kwenye maisha yao.


Kuhusu msaada huo, Mkurugenzi huyo alisema hautakuwa mwisho bali wataendelea kusaidia kituo hicho ili kutatua kero zinazowakabili.

Naye mlezi wa kituo hicho cha nyumba ya matumaini, Sister Adelida Venanci, alisema hivi sasa kuna watoto 69, wanaowalea na wanakabiliwa na ukosefu wa fedha.

Alisema kituo hicho kinapokea watoto kutoka Mkoa wa Singida na Dodoma pia hakina vitanda vya kutosha kwa ajili ya watoto.

"Shida nyingine ni umeme hapa tunatumia Luku na kutokana na kutokuwa na fedha imekuwa ni hatari sana kwa kuwa wakati mwigine hatuwezi kununua, pia tuna tumia kuni kupika na kupata ni kazi sana kwa kuwa lazima uwe na kibali na lori moja la kuni ni Sh. 400,000," alisema.

Alisema ili kukabiliana na hali hiyo wameamua kufanya shughuli za kilimo na ufugaji ili kupunguza gharama za chakula pamoja na mahitaji mengine.



# SMZ kuongeza kiwango cha ufaulu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Zanzibar, imesema itaendelea kuimarisha mazingira mazuri katika sekta ya elimu ili kuongeza kiwango cha ufaulu na kuleta mabadiliko ya elimu nchini.

Akifungua mkutano wa tatu wa kutathmini maendeleo na changamoto za sekta ya elimu Zanzibar, Waziri wa Kilimo, Maliasili Mifumo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, alisema, mabadiliko hayo yatafanikiwa iwapo ushiriki wa wazazi utakuwa mzuri katika kulipa umuhimu suala la elimu kwa watoto wao ili kuleta matokeo chanya katika sekta hiyo.

Aidha, alisema maendeleo bora ya elimu ni mafanikio ya taifa, hivyo kuna umuhimu kwa wazazi kuongeza ushiriki wao ili kufikia lengo la mabadiliko ya elimu Zanzibar.

"Mbali na jitihada zinazochukuliwa na serikali yetu katika sekta hii, lakini ipo haja kuhakikisha wazazi wanaipa elimu umuhimu wa pekee katika maendeleo ya watoto wao," alisema.

Waziri Mmanga alieleza kuwa Serikali ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Ali Mohamed Shein kuweka mwongozo mzuri wa kuimarisha elimu umeleta mafanikio makubwa ikiwamo kuongezeka kwa uandikishaji wapya wa wanafunzi na ufaulu mzuri.

Alisema jumla ya watoto 85,974 wameandikishwa katika ngazi ya elimu ya maandalizi mwaka 2019 sawa na asilimia 81.4, ambalo ni ongezeko la asilimia 12 ukilinganisha na uandikishaji wa mwaka 2018.

Alieleza kuwa kwa upande wa elimu ngazi ya msingi, uandikishaji umeongezeka kutoka wanafunzi 276,858 mwaka 2018 na kufikia wanafunzi 290,510 mwaka 2019 .

Hata hivyo, alisema kwa elimu ya sekondari jumla ya wanafunzi 130,711 waliingia sekondari mwaka 2019 ukilinganisha na wanafunzi 122,323 walioandikishwa mwaka 2018.

Aidha, alisema matokeo ya mitihani yameimarika na wanafunzi waliofanya mitihani ya kidato cha nne imeongezeka na kufikia 1,808 mwaka 2019 ukilinganisha na wanafunzi 1,070 waliofaulu mwaka 2018.

Waziri huyo aliwataka washiriki wa mkutano huo kuhakikisha wanaendesha mijadala ya wazi ambayo itakuwa chachu ya kuimarisha maendeleo ya elimu Zanzibar kwa kutumia utafiti mbalimbali uliofanywa ili kupata suluhisho ya changamoto zinazokwamisha sekta hiyo.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Radhia Rashid Haroub, alisema licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya elimu, lakini bado kuna changamoto mbalimbali ikiwamo uchakavu wa majengo ya shule yaliyojengwa kwa miaka mingi.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Jumuiya za elimu zisizo za serikali, Khamis Abdallah Said, aliishukuru serikali kwa kutambua mchango wa taasisi binafsi katika elimu na kuomba kushirikiana katika kutatua vikwazo vinavyoikabili sekta hiyo ukiwamo uhaba wa vifaa vya kufundishia pamoja na uwelewa mdogo wa lugha ya Kiingereza kwa walimu.

Mkutano huo wa siku tatu umewashirikisha wadau wa elimu wakiwamo washirika wa maendeleo, wakurugenzi wa idara mbalimbali za serikali, wawakilishi wa asasi za kiraia, maofisa elimu wilaya na mikoa, kamati za shule, wazazi, walimu na wanafunzi ambapo kaulimbiu ya mkutano huo ilikuwa "ushiriki wa jamii katika upatinaji wa matokeo chanya ya elimu ya mtoto".



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, wakati alipofika kujitambulisha na kufanya mazungumzo, Ikulu Zanzibar, jana. **PICHA: WMNN**

# Upepo wasitisha safari za boti kwa muda

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KUTOKANA na upepo na mvua kubwa zilizoanza kunyesha alfajiri ya kuamkia jana, Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) imesitisha usafiri wa boti kwa muda hadi upepo ulipopungua.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Abdallah Kombo, alisema kuwa jana hakukuwa na usafiri wa boti wa saa moja asubuhi kama ilivyozoeleka siku zote boti za abiria huanza safari zake hutoka Zanzibar na kuelekea Dar es Salaam saa moja asubuhi.

Alieleza kuwa kutokana na upepo huo mkali walisitisha safari hiyo kwa muda ili kuokoa maisha ya wananchi na mali zao waliokuwa wasafiri wa boti ya Azam na Zanzibar One, ambazo huondoka saa moja asubuhi.

Alisema baada ya upepo kupungua na kujiridhisha, waliziruhusu kuondoka saa mbili asubuhi na kuelekea Dar es Salaam ili wasafiri waende kufanya shughuli zao.

"Tunaomba watuwie radhi wasafiri waliopanga kuondoka saa moja asubuhi leo (jana) pamoja na wamiliki wa boti… tumefanya hivyo kwa usalama wao kwa sababu upepo ulimkuwa mkali ulioambatana na mvua kubwa na ngurumo za radi," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi hasa wavuvi kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua na upepo, na kuwa na utamaduni wa kusikiliza taarifa zinazotolewa na mamlaka ya hali ya hewa ili kuepukana na maafa ambayo yanaweza kuepukika.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Maafa Zanzibar, Makame Khatib Makame, alisema kuwa hawajapata taarifa kamili kuhusiana na maafa kutokana na mvua na upepo mkali ulioanza juzi usiku.

"Zipo athari ndogondogo zilizotokea kutokana na upepo kama miti kukatika, lakini bado hatujapokea taarifa za maafa ya kifo au maji kujaa maji kutokana na mvua na upepo mkali… hivi sasa ndio tunajiandaa kwenda kwa wananchi ili kama kuna athari zozote tuweze kuzijua," alisema mkurugenzi huyo.

Aidha, alisema mamlaka hiyo imeitisha kikao cha dharura cha mikakati ya maafa wilaya ili kuchukua tahadhari za kukabiliana nayo.

Aliwataka wananchi kuchukua tahadhari na wale ambao wanaishi mabondeni kuhama ili kuepukana na athari ambazo zinaweza kujitokeza.

# Wataka kasi ujenzi barabara ya Jozani

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANANCHI wa Kijiji cha Ukongoroni Mkoa wa Kusini Unguja, wameiomba serikali kuharakisha ujenzi wa barabara inayotoka Jozani hadi kijijini kwao ili kuondokana na usumbufu wanaoupata sasa.

Wakizungumza na Nipashe kijijini hapo, wananchi hao walisema kuwa kutokamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo, wanapata usumbufu wa usafiri wanapotaka kwenda nje ya kijiji hicho kwa ajili ya shughuli zengine zikiwamo za kiuchumi.

Shauri Ali Makame, alisema kuwa kutokamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo, wanashindwa kusafirisha mazao yao kupeleka sokoni.

"Kama ulivyojionea ndugu mwandishi, usafiri wa gari za abiria kwetu ni shida… tuna gari moja tu ya abiria ukiikosa hiyo huna safari au utembee kwa mguu hadi Jozani, wakati ni masafa marefu zaidi ya kilomita tano hadi kufika barabara kuu ya Jozani," alisema.

Naye Ushenza Mwita Makame, alisema kutokamilika ujenzi wa barabara hiyo wanapata usumbufu mkubwa hasa wakati kinamama wanapokuwa wajawazito kuharakishwa hospitali kwa ajili ya kujifungua.

Alieleza kuwa kituo cha afya kilichopo kijiji hapo hakitoi huduma za mjamzito kujifungua, hivyo hulazimika kwenda Hospitali ya Makunduchi kwa ajili ya kupata huduma hiyo.

"Tunasumbuka sana katika suala la usafiri hasa kwa wajawazito kuwatoa hapa na kuwapelekea hospitali kwa ajili ya kujifungua," alisema.

Kwa upande wake Naibu Sheha wa Shehia ya Ukongoroni, alieleza kuwa ujenzi wa barabara hiyo umeanza na serikali ipo katika hatua za kukamilisha ujenzi huo ili kuwaondoshea usumbufu wananchi katika suala la miundombinu ya barababra.

Akizungumzia kuhusu kituo cha afya kijiji hapo, alisema kuwa kituo hicho kina uwezo wa kutoa huduma za uzazi, lakini tatizo hawana wataalamu kwa ajili ya kuwazalisha wajawazito.

# Wanawake wapewa somo kuwa wathubutu

**Na Mwandishi Wetu, SIMIYU**

BENKI ya NMB imewataka wanawake wote nchini kutumia nafasi na uwezo walionao kudhubutu katika kufanya jambo lolote la kujiletea maendeleo ikiwa pamoja na kujiamini kwa kile wanachoweza kufanya.

Wito huo ulitolewa juzi na Kaimu Mkurugenzi wa Benki hiyo, Ruth Zaipuna, wakati akitoa salamu za benki hiyo kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake kitaifa yaliyofanyika mkoani Simiyu uwanja wa Halmashuari ya Mji wa Bariadi.

Zaipuna aliwasisitiza wanawake kuendelea kuthubutu, kujiongezea maarifa, kuongeza ujuzi na uzoefu ili kuweza kufikia malengo yao, sambamba na kutiana moyo katika kujenga umoja wa kitaifa.

Alisema kuwa NMB imekuwa ikipata mafanikio makubwa hapa nchini kutokana na kutambua kuwa ajenda ya usawa wa kijinsia ni ajenda ya kibiashara ndani ya benki yenyewe na nje.

Alisema kuwa NMB iligundua kuwa kampuni nyingi kubwa duniani ambazo zimepata mafanikio makubwa, yaliweka ajenda ya usawa wa kijinsia kama ajenda kuu kwao katika kujiletea faida kwenye biashara yao.

"NMB tuligundua kuwa kampuni nyingi duniani zilipogundua hili na kulifanyia kazi, zilipata mabadiliko makubwa kwa namna wanavyofanyabiashara na maamuzi na kupata faida kubwa na jamii kwa ujumla," alisema Zaipuna.

"Kama benki kubwa nchini nasi tulipogundua hili tukaanza kulitekeleza, ambapo utekelezaji wake siyo ndani tu ya benki, lakini pia hata kwa wateja wetu na ndiyo maana tumekuwa na huduma rafiki kwa wanawake," aliongeza.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi huyo alisema kuwa mbali na huduma hizo, benki hiyo imekuwa ikisaidia sekta ya elimu hasa kwa wasichana, lengo likiwa kuwafanya waweze kufikia malengo yao.

Alisema kuwa ili wanawake waweze kufanikiwa na kufikia malengo lazima washikane mikono, washirikiane katika nyaja za elimu, uongozi, malezi, biashara pamoja na mahusiano.

"Niwatie moyo wanawake wote nchini kuwa tunaweza, kama tutaamua kufanya kazi bila ya kubagua, kuangalia hali uliyonayo, tutaweza kufikia malengo kikubwa tuwe na nia, hali na uwezo," alisema Zaituna.

# Alalamika kufukuzwa kazi serikalini bila mafao

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA mtumishi wa Shirika la Elimu Kibaha, Mwbana Kilewa, amelalamika kunyimwa haki zake ikiwamo mafao kwa madai kuwa hakuwa na sifa licha ya kuajiriwa kwa nafasi ya mlinzi akiwa na elimu ya darasa la saba.

Akizungumza katika ofisi za Nipashe, alisema aliajiriwa Desemba 27 mwaka 2000 kwa mkataba wenye kumbukumbu namba 9212 wa miezi mitatu na kila ulipoisha aliongezewa muda akiwa na elimu ya darasa la saba.

Alisema kwa muda wote alilipwa kima cha chini cha mshahara wa taasisi za serikali na makato yake kupelekwa kwenye Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Alisema Julai 18, mwaka 2017 aliandikiwa barua ya kusimamishwa kwenye mfumo wa mishahara, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora).

Kilewa alisema mwajiri alidai kuwa sheria imeweka masharti kwamba kiwango cha chini cha kuwezesha mtumishi kuajiriwa katika utumishi wa umma ni cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne, na kwamba licha ya kuandikiwa barua awasilishe vyeti hivyo, lakini hakuwa navyo.

Alisema barua hiyo ilieleza kuwa amfukuzwa kazi kwa kuwa ameshindwa kupeleka vyeti hivyo, wakati walijua kuwa ana elimu ya darasa la saba tangu anaajiriwa.

"Nimeajiriwa kwa mkataba toka wakati huo hadi mwaka 2010 nilipewa ajira kamili, cha kushangaza wamenifukuza kazi kwa madai sina vyeti wakati nilianza kuajiriwa chini ya waraka wa utumishi namba 1 wa mwaka 2004," alisema.

"Sikuajiriwa kwa vyeti feki bali niliajiriwa kwa mkataba wakijua elimu yangu, lakini nimehukumiwa kama vyeti feki na nimekosa haki zangu ambazo sikustahili kukosa, mfano nilichangia Sh. milioni 6 NSSF tangu mwaka 2001 hadi 2017 nikichangia miezi 15, hizo fedha zimekwenda wapi?" Alihoji.

Kwa mujibu wa barua ya Katibu Mkuu Utumishi ya Januari 31, mwaka huu, iliyosainiwa kwa niaba yake na Ibrahim Mahuni, yenye kumbukumbu namba FC.28/205/01/"Q"/127, suala lake halitekelezeki.

"Ajira yako haikuwa mwendelezo wa ajira ya kwanza uliyoajiriwa kwa mkataba mwaka 2001," ilisema sehemu ya barua hiyo.

Barua hiyo ilisema maombi yake ya kurejeshwa kazini hayatekelezeki kwasababu anakosa sifa kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa mwaka 2004 ukisomwa pamoja na Kanuni 17 (5) ya kanuni za utumishi wa umma za mwaka 2003.

Aidha, aliiomba serikali kufuatilia suala hilo kwa kina ili apate stahili zake kwa kuwa aliajiriwa kwa mkataba kabla ya waraka wa utumishi wa mwaka 2004.

Mwaka jana, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), George Mkuchika, alikaririwa akisema watumishi wote waliokuwa na ajira za kudumu au za mikataba waliokuwa kazini kabla ya Mei 20, mwaka 2004 walipoanza kutumika waraka wa utumishi namba 1 wa mwaka 2004 warejeshwe kazini.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan (kulia), akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Serikali wa NMB Vicky Bishubo (kushoto), alipotembelea banda la benki hiyo mjini Bariadi mkoani Simiyu kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Wa pili kulia ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bisimba awapasha watetezi haki wanawake

**Na Sabato Kasika**

WATETEZI wa wanawake na haki za binadamu, wamekumbushwa kuwa kazi hiyo siyo ya ajira, bali ni ya kujitolea na ni ya wito, hivyo waifanye kwa moyo wote.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Hellen Kijo-Bisimba.

Alikuwa katika uzinduzi wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Wanawake Tanzania na kusema, ajira ina saa za kufanya kazi, lakini suala la utetezi ni wakati wowote.

"Kama kuna mtu anadhani kuwa utetezi ni ajira, ni bora atafute kazi nyingine ya kufanya kwani hii ni ya wito, wakati wowote unafuatwa na watu kusikiliza matatizo yao," alisema Kijo -Bisimba.

Naye Mkurugenzi wa Women Fund Tanzania, Mary Rusimbi, aliutaka mtandao huo kuhakikisha unasimama imara bila kuyumba.

"Majukwaa yanayotuunganisha ni muhimu sana, katika kuleta mabadiliko yenye tija kwa wote, na kwamba Women Fund Tanzania unaunga mkono," alisema Rusimbi.

Alisema, anatarajia kuona mtandao huo haugawi watu katika makundi na badala yake bila kujali umri, wawe wamoja na kuhakikisha lengo lao linatimia.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwohede, Justa Mwaituka, alisema utetezi wa haki za wanawake na haki za binadamu hawapaswi kuwa waoga.

"Mnaweza kuitwa majina mengi ya kukatishs tamaa, lakini msirudi nyuma katika kazi hii kwani ina changamoto zake, na pia mjue mnachopambania, kiko eneo lipi kisheria au kikanuni, " alisema Mwaituka. Alisema, kwa miaka 20 wao Kiwohede imepambania kutokomeza suala la changudoa bila kukata tamaa, hivyo mtandao huo ni muhimu uige mfano.

"Kingine ni mitandao yote ya kutetea haki za wanawake na haki za Bunda kuwa kitu kimoja, wasiwepo wa kudhani kwamba wanaweza kufanya kazi peke yao bila ushirikiano," alisema.

Akielezea uanzishwaji wa mtandao huo, katibu wake, Hilda Stuart, alisema, unaundwa na mashirika yasiyo ya kiserikali zaidi ya 50.

"Lengo ni kuweka wazi majukumu ya mtandao, changamoto zake, kujengea wanawake uelewa kuhusu dhana za kijinsia na ubaguzi wa kujinsia," alisema Hilda.

HABARI KIMATAIFA

## Rais Xi Jinping atembelea mji wenye corona

**BEIJING,** China

RAIS wa China, Xi Jinping, ameutembelea mji wa Wuhan jana kwa mara ya kwanza tangu mji huo ulipokumbwa na janga la mlipuko wa virusi vya corona Januari mwaka huu.

Hatua ya Rais huyo wa China kwenda Wuhan ambako ni kitovu cha maradhi yanayosababishwa na virusi vya corona ni dalili kubwa inayowafanya maofisa kuamini kwamba mlipuko huo umedhibitiwa.

Ziara ya Xi imekuja baada ya hatua ya mji wa Wuhan na Jimbo la Hubei kuwekwa kwenye karantini tangu mwishoni mwa Januari kuonyesha kufanikiwa na maambukizi mapya yamepungua kwa kiasi kikubwa.

Hatua iliyopigwa na China ni ishara ya namna tatizo hilo linavyoendelea kuenea duniani ambapo sasa unasambaa kwa kasi kubwa nje ya China wakati ambao nchi ya Italy imeanza kutekeleza hatua ya karantini nchi nzima. **DW**

# Marekani yaanza kuondoa majeshi Afghanistan

**KABUL,** Afghanistan

MAOFISA wa Marekani wamesema baadhi ya wanajeshi wake wameanza kuondoka nchini Afghanistan, kama ilivyokubaliwa kwenye makubaliano ya amani na kundi la Taliban.

Mamia ya wanajeshi wa Marekani wameanza kuondoka nchini humo kama ilivyokuwa imepangwa awali, lakini hawatobadilishwa kutokana na kwamba Marekani inataka kusonga mbele na mipango yake ya kupunguza idadi ya askari wake kutoka 13,000 hadi 8,600.

Hatua ya kuwaondoa askari hao imekuja wakati ambao viongozi hasimu wa Afghanistan wote wakiapishwa Jumatatu katika hafla mbili tofauti kama marais wa nchi, na hivyo kuibua wasiwasi kwa Marekani wa jinsi ya kuendelea na utekelezaji wa makubaliano ya kukomesha vita ya miaka 18.

Mvutano baina ya Rais Ashraf Ghani ambaye alitangazwa kuwa mshindi wa uchaguzi wa Septemba mwaka jana na hasimu wake Abdullah Abdullah ambaye alielezea udanganyifu katika uchaguzi, unatoa mashaka kwa hatua muhimu inayofuata na hata kuhatarisha kutumbukia tena katika machafuko.

**Jukumu letu ni kuhakikisha amani na kumaliza miaka 40 ya vita. Nitahakikisha amani inarejea na ujasiri wa watu na mfumo wa Jamhuri.**

Mvutano huo wa kisiasa umeleta shakani mazungumzo ya ndani na kundi la Taliban ingawa Rais Ghani alisema kwamba alianza kuunda timu ya majadiliano.

"Jukumu letu ni kuhakikisha amani na kumaliza miaka 40 ya vita. Nitahakikisha amani inarejea na ujasiri wa watu na mfumo wa Jamhuri," alisema Rais Ghani wakati akiapishwa Jumatatu.



Msemaji wa jeshi la Marekani nchini Afghanistan, Sonny Legget (pichani) alisema kwamba jeshi limeanza kutimiza sharti la kupunguza wanajeshi hadi 8,600 ndani ya siku 135.

Kati ya wanajeshi 13,000 wa Marekani walioko Afghanistan, 8,000 wanajihusisha na mafunzo na kuvishauri vikosi vya Afghanistan, wakati wengine 5,000 wakishiriki kwenye operesheni ya kupambana na ugaidi sambamba kulisaidia jeshi la nchi hiyo pindi wanapohitajika.

Ghani alikuwa akijishauri kuwaachia wafungwa wapatao 5,000 wa Taliban, kitu kilichokubaliwa kwenye mkataba wa amani wa Taliban na Washington.

Lakini Jumanne Ghani aliahidi kwamba atatangaza amri ya kuachiliwa wafungwa, baada ya Marekani na maofisa kadhaa wa kigeni kuunga mkono juhudi hizo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, alipongeza hatua hiyo ya Ghani ingawa alipinga vikali kuanzishwa kwa serikali mbili mjini Kabul. **DW**



Rais wa China, Xi Jinping akiongea na wakazi wa Beijing. **PICHA: XINHUA**

# Kenyatta aainisha vipaumbele vita dhidi ya malaria

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, ambaye hivi karibuni aliteuliwa kuwa mwenyekiti wa Umoja wa Marais wa Afrika wanaopambana na malaria (ALMA), ametangaza vipaumbele vinne katika kutokomeza malaria Afrika ifikapo mwaka 2030.

Vipaumbele hivyo vinatarajia kuleta mapinduzi vinalenga kutafuta suluhu dhidi ya changamoto za mapambano ya kutokomeza malaria.

Changamoto hizo ni pamoja na ushiriki hafifu wa wanawake, watoto na vijana, uhaba wa fedha toka sekta za ndani, za umma na binafsi pamoja na tishio la kudumaa kwa michango ya wahisani.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kenyatta alisema: "Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye vita hii ndani ya miaka 10 iliyopita, ili kuwa na Afrika tunayoitaka kama ilivyoelezwa kwenye mpango wa 2063, tusijisahau, badala yake tutafute na kupata rasilimali zaidi zitakazotusaidia kutokomeza malaria na kuokoa maisha."

Alisema: "Na ndiyo maana tumeainisha maeneo ya vipaumbele yatakayokuwa msingi wa utendaji kazi wangu kama mwenyekiti wa ALMA".

Kenyatta alitaja mikakati hiyo ni uanzishwaji wa majukwaa ya kidijitali yanayofika katika mataifa mbalimbali ili kusaidia upatikanaji na uwazi wa takwimu za mapambano dhidi ya malaria.

Mkakati mwingine ni ushirikiano na mashirika ya kikanda ndani ya Afrika kufanya kazi na mashirika ya kikanda ili kushirikiana na wakuu wa nchi na serikali katika kujadili na kutatua changamoto kubwa na kutafuta majibu ya namna ya kutokomeza ugonjwa wa malaria.

Mwingine ni kuanzishwa kwa mabaraza na mifumo ya kutokomeza malaria, kuanzisha mabaraza mapya 15 ya kutokomeza malaria, kutafuta fedha zitakazosaidia kuongeza ushirikiano wa ngazi za juu wa sekta tofauti ili kutia chachu juhudi za kupata fedha zaidi za ndani ikiwamo kutoka katika sekta binafsi.

Kenyatta alitaja mkakati mwingine ni wa makundi ya ushauri ya vijana kwa kushirikiana na viongozi vijana toka maeneo mbalimbali ya kiongozi barani Afrika, kujenga "Jeshi la Vijana" dhidi ya malaria.

"Kikosi-kazi hiki cha mabalozi vijana kitaanzisha ushirikiano wa kisiasa, utafutaji wa fedha, ubunifu, utafiti na maendeleo na hata kuundwa kwa kada ya watu wanaopambana dhidi ya malaria," alisema Kenyatta.

Mtendaji Mkuu wa ushirikiano wa RBM wa Kutokomeza Malaria, Dk. Abdourahmane Diallo alisema: "Uongozi toka kwa viongozi wa nchi na serikali barani Afrika ambao kutokomeza malaria ni moja ya sera zao muhimu za kisiasa, ni muhimu sana katika vita hii.

Alisema vipaumbele vinne vya Rais Kenyatta, vikiongozwa na ubunifu na ushirikishwaji wa wadau wote ndio njia sahihi ya kufikia malengo ya kutokomeza malaria. **ALMA**

# Mhagama asisitiza ofisi mpya NEC kuratibu uchaguzi mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amekagua hatua ya ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), zilizopo eneo la Njedengwa jijini Dodoma, na kusema serikali imedhamiria shughuli za uchaguzi mkuu mwaka huu kufanyika kwenye jengo hilo jipya la tume hiyo.

Alibainisha hayo jana alipofanya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa majengo ya tume hiyo, ambapo alikagua hatua za ujenzi wa ofisi za tume hiyo kwa kukagua jengo kuu la ofisi, jengo la kutangazia matokeo na ghala la kuhifadhi vifaa.

Kukamilika kwa majengo hayo itakuwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliyoyatoa Novemba mwaka jana.

Waziri Mkuu aliitaka tume hiyo kuhakikisha ujenzi wa ofisi zake, unakamilika kwa wakati, ili shughuli za uchaguzi mkuu wa mwaka huu zinafanyike kwenye majengo hayo.

Chuo Kikuu cha Ardhi na Kampuni ya Ujenzi ya Jeshi la Kujenga Taifa- SUMA JKT CCL ndio wanaohusika na shughuli za ukandarasi wa majengo hayo.

NEC idara huru iliyoanzishwa mwaka 1993 kwa mujibu wa Ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1997.

Kwa kipindi chote hicho tangu kuanzishwa kwake tume hiyo haijawahi kumiliki jengo lake lenyewe, hivyo mwaka 2016, Rais John Magufuli alikubali ombi la tume hiyo kujenga jengo lake.




Muuguzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyamala, Rose Musa (wa tatu kushoto), akipokea msaada wa vitu mbalimbali vikiwamo sabuni, mashuka na mataulo ya kike vilivyotolewa na wafanyakazi wa kampuni ya Bima ya Jubilee Insurance, kwa kusaidia wanawake waliolazwa katika wodi ya wazazi ya hospitali hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, jijini Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU.**

# Ukerewe kutokomeza malaria kwa kuangamiza viluwiluwi

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

UANGAMIZAJI wa viluwiluwi vya mbu waenezao malaria kwa kutumia viuadudu na upuliziaji wa dawa ya ukoko majumbani umezinduliwa ili kuangamiza mbu katika Wilaya ya Ukerewe.

Akizindua zoezi hilo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, aliwataka wananchi wilayani humo kupuuza uvumi kwamba dawa hiyo inasababisha kunguni na kupunguza nguvu za uzazi.

Alisema malaria ni ugonjwa unaosababisha athari nyingi za kiafya na hata vifo kwa jamii hasa kwa watoto na wajawazito na kwamba utafiti wa viashiria vya ugonjwa huo uliofanyika mwaka 2017, Mkoa wa Mwanza bado unaonekana kuwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya ugonjwa huo kwa asilimia 8.1 kikiwa juu ya kiwango cha taifa ambacho ni asilimia 7.3.

Upuliziaji huo utakaodumu kwa mwezi mmoja ulianza kutekelezwa Machi 3, mwaka huu katika vijiji 76 vya wilaya hiyo, ukifadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Abt Associates.

"Matokeo ya upimaji wa vimelea vya malaria kwa watoto wa shule ya msingi uliofanyika mwaka 2017 na 2019 wilayani humo, yalionekana kuwa na kiwango kikubwa cha watoto wenye malaria na mwaka 2017 ni kwa asilimia 51, huku mwaka jana ikiwa ni asilimia 44.2, hivyo hivyo takwimu za afya zinazotokana na mfumo wa Wizara ya Afya katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo wilaya hiyo imeonekana kuwa na kiwango kikubwa cha vimelea vya ugonjwa huo kwa asilimia 52.6 ya wagonjwa waliotumwa maabara kupima mwaka 2017 walikutwa na vimelea vya malaria, asilimia 15.4 kwa mwaka 2018 na asilimia 51.1 kwa mwaka jana," alisema Mongella.

Dk. Godian Kikompolisi, ambaye ni mratibu wa mkoa Abt Associates, alisema dawa hiyo inatumia wastani wa siku tano kuua mbu waenezao malaria kwenye ukuta wa nyumba.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Silas Wambura, alisema ili kuangamiza mbu waenezao malaria katika mazingira ya kisiwa cha Ukerewe, mbinu mbalimbali zinatumika kwa wakati mmoja.

"Tumeanza na mazoezi haya mawili, lakini lengo letu mbu anapozaliwa kwenye madimbwi tunanyunyuzia dawa huku zoezi la kuwaua waliopo kwenye majumba linaendelea hivyo tuna tumia silaha mbili kwa wakati mmoja," alisema Wambura.

Mashauri Saidi na Paskazia Masanga, wakazi wa kijiji cha Hamukoko, waliwaomba wataalamu wa afya kuanza kuweka dawa kwenye madimbwi ndipo waingie kwenye nyumba zao.

Zaidi ya kaya 80,000 katika vijiji 76 vya wilaya hiyo zitapata huduma hiyo, huku zoezi hilo likitoa na ajira kwa wakazi wa Ukerewe, wananchi 622 na viongozi wa vitongoji 483 wamepatiwa ajira za muda mfupi.

## Shule yaomba kutatuliwa miundombinu ya barabara

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama, mkoani Shinyanga imeombwa kutatua changamoto ya miundombinu ya barabara katika eneo la shule mpya ya msingi Maila ili kuondoa usumbufu kwa wanafunzi.

Shule hiyo ilijengwa kwa nguvu ya wananchi wa mtaa wa Nyihogo, kitongoji cha Amani B Maila kwa lengo la kuepusha ajali kwa watoto kugongwa na magari wakati wakivuka barabara na Rais John Magufuli, aliunga mkono kwa kuchangia Sh. milioni tano.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Masula Japhet, alitoa kilio hicho baada ya kutembelewa na Mbunge wa Jimbo la Kahama Mjini, Jumanne Kishimba, kukagua ujenzi wa majengo ya shule na kupata taarifa ya changamoto zinazoikabili.

Japhet alimweleza mbunge huyo kuwa shule hiyo yenye wanafunzi 621 na walimu saba ina vyumba vya madarasa vinane ambavyo havitoshelezi idadi ya wanafunzi ikiwamo ofisi moja ya walimu.

Alisema mahitaji ni vyumba 14 na kukosekana kwa miundombinu ya barabara.

"Mheshimiwa Mbunge changamoto kubwa inayotukabili shuleni ni kukosekana kwa miundombinu ya barabara kipindi cha mvua za masika kama sasa wanafunzi wanaosoma hapa wanateseka hata wewe umeona gari umeliacha mbali na shule, tusaidie mheshimiwa tushirikiane na serikali pamoja na wadau wengine kumaliza changamoto," alisema Japhet.

Diwani wa Kata ya Nyihogo, Shadrack Mgwami, alimweleza mbunge kuwa wananchi walihamasika na ujenzi wa shule hiyo na kwamba hadi sasa masomo yanaendelea na kati ya vyumba vinane vilivyopo vinavyotumika ni saba na kuongeza kuwa kunahaja ya kuongeza vyumba vingine vya madarasa.

Alisema fedha aliyotoa Rais na nyingine kutoka Mfuko wa Jimbo zipo katika akaunti ya kijiji na changamoto ni mfumo wa kuzihamisha.

Kwa upande wa Kishimba alisema kwa sasa hataweza kutatua changamoto ya barabara na kueleza cha muhimu kwa sasa nguvu kubwa iwekezwe katika ujenzi wa vyumba vya madarasa.

"Binafsi nimechangia shule hii zaidi ya Sh. milioni tano za kwangu binafsi na za mfuko wa jimbo pamoja na matofali 2,000, kwa sasa sitaki kusikia suala la ujenzi wa barabara badala yake nguvu kubwa tuziweke kwenye madarasa ili watoto wetu wasome bila shida," alisema Kishimba.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**HAGALI MARTIN MBULLA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya bajaji yenye namba za usajili **MC 780 AUW.** Chassis namba...Engine namba. ... Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/151509/2020**

115663702

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 66 YA MWAKA 2019**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**YOHANA DAUDI MAJOLA BALELE**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**EDDA YOHANA BALELE**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa baruza za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 21 Mwezi wa April, 2020.

Imethibitishwa Dar es salaam, leo tarehe 3 Mwezi wa Machi, 2020.

MUTABUZI & CO. ADVOCATES
P. O. Box 5539,
D' SALAAM.

115662802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA: 63)**
**Mahakama ya Mwanzo ya …………..MJINI**
**………….TANGA**
**Wilaya ya TANGA**
**MADAI NAMBARI…29….. ya…. 2020**
**Mdai LAURENT FUNGAVYEMA**
**Mdaiwa METHOD NDAMNYAZWE**

Kwa: METHOD NDAMNYAZWE
C/O MWENYEKITI KANGE

Kwa kuwa mdai ameleta MADAI YATshs 1,120,980/=

Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya **JUMANNE** Tarehe17/03/2020 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shauri hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 09/03/2020.

115663302

---

**JAMHURIYAYAMUUNGANOWATANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;71/2020**

**Ombi la KASIMU AMAN KASANGA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu GRACE EMILY SENGO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 10/03/2020.

115663802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA WATANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;68/2020**

**Ombi la LOVENESS LEONARD MTAITA. Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu LEONARD AMOS MTAITA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/03/2020

115663902

---

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

**CHINA CIVIL ENGINEERING CONSTRUCTION CORPARATION** anatangaza kupotelewa na kadi za gari aina za **SINO TRUCK** yenye namba za usajili **T949CGW** na **T920CGW**.Chassis namba **CC162803.** Engine namba. **E3718C00032** na **CC162804,** Engene no. **E37118C00034.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/217898/2020**

115663602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;70/2020**

**Ombi la SALUM SAID RAJABU Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SAID RASHID ABDALLAH**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 15/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/03/2020.

115664002


**Uza, Chenye Thamani Kubwa**

**Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# MARI ATAKA MKATABA WA KUDUMU ARSENAL

**LONDON,** England

MCHEZAJI anayecheza kwa mkopo Arsenal, Pablo Mari, anataka mkataba wa kudumu kwa miamba hao wa Ligi Kuu England kutoka Flamengo mwishoni mwa msimu huu.

Mari aliondoka kwa mabingwa wa Brazil Flamengo na kujiunga Arsenal kwa mkataba wa awali wa mkopo wakati wa dirisha dogo la Januari na beki huyo amenogewa.

Katika mechi zake mbili alizoichezea Arsenal, mlinzi huyo wa kati Mhispania, Mari amekisaidia kikosi hicho cha Mikel Arteta kucheza mechi mbili bila kuruhusu bao.

"Ndio, bila shaka," alisema Mari akiwaambia waandishi wa habari wakati alipoulizwa kama anataka kujiunga kwa mkataba wa moja kwa moja Arsenal baada ya ushindi wa Jumamosi wa 1-0 dhidi ya West Ham.

"Nina furaha hapa. Nitajaribu kucheza kwa kiwango changu hadi mwisho wa msimu. "Natumaini pia klabu ina furaha na mimi na halafu tutatafuta kuwa na mwisho mzuri kwa kila mmoja.

"Nataka kucheza hapa katika moja ya ligi bora duniani na nipo hapa kwa sasa. Nitafanya kila linalowezekana kwa timu, kwa klabu, kushinda mechi na pia kwa mashabiki kufurahia na mimi."

Arsenal wapo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kucheza mechi 28, wakipitwa pointi nane na wapinzani wao wa jiji la London, Chelsea, ambao wapo nafasi ya nne ambayo ni ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Arteta: Man City haina bahati

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesisitiza Manchester City imekuwa "haina bahati" msimu huu huku ikitoka kucheza kichapo kwa dabi ya Manchester.

Kikosi hicho cha Pep Guardiola kilifungwa 2-0 na Manchester United Jumapili na kuwaacha vinara wa Ligi Kuu Liverpool wakihitaji pointi sita tu kushinda taji hilo.

Kwa ujumla kikosi cha Jurgen Klopp kinaweza kuwa bingwa kabla ya mechi yao ijayo kama City itapoteza mechi zake mbili za nyumbani dhidi ya Arsenal na Burnley wiki hii.


City imefungwa mara mbili na United na mara moja na Tottenham tangu Arteta aondoke kwenye nafasi yake ya kocha msaidizi kuchukua majukumu ya ukocha pale kwenye dimba la Emirates, na kuacha pengo kwa Guardiola, licha ya kushinda taji la EFL na kupata ushindi wa 2-1 dhidi ya Real Madrid kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora.

Arteta anaamini bahati haijawa upande wao na hana shaka kwamba Arsenal lazima iwe katika ubora wake ili kupata matokeo pale kwenye dimba la Etihad.

"Wakati mwingine, mambo madogo yanatengeneza tofauti. Nafikiri wamekuwa hawana bahati," alisema Jumatatu. "Huu ni mchezo wa soka. Inaweza kutokea.

"Tumekuwa kwenye ubora wetu, kwa uhakika kuwa na nafasi ya kushinda mchezo."





# *Shaw: Kuna mengi yanakuja kwa Fernandes*

**MANCHESTER,** England

BEKI wa kushoto wa Manchester United, Luke Shaw ameonya kuna mambo mengi mazuri yanakuja kutoka kwa nyota Bruno Fernandes pale Old Trafford.

Fernandes amekuwa nguzo muhimu tangu alipotua hapo kutoka Sporting CP Januari, akifunga mabao mawili na kutoa asisti tatu kwenye mechi tano za Ligi Kuu England. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno alitengeneza pasi nzuri kwa Anthony Martial kwenye ushindi wa 2-0 Jumapili dhidi ya Manchester City - na shuti lake lilipanguliwa kabla ya Scott McTominay kufunga bao la ushindi.

Fernandes amesifiwa kwa kiwango alichoonyesha na mchezaji mwenzake Shaw ameungana na orodha ya wachezaji wengine kumsifia.

"Ni mchezaji mwenye uwezo wa aina yake tangu atue hapa na tayari amekuwa na asisti na magoli machache.

"Tutaendelea kushirikiana nae na kusukuma mafanikio ya klabu kwa sababu kuna mengi yanakuja kutoka kwake."

United kwa sasa inaonekana kuwa kwenye kiwango bora chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer na haijapoteza mchezo wowote katika mechi 10 kwenye mashindano yote.

HABARI MICHEZO

# Mbappé hatarini kuikosa Dortmund

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain imekumbwa na pigo kubwa kuelekea mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora dhidi ya Borussia Dortmund baada ya fowadi wake, Kylian Mbappé kushindwa kufanya mazoezi Jumatatu.

Dortmund walipata ushindi wa 2-1 pale kwenye dimba la Signal Iduna Park katikati ya Februari shukrani kwa mabao mawili ya Erling Haaland, lakini Neymar aliwafungia la kufutia machozi.

PSG bado inahitaji kubadilisha upepo Jumatano, lakini sasa itakuwa bila ya Mbappé leo Jumatano baada ya kushindwa kufanya mazoezi na wachezaji wenzake.

PSG walikuwa wakitarajia Mbappé kuwa fiti jana Jumanne kwa ajili ya mchezo huo wa leo, lakini yupo kwenye hatihati ya kuukosa mchezo huo.

Hata hivyo, Mbappé katika mechi za hivi karibuni hajawa kwenye kiwango chake na hivyo kukosekana kwake kunaweza kusiwe pigo kubwa kwa kikosi hicho.

Mfaransa huyo awali alikabiliwa na majeruhi kabla ya kurudi uwanjani na kuna uwezekano mkubwa akaukosa mchezo wa leo.






# BERGWIJN AMPA PIGO MOURINHO

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, José Mourinho, amebainisha kwamba, Steven Bergwijn atakuwa nje kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki baada ya kuumia enka wakati wa mchezo wa sare ya kufungana 1-1 dhidi ya Burnley.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi alimaliza dakika zote 90 kwenye mchezo huo wa wikendi licha ya kuumia na ilionekana majeruhi yake sio makubwa.

Akizungumza kuelekea mchezo wa jana Jumanne dhidi ya RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Mourinho alisema: "Simtarajii Steven kucheza tena msimu huu."

"Naweza kuamini hilo? Ndio, naweza," alisema Mourinho na kuongeza. "Sikujua kama hali itakuwa hivi, hasa kutokana na namna alivyoumia.

"Ni Harry Kane pekee ndio majeruhi yake yalionekana kuwa makubwa zaidi tangu Desemba kwenye Ligi Kuu.

"Hugo Lloris, (Moussa) Sissoko, Sonny (Son Heung-min), Steven Bergwijn wote ni majeruhi na hawatarajii kurudi dimbani hivi karibuni.

"Hivyo ndio hali halisi ilivyo kwa sasa. Kisaikolojia tulikuwa na majeruhi mengi. Kwa hakika sasa tupo kwenye wakati mgumu kuelekea mwishoni mwa msimu."

# *Barcelona vs Napoli kucheza bila mashabiki*

**BARCELONA,** Hispania

MCHEZO wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 kati ya Barcelona na Napoli utachezwa bila mashabiki huku milango ikiwa imefungwa kutokana na tishio la ugonjwa wa corona.

Serikali ya jimbo linalojitawala kisiasa la Katalunya limetangaza kwamba mchezo huo utakaopigwa Machi 18 pale kwenye dimba la Camp Nou hautaruhusiwa kuhudhuriwa na mashabiki.

Maamuzi yao yamethibitishwa na Barca baada ya kikao kati ya maofisa wa klabu na wa serikali ya Katalunya, akiwamo Katibu Mkuu wa soka, Gerard Figueras. Taarifa hiyo ilisema: "Maamuzi haya yamechukuliwa kwa sababu ya usalama wa afya."

Tangazo hilo limekuja baada ya nchini Italia ligi zote kusimamishwa hadi Aprili 3 kwa sababu ya mlipuko huo wa ugonjwa wa corona.

Waziri Mkuu wa Italia, Giuseppe Conte, alisema Jumatatu kwamba, wananchi wote wa Italia hawataruhisiwa kusafiri labda kwa dharura tu.

Hata mchezo wa jana Jumanne kati ya Atalanta na Valencia pia ulichezwa bila mashabiki.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LIGI KUU ITALIA YAPIGWA 'STOP'

Ni kutokana na kasi ya maambukizi ya virusi vya corona, lakini mechi za Ligi ya Mabingwa...

**MILAN,** Italia

SERIKALI ya Italia imesimamisha michezo yote nchini humo kwa muda wa mwezi mmoja kufuatia kuenea kwa virusi vya ugonjwa wa corona.

**Kamati ya Olimpiki ya Taifa ilithibitisha katika taarifa yake juzi kuwa shughuli zote za michezo nchini humo ikiwamo mechi za Ligi Kuu Italia maarufu Serie A, ambayo ndiyo ligi ya juu nchini humo, lakini hai tahusisha klabu za Italia na timu za Taifa ambazo zinakabiliwa na mechi za mashindano ya kimataifa kama Ligi ya Mabingwa Ulaya.**

Kamati hiyo ambayo inasimamia michezo yote nchini humo, ilisema katika taarifa yake kuwa agizo hilo la kusimamisha michezo litadumu hadi Aprili 3, mwaka huu na itasubiri tamko la serikali ili kutoa maelekezo mengine.

Italia sasa ni nchi ya tatu yenye idadi kubwa ya wagonjwa waliobainika kuwa na virusi vya corona, nyuma ya China na Korea Kusini, hali ambayo imesababisha kusimamisha michezo yote.

Zaidi ya watu milioni 16 wanaoishi eneo la Kaskazini mwa Italia wamewekwa katika uangalizi maalumu ili kupunguza maambukizi ya virusi hivyo.

Ligi Kuu ya nchi hiyo ilianza kutekeleza agizo la kupambana na maambukizi Jumapili iliyopita kwa mechi tano kuchezwa bila ya mashabiki, ikiwamo mchezo kati ya mabingwa mara nane mfululizo wa ligi hiyo, Juventus dhidi ya Lazio, ambao ulimalizika kwa kugawana pointi moja moja.

Serie A ilikuwa haijawahi kusimama tangu kumalizika kwa vita vya pili vya dunia.

Taarifa kutoka kwa kamati hiyo ambayo inajulikana kwa jina la CONI, ilitolewa zikiwa zimebakia dakika chache kabla ya kuanza kwa mechi kati ya Sassuolo dhidi ya Brescia, mchezo ambao uliahirishwa kabla ya kuanza.

CONI ilifafanua katazo hilo halitahusisha mechi za mashindano ya kimataifa na timu za Taifa kwa sababu hizo haziko chini yake. Juventus, Napoli na Atalanta ziko katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati Inter Milan na Roma zenyewe zinachuana kuwania ubingwa wa Ligi ya Europa.

Mapema wiki hii, Shirikisho la Mchezo wa Kuogelea Italia liliondoa timu yake katika mashindano ya kimataifa ikiwamo mechi za kuwania tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki iliyopangwa kufanyika mjini Riccione wiki ijayo.

Michezo ya Olimpiki ambayo itachezwa mjini Tokyo miezi minne ijayo, inatajwa zaidi ya wanamichezo 300 wa Italia walifuzu tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki iliyofanyika mwaka 2016 jijini Rio de Janeiro.

Ufaransa, Polisi ilisema mechi kati ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya nchi hiyo Paris Saint-Germain dhidi ya Borussia Dortmund itakayochezwa kwenye Uwanja wa Parc des Princes itachezwa bila ya mashabiki.

Imeelezwa kuwa maambukizi ya virusi vya corona yameendelea kwa kasi baada ya kuripotiwa kwa wagonjwa 7,375, ikiwamo vifo 366.

## ZISIKUPITE

### GREALISH AWINDWA

MANCHESTER United inajipanga kutoa kiasi cha pauni milioni 100 ili kumsajili kiungo wa Aston Villa na Timu ya Taifa ya England, Jack Grealish (24), na nyota anayekuja juu wa Birmingham, Jude Bellingham (16). ***(Star)***

### UNITED KUMUUZA LINGARD

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard, ambaye ana umri wa miaka 27, anajiandaa kuuzwa na klabu yake ya Manchester United katika kipindi cha majira ya joto. ***(Goal)***

### WILLIAN NJIA PANDA

WINGA wa Chelsea Mbrazil Willian (31), ameweka wazi kuwa hafahamu hatima yake ndani ya kikosi hicho kutokana na kutokuwapo kwa mazungumzo yoyote ya kusaini mkataba mpya baada ya awali kumalizika mwishoni mwa msimu. ***(Evening Standard)***

### ZAKARIA ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inaongoza katika mbio za kuwania saini ya kiungo mkabaji wa Borussia Monchengladbach na Timu ya Taifa ya Uswiswi, Denis Zakaria, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Star)***

### AGUERO AIVURUGA CITY

MANCHESTER City bado inamatumaini straika wake raia wa Argentina, Sergio Aguero (31), ambaye anashikilia rekodi ya kuwa kinara wa mabao ndani ya timu hiyo hatafanya mchakato wa kuondoka katika majira ya joto, licha ya kuwapo kwa adhabu ya kutoshiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Evening Standard)***

### STEGEN KUBAKI BARCA

BARCELONA inataka kumpa mkataba mpya golikipa wake Mjerumani Marc-Andre ter Stegen (27), ili kumaliza tetesi za kuondoka klabuni hapo baada ya kuwindwa na timu mbalimbali za Ulaya ikiwamo Chelsea. ***(Sport)***

### FLOYD AITAKA NEWCASTLE

BINGWA wa zamani wa ngumi za kulipwa, Floyd Mayweather ameweka wazi kwamba anataka kuinunua klabu ya Newcastle. ***(Newcastle Chronicle)***

### BEGOVIC ANUKIA INTER

INTER Milan inajiandaa kumsajili golikipa wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Bosnia, Asmir Begovic (32), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu ya AC Milan ili kurithi mikoba ya Samir Handanovic (35), katika msimu ujao. ***(La Repubblica, via Sempre Inter)***

### COURTOIS KUIKOSA UNITED

GOLIKIPA wa Real Madrid Mbelgiji Thibaut Courtois (27), huenda akawa nje katika mechi mbili ikiwamo ya hatua ya 16 Bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City kwa sababu ya kusumbuliwa na maumivu ya misuli kwenye mguu wake wa kushoto. ***(ESPN)***

### LEEDS, SOUTHAMPTON VITANI

LEEDS imeungana na Southampton kuwania saini ya beki wa Oxford, Rob Dickie, raia wa England ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

## Watumishi wahimizwa michezo

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WATUMISHI katika Halmashauri ya Manispaa ya Wilaya ya Ilemela jijini hapa wametakiwa kujitokeza kushiriki kwenye bonanza la michezo lililoandaliwa na halmashauri hiyo kwa ajili ya kuimarisha afya ili kuongeza ufanisi wa kazi.

Kauli hiyo imetolewa na Ofisa Utamaduni wa Manispaa ya Ilemela ambaye alikuwa mgeni rasmi wa bonanza la halmashauri hiyo, Ernest Biseko, aliyewataka watumishi hao kuitumia fursa hiyo ya kuimarisha afya zao.

Biseko alisema bonanza hilo sasa litakuwa likifanyika kila baada ya miezi mitatu na wanaamini litaimarisha viwango vya wafanyakazi wa halmashauri hiyo.

Alisema kwa kufanya mazoezi, wafanyakazi watajiepusha na watapambana na magonjwa yasiyoambukiza huku wakiimarisha afya ya akili.

"Niwapongeze kwa kujitokeza katika bonanza hili, lakini nawaomba tutumie michezo hii kwa kuimarisha afya zetu dhidi ya magonjwa na itusaidie kuongeza ufanisi pindi tunapokuwa tunatoa huduma kwa wananchi katika maeneo yetu ya kazi," alisema Biseko.

Katika mchezo wa soka, Watumishi wa Kata ya Pasiansi waliibuka kidedea kwa kuichapa timu ya Watumishi wa Kata ya Kayenze mabao 2-1 huku mpira wa pete Watumishi wa Makao Makuu waliwafunga wenzao wa Kata ya Nyakato.

# MORRISON AFUNGUKA KUENDELEZA MAZURI

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Bernard Morrison, amesema ataendelea kuifungia timu yake mabao muhimu katika mechi za Ligi Kuu Bara na mashindano ya Kombe la FA ili wafikie malengo waliyoyaweka katika msimu huu.

**Morrison alifunga bao pekee katika mechi ya watani wa jadi iliyochezwa Jumapili iliyopita na kuipunguza kasi Simba ambayo inapambana kutetea ubingwa wa ligi hiyo ambao wanaushikilia.**

Mshambuliaji huyo alisema alichokifanya mbele ya watani zao Simba ni sehemu ya ubora alionao na hali hiyo ilitokana na ushirikiano ambao ameupata kutoka kwa wachezaji wenzake na mashabiki wao waliojitokeza kwa wingi uwanjani.

Aliongeza kuwa ni kawaida yake kufunga aina ya mabao hayo, pia aliona kuna upenyo wa kupiga na kufanikiwa kufunga.

"Nafurahi kufanya kile ambacho ninakipenda, kiukweli tulijiandaa vizuri na kila mchezaji alikuwa tayari kuona tunashinda, hicho ndicho kimetokea, shukrani kwa mashabiki kwa sapoti waliyotuonyesha," alisema Morrison.

Alisema mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa kwa wapinzani wao kukosa nafasi nyingi na wao kutumia mapungufu ya Simba kupata ushindi huo.

Aliwataka mashabiki wa Yanga kuendelea kujitokeza katika mechi zinazofuata na wao watahakikisha hawatawaangusha kuelekea mbio za ubingwa wa Bara na mashindano ya Kombe la FA.

"Nina imani ushindi huu ni chachu ya kufanya vizuri kwa michezo yetu ijayo kwa kuhakikisha malengo yetu ya kumaliza ligi tukiwa katika nafasi mbili za juu," Morrison alisema.



Meya wa Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto (katikati), akiongoza mazoezi ya vikundi vya jogging vya vijana wa Kata ya Vingunguti, ambao mbali na mazoezi hushirikiana kutatua kero zinazoikabili kata hiyo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# *Manara, Bocco wawatuliza mashabiki*

**Na Somoe Ng'itu**

HUKU bado wakiwa na maumivu ya kufungwa na watani zao Yanga, nahodha wa Simba, John Bocco, amewataka mashabiki wa timu hiyo kutokata tamaa kwa sababu bado wao ndio wanaongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Bocco aliliambia gazeti hili kupoteza mechi dhidi ya Yanga sio mwisho wa ligi, na wao wataendelea kupambana kuhakikisha wanabakia kileleni hadi mwisho wa msimu.

Mshambuliaji huyo alisema mechi zote za ligi ni ngumu, hivyo mashabiki wafahamu huo ni mmoja kati ya michezo yenye changamoto iliyoko katika ligi, lakini bado Simba ina nafasi nzuri ya kutimiza malengo.

"Lengo kuu ni kutetea ubingwa, bado hatujatoka nje ya malengo, kweli inauma kufungwa na Yanga, lakini sio mwisho wa mapambano, tutawafurahisha," alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa Azam FC.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, aliwataka mashabiki wa klabu hiyo kuongeza utulivu kwa sababu nafasi waliyonayo katika msimamo wa ligi ni ya juu na si rahisi kuteremka.

Manara alisema huu si wakati wa kutafuta 'mchawi' na badala yake kujipanga kushinda mechi zao zinazofuata.

"Tumeumia, huu ndio mpira, kwa tamaduni zetu lazima tucharurwe kama ambavyo tungewacharura iwapo tungeshinda, lakini maisha lazima yaendelee, muhimu ni kujipanga kwa mchezo unaofuata kesho (leo), tusitoke katika reli na sote tunajua ubingwa uko mikononi mwetu, tusithubutu kumtafuta mchawi," Manara alisema.

Mabingwa na vinara hao wa Ligi Kuu Bara leo wanatarajia kuwakaribisha Singida United kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

# Tanzania yagawa dozi kwa Liberia

**Na Mwandishi Wetu**

YOSSO wa Tanzania wameanza vizuri mashindano maalumu ya soka la vijana wa umri chini ya miaka 16 (U-16), kwa kuwafunga wenzao wa Liberia mabao 3-0 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana.

Mashindano hayo yanayoshiriki nchi tatu za Malawi, Liberia na wenyeji Tanzania, ni maalumu kwa ajili ya kuziandaa timu hizo na michuano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Afrika kwa vijana wa umri chini ya miaka 17 (U-17).

Mabao yote ya timu ya Tanzania inayofundishwa na Kocha Mkuu, Maalim Saleh yalifungwa katika kipindi cha kwanza na Omar Abbas, Abdulrazak Salim na Ladak Juma.

Michuano hiyo itaendelea tena kesho kwa Liberia kuikabili Malawi na itamalizika Machi 14, mwaka huu kwa Malawi kuwavaa wenyeji Tanzania.

# Michezo

Jumatano Machi 11, 2020

Nipashe



Ligi Kuu Italia yapigwa 'stop'

UKURASA 30



Mchezaji wa Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 16 (U-16), Kassim Ibrahim (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Liberia katika mechi ya mashindano maalumu iliyofanyika kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. Tanzania ilishinda mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba, Singida mechi ya rekodi

## ●●● Msimbazi yajipanga kuendeleza ubabe na kujiimarisha katika mbio za ubingwa, huku Singida...

**Na Saada Akida**

HASIRA za kupoteza mechi dhidi ya watani zao Yanga, vinara Simba wanatarajia kumaliza 'machungu' yao katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida United itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Simba itashuka dimbani kupata pointi tatu na kurejesha furaha kwa mashabiki wao huku wakiendelea kujiimarisha kileleni wakati Singida United inayoburuza mkia yenyewe ikipambana kupata alama muhimu za kuwaondoa kwenye hatari ya kushuka daraja.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, alisema tayari ameyafanyia kazi mapungufu ya kikosi chake aliyoyabaini katika mechi iliyopita ili leo waondoke na pointi tatu na si matokeo mengine.

Sven alisema amewataka wachezaji wake kusahau matokeo ya mchezo uliopita na sasa kuimarisha nguvu na maandalizi ya mechi iliyoko mbele yao.

Kocha huyo alisema anahitaji kikosi chake kupambana na kujitolea kutafuta matokeo chanya kwa sababu nafasi ya kutimiza malengo yao bado haijakamilika.

"Sasa tunajipanga kwa michezo iliyobakia, matokeo yaliyopita yasitutoe katika malengo yetu, tunahitaji ubingwa na hilo vijana wangu wanatambua, sasa tupo tayari kutafuta pointi muhimu katika mchezo wetu wa kesho (leo)," alisema Sven.

Aliongeza anatambua ugumu uliopo katika ligi hiyo hasa wanapokutana na timu zilizoko katika nafasi za chini kwa sababu kwao mechi zote ni zaidi ya fainali.

"Tutaingia kucheza kwa tahadhari, tunajua Singida United ipo katika nafasi mbaya ya kushuka daraja, itacheza kwa bidii na itatupa ushindani, mechi haitakuwa rahisi kwao pia," alisema Sven.

Naye Kocha wa Singida United, Ramadhani Nswanzurwimo, alisema kikosi chake kipo vizuri na kimekuja Dar es Salaam kwa kazi moja ya kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo.

Nswanzurwimo alisema bado hajakata tamaa na wataendelea kupambana hadi mwisho kutafuta pointi katika mchezo wao wa leo na mingine itakayofuata ya ligi hiyo.

"Maandalizi yapo vizuri, tumejipanga kutafuta alama muhimu, tunafahamu tunakutana na timu nzuri, lakini pia imepoteza mechi yao iliyopita, hivyo mchezo utakuwa mgumu kwetu na kwao pia," Nswanzurwimo alisema.

Simba ambao ni mabingwa watetezi, inaongoza ligi ikiwa na pointi 68 wakati Singida United yenye pointi 12 inaburuza mkia.

# Kapombe arejea, Nyoni nje Stars

**Na Mwandishi Wetu**

BEKI mahiri wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Shomari Kapombe amerejeshwa katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), kitakachoingia kambini kujiandaa na mechi dhidi ya Tunisia itakayochezwa ugenini Machi 27, mwaka huu.

Kapombe alitangaza kujiuzulu kuichezea Taifa Stars kwa madai ya kutaka kupumzika ili kuimarisha afya yake baada ya kuandamwa na majeraha ya mara kwa mara.

Hata hivyo, Stars itakosa huduma ya beki mkongwe, Erasto Nyoni ambaye atakuwa nje kwa muda wa wiki mbili baada ya kuumia kifundo cha mguu katika mechi ya watani wa jadi iliyochezwa Jumapili iliyopita na Yanga kuibuka na ushindi wa bao 1-0.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema Kapombe amekubali kurejea katika kikosi hicho baada ya kufanya mazungumzo na viongozi wa benchi la ufundi la timu hiyo.

Ndimbo alisema Kapombe, beki huyo wa zamani wa Polisi Morogoro, ameridhia kurejea kufanya majukumu ya kitaifa na kuongeza kikosi hicho kitaingia kambini kesho.

Alitaja wachezaji wengine walioitwa katika kikosi hicho ni Robert Kisu (Gor Mahia), Metacha Mnata (Yanga), Aishi Manula (Simba), Salum Salula (Malindi), Kapombe, Mohammed Hussein, John Bocco, Hassan Dilunga na Jonas Mkude (Simba), Said Makapu, Juma Abdul, Kelvin Yondani, Ditram Nchimbi, Feisal Salum 'Fei Toto' na Balama Mapinduzi (Yanga).

Wachezaji wengine ni Kelvin Kijiri (KMC-U20), Nickson Kibabage, Simon Msuva, (Difffa el Jadida-Morocco), David Bryson (Gwambina -U-23), Bakari Mwamnyeto, Ayoub Lyanga (Coastal Union), Aggrey Morris, Suleiman Iddi 'Nado', Shaban Chilunda, Salum Aboubakar 'Sure Boy', Bryson Raphael (Azam FC), Six Sabilo (Polisi Tanzania), Farid Mussa, Lucas Kikoti , Reliants Lusajo (Namungo), Mbwana Samatta (Aston Villa), Himid Mao (Enppl, Misri) na Abdi Banda wa Highlandspark ya Afrika Kusini.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042